**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# TAARIFA YA UKAGUZI MAALUM ULIOFANYIKA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Barabara ya Samora na Ohio,
S.L.P. 9080,
Simu: 255 (022) 2115157/8,
Faksi: 255 (022) 2117527,
Barua pepe: ocag@nao.go.tz
Tovuti: www.nao.go.tz
**DAR ES SALAAM**.

**Desemba, 2011**

**YALIYOMO**

VIFUPISHO ........ iii
MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU YALIYOJITOKEZA (EXECUTIVE SUMMARY) ........ 1
1.0 Mifumo dhaifu ya udhibiti wa ndani ........ 1
2.0 Kutozingatia Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma ........ 3
3.0 Mishahara ya watumishi ambao hawako kazini kuwa katika orodha ya ........ 3
Mishahara ........ 3
4.0 Mapungufu katika Ukusanyaji wa Mapato toka Vyanzo vya Halmashauri ........ 4
5.0 Ubadhirifu wa Fedha za Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri ........ 4
6.0 MIRADI YA MAJI (NRWSSP) ........ 7
7.0 Mfuko wa Afya wa Pamoja ........ 8
8.0 Mapungufu katika Hati za Malipo zilizopatikana ........ 14
9.0 Kutokamilika kwa miradi ya ujenzi wa Maabara 21 iliyogharamiwa na LGCDG. 15
10.0 Mapungufu katika Kitengo cha Usafiri na Usafirishaji: ........ 15
11.0 Makato ya mishahara ambayo hayajalipwa kwenye Taasisi husika ........ 16
12.0 Sababu mbali mbali za ujumla zilizosababisha ubadhirifu wa fedha katika
Halmashauri: ........ 16
13.0 Mapendekezo ya jumla kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ........ 16
14 .0 Maeneo yenye ubadhirifu ........ 17
SURA YA KWANZA ........ 19
1.0 UTANGULIZI ........ 19
SURA YA PILI ........ 22
2.0 MAMBO YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI MAALUM ........ 22
SURA YA TATU ........ 129
3.1 KIINI CHA TATIZO ........ 129
SURA YA NNE ........ 131
4.0 MAFUNZO KUTOKANA NA HALI ILIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI HUU
MAALUMU ........ 131
SURA YA TANO ........ 133
5.0 MAPENDEKEZO ........ 133
SURA YA SITA ........ 140
6.0 HITIMISHO ........ 140

**VIFUPISHO**

| | |
|---|---|
| GN 97 | Public Procurement (Goods, works, non-consultant services and Disposal of Public Assets by Tender) Regulations, 2005 |
| GN No. 177 | Local Government Authorities Tender Boards (Establishment and Proceedings Regulations, 2007. |
| BoQ | Mchanganuo wa gharama za kazi (Bills of Quantity) |
| CHF | Mfuko wa Afya wa Jamii |
| LGDG | Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa |
| OWM-TAMISEMI | Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| MMAM | Mradi wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi |
| TACAIDS | Mradi wa Ukimwi |
| VVU | Virus vya Ukimwi |
| MESS | Mpango wa Elimu wa Shule za Sekondari |
| CHF | Mfuko wa Afya wa Jamii |

Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P 9120,
**DAR ES SALAAM.**

**TAARIFA YA UKAGUZI MAALUM ULIOFANYIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU**
**KWA KIPINDI CHA 2007/2008-2009/2010**

## MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU YALIYOJITOKEZA (EXECUTIVE SUMMARY)

Sehemu hii inaeleza kwa muhtasari mambo muhimu yaliyojitokeza katika Ukaguzi huu maalum. Wakati wa ukaguzi maalum katika Halmashauri ya Wilaya – Kishapu, tumebaini dosari na mapungufu mbalimbali ambayo maelezo ya kina yametolewa katika Aya husika. Masuala na mambo muhimu yanayohusiana na mapungufu hayo ambayo yamo katika taarifa hii ni haya yafuatayo:

### 1.0 Mifumo dhaifu ya udhibiti wa ndani

Katika kupitia mifumo ya udhibiti wa ndani na uhasibu, ukaguzi huu ulibaini mapungufu mbali mbali yaliyosababishwa na udhaifu wa mfumo wa ndani katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu . Pia kitengo cha Uhasibu kimekuwa hakina usimamizi na mgawanyo wa kazi nzuri hali ambayo imepelekea kutokea kwa mapungufu mengi kuhusiana na usimamizi wa rasilimali za Halmashauri kama ifuatavyo:

### 1.1 Mgawanyo wa kazi

Halmashauri haikuwa na mgawanyo wa kazi kimaandishi katika idara ya Uhasibu hivyo upotevu wa rasilimali za serikali na utendaji kazi uliochini ya kiwango stahiki haukuweza kugundulika na kuzuilika kwa muda muafaka.

Mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani, uliruhusu baadhi ya watendaji katika Idara ya uhasibu kufanya kazi ambazo zingekuwa nje ya majukumu ya kazi zao kwa mfano Mtunza fedha Ndugu Musa Limbe alitambulishwa Benki kushughulikia masuala yote ya fedha katika akaunti za Halmashauri katika Benki ya NMB Tawi la Manonga Mjini Shinyanga.

Hali hii ilisababishwa na kutotilia umuhimu wa kujenga mfumo imara wa udhibiti wa ndani kabla na baada ya kuanzishwa kwa Halmashauri mpya, ambapo Mweka Hazina wa Halmashauri alipaswa kuhakikisha kuwepo kwa mfumo makini wa udhibiti wa ndani na uwepo wa taratibu za kifedha

zilizoanishwa kwa uwazi kwa mujibu wa Agizo Na. 5(f) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mtaa ya Mwaka 1997.

### 1.2 Hati za malipo hazikuwa zinatunzwa vizuri

Hati za malipo zenye thamani ya Sh.1,171,735,534 zilizolipwa katika mwaka wa fedha 2009/2010 hazikuonekana wakati wa ukaguzi wa kawaida pia hazikuweza kupatikana hadi mwisho wa ukaguzi huu maalumu.

Ukaguzi ulibaini kuwa mpaka wakati wa ukaguzi huu maalumu hakuna Mhasibu aliyeteuliwa na Mweka Hazina kwa maandishi kuwajibika na utunzaji wa hati za malipo wala kuwepo sehemu maalum ya kuhifadhia hati za malipo, kwani kila Mhasibu anahifadhi Hati za malipo zinazohusiana na akaunti anayoisimamia, hivyo zinahifadhiwa sehemu tofauti katika Ofisi zao pasipo kuwepo na udhibiti wowote.

Uwezekano wa kuchukuliwa kwa hati za malipo na kila mhasibu ni mkubwa, hivyo udhibiti wake ni hafifu kwani hakuna “movement register” ya hati za malipo.

### 1.3 Kukosekana kwa mfumo Funganishi wa usimamizi wa Fedha (IFMS)

Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Halmashauri ilianza kutumia Mfumo wa Teknolojia ya Mawasiliano (Quick Use Accounting Package) kwa kusaidiwa na Afisa toka Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa, Mkoa wa Shinyanga Ndugu Monata ambaye aliiuzia Halmashauri Mfumo huo bila idhini ya TAMISEMI.

Mfumo huu haukidhi udhibiti wa matumizi ya fedha kwa maana matumizi yanapoidhinishwa hayaendani na fedha zilizopo katika kifungu husika cha matumizi hayo hivyo kufanya akaunti husika kutumia fedha zaidi ya kiasi kilichopo. Aidha, katika Mfumo huo hakuna mgawanyo wa majukumu ya kiutendaji ndani ya mfumo kwani mtumiaji mmoja amewezeshwa kufanya taratibu zote za malipo.

Hii ni dhahiri kwamba matumizi mabaya ya fedha za umma yanawezekana kutokea kupitia mfumo huo ambao hauna uthibiti wa kutosheleza mahitaji ya Halmashauri.

### 1.4 Utendaji kazi dhaifu wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani.

Ukaguzi huu maalum ulibaini kuwa Halmashauri tangu ilipoanzishwa mwaka 2005 ilikuwa haina mkaguzi wa ndani mpaka ilipofika Novemba, 2007 alipoteuliwa Ndg. Exaud Massawe – Mhasibu Daraja I kukaimu nafasi ya mkaguzi wa ndani. Hali hiyo imesababisha kuwa na mapungufu mengi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na malipo mbali mbali yaliyofanyika katika kipindi za mwaka 2005 hadi hapo alipoteuliwa Kaimu Mkaguzi wa Ndani.

Wakati wa ukaguzi maalumu ukifanyika, ilibainika kuwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani hakiandai Mpango wa kazi wa Ukaguzi wa mwaka na Mawanda ya utendaji wa mkaguzi wa ndani hayakuwa yameainishwa katika barua yake ya uteuzi. Hii ilisababisha mkaguzi wa ndani afanye kazi hata zile zisizomhusu kama vile ukaguzi wa awali wa hati za malipo (pre- audit) .

Kitengo cha ukaguzi wa ndani kushindwa kuisaidia Halmashauri kufikia malengo tarajiwa na kulinda maslahi ya Halmashauri kwa kutofanya kazi ambazo zitaisaidia Halmashauri katika kujua mapungufu mbalimbali kinyume na Agizo Na. 12 – 16 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1997.

## 2.0 Kutozingatia Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma

Katika kufanya tathmini ya taratibu za manunuzi kulingana na Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2005 ukaguzi huu maalumu umebaini kasoro na mapungufu yafuatayo:

Mkuu wa kitengo cha usimamizi wa manunuzi (PMU) kutoripoti moja kwa moja kwa Afisa Masuuli (Accounting Officer) na Mpango wa Mwaka wa Manunuzi kutofuata mwongozo (templates) zilizotolewa na PPRA. Pia, nyaraka za Zabuni mahsusi zenye viwango (Standard Tender Documents) hazitumiki.

Kinyume na kanuni Na.54 (1) ya G.N. Na. 97 ya mwaka 2005 Idara zinazofanya manunuzi huidhinisha nyaraka za zabuni (bidding documents) na aina za manunuzi (Procurement methods) badala ya kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni, kabla ya kutolewa kwa washindani (Wazabuni).

Kutokuwepo kwa taarifa za ukaguzi wa vifaa/bidhaa zilizonunuliwa kwani Afisa Masuuli hajateua Kamati za kukagua na kukubali (Goods Inspection/ (Acceptance Committee), kutokuwepo kwa taarifa za maendeleo na utekelezaji wa mikataba za siku, wiki na mwezi.

Uchambuzi wa Zabuni haufuati miongozo ya tathmini na mihtasari ya ufunguzi wa Zabuni haiambatanishwi (Evaluation Guidelines) inayotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) vilevile hakuna taarifa za uchambuzi. Pia, wakati mwingine wajumbe wa timu ya uchambuzi hawasaini fomu za kiapo (Covenant forms).

## 3.0 Mishahara ya watumishi ambao hawako kazini kuwa katika orodha ya Mishahara kiasi cha Sh.66,325,161.88

Katika kupitia malipo ya Mishahara ukaguzi maalumu uligundua kuwepo Mishahara ya watumishi ambao hawako kazini kuwa katika orodha ya

Mishahara kiasi cha Sh. 66,325,161.88. Kati ya kiasi hicho, Sh.43,854,576.66 zililipwa kwa watumishi ambao wamestaafu, kufariki, kufukuzwa kazi, kuacha kazi na kutoripoti kazini. Aidha kiasi cha Sh. 22,470,585.22 kilitokana na sababu za utoro ambapo hakuna hatua zozote stahiki za kinidhamu zilizochukuliwa na mamlaka za nidhamu. Hata hivyo, hakuna uthibitisho kuwa fedha hizi zinarudishwa Hazina kupitia Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa kama inavyotakiwa na waraka wenye kumb. Na. EB/AG/5/03/01/Vol. iv/136 wa tarehe 31/8/2007.

## 4.0 Mapungufu katika Ukusanyaji wa Mapato toka Vyanzo vya Halmashauri

Halmashauri haikuweza kutoa orodha ya mawakala waliopitishwa au kuidhinishwa na Halmashauri kwa miaka ya 2007/2008 na 2008/2009 ili kukusanya ushuru katika vyanzo vyake mbalimbali yakiwemo masoko na magulio ili iweze kupitiwa wakati wa Ukaguzi, pamoja na Ukaguzi kufatilia upatikanaji wa mikataba hiyo kwa Mwanasheria wa Halmashauri Bwana Peter Malembeka, Mhasibu wa Mapato Bwana Makokota Elbert na Mtunza Fedha Bwana Mtaki Masululi ambao walitakiwa kuiwasilisha Mikataba hiyo hawakuweza kuipata.

Katika kupitia mikataba ya 2009/2010 iliyowasilishwa haioneshi kumbukumbu namba za mikataba, pia haina dhamana ya usalama (Security Bond). Pia ukaguzi maalum umebani kuwa Halmashauri ilishindwa kukusanya mapato yatokanayo na masoko na magulio toka kwa Mawakala kiasi cha Sh.32,230,000.

## 5.0 Ubadhirifu wa Fedha za Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri

Timu ya ukaguzi haikupatiwa nyaraka ilizoomba kwa Meneja - NMB Tawi la Manonga kupitia Mkurugenzi wa Halmashauri kama Hundi zilizolipwa (paid cheques), orodha za watia sahihi katika akaunti za Halmashauri (Signature Specimen), Taarifa za Benki (Bank statements) na vyeti vya kuonesha Salio (Certificate of balances).
Orodha za watia sahihi wa akaunti 20 za Halmashauri zilizoko NMB, hazikuweza kutolewa na Meneja wa Benki kwa ajili ya ukaguzi. Aidha, hundi 158 zilishindwa kutolewa na benki kwa ajili ya ukaguzi.

Aidha, Meneja wa Benki kupitia Barua yake yenye kumbukumbu Na. NMB/KDC/AC/01/06 ya tarehe 21/06/2011 akijibu barua ya ukaguzi alieleza kuwa hatoweza kutoa nyaraka hizo, akidai kuwa taratibu za Benki hazimruhusu kutoa nyaraka hizo. Kukosekana kwa nyaraka hizo ukaguzi umeshindwa kujiridhisha na uhalali wa watia saini katika baadhi ya malipo.

Katika kupitia kumbukumbu za fedha zikiwemo daftari la fedha (Cash books), hundi zilizolipwa, taarifa za benki ilibainika kuwepo kwa ufujaji na ubadhirifu wa fedha kiasi cha Sh.5,513,049,264 zilizofanyika kwa njia mbali mbali kama inayooneshwa katika aya zifuatazo hapa chini:

### 5.1 Taarifa za benki zilizoghushiwa Sh.235,057,185.64

Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa taarifa za benki zilighushiwa na kutumika kufanya usuluhisho wa benki ambapo zilisainiwa na Mweka Hazina Ndugu Muhidini Mohamedi na kupelekea salio la akaunti hizo kuwa na tofauti ya Sh.235,057,185.64 ambazo tayari zilikuwa zimeshaibiwa toka katika akaunti hizo kwa njia za Malipo yasiyo na hati za malipo, kuongezwa kwa tarakimu katika hundi ikilinganishwa na vibutu, uhamishaji wa fedha usio na idhini ya Mkurugenzi kwenda katika akaunti ambazo ni rahisi kuzitoa isivyo halali, Malipo yaliyofanyika bila kuidhinishwa na Mkurugenzi na Malipo ya hundi zilizolipwa na Benki zikiwa zimesainiwa na maafisa ambao siyo walioidhinishwa kusaini hundi za akaunti husika, kughushiwa kwa sahihi za wahusika katika hundi zilizolipwa na benki na Hundi zilizooneshwa kufutwa katika vibutu (Cancelled) lakini zilioneshwa kulipwa na Benki.

### 5.2 Hundi zilizoghushiwa na kulipwa zaidi ikilinganishwa na vibutu Sh.502,155,820

Ukaguzi uliofanyika kwa kulinganisha rekodi za Halmashauri na zile za Benki, ulibaini kuwepo malipo kwa walipwaji mbalimbali katika Akaunti za CHF, Maendeeo, EGPAF, NRWSSP, TACAIDS NA DASIP yenye mashaka yenye jumla ya Sh.502,155,820 yaliyotokana na uwezekano wa kughushi hundi katika akauti mbalimbali za Halmashauri.

Hali hiyo ilitokana na kukosekana kwa baadhi ya watumishi wa Idara ya Fedha na maafisa wengine. Pia Udhaifu katika Mfumo wa udhibiti wa ndani wa Halmashauri ambapo Uhamishaji wa fedha usio na idhini na kibali cha Mkurugenzi uliweza kusaidia kufanya wizi wa fedha hizo bila kizuizi chochote kwa kushirikiana na watumishi/mtumishi wa Benki ya NMB tawi la Manonga. Hali hii ilisababisha kutotekelezwa kwa Shughuli zilizopangwa na Halmashauri kutotoa huduma bora kwa wananchi.

### 5.3 Uhamisho wa fedha toka Akaunti moja kwenda nyingine bila idhini ya Mkurugenzi na kutumika kinyume na malengo Sh.1,676,246,259

Katika kupitia hati za malipo na daftari la fedha kwa mwaka 2009/2010 ilibainika kuwa jumla ya Sh.1,676,246,259 zilihamishwa kutoka akaunti moja kwenda nyingine bila idhini ya Mkurugenzi na zikatumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa, kwani fedha hizi zilitakiwa kutumika katika akaunti husika kwa shughuli zilizokusudiwa na zilizoidhinishwa na bajeti ya Halmashauri.

Aidha, fedha hizi zilihamishwa kuziba mapengo kwenye akaunti ambazo fedha zake zilikuwa zimeshatumika kwa malengo yasiyokusudiwa au kuibwa

na watumishi wasio waaminifu ambao wametajwa katika aya namba 2.6 ya taarifa hii.

### 5.4 Uhamisho wa fedha ambao haukufika katika akaunti zilikohamishiwa Sh.1,957,659,279

Uchunguzi uliofanywa katika daftari la malipo (System Cash Books) na taarifa za Benki (Bank Statements) katika mwaka wa fedha 2009/2010 ilibainika kuwa Halmashauri ilifanya uhamisho wa fedha wenye jumla ya Sh.1,957,659,279 Kutoka akaunti moja kwenda nyingine na fedha hizi zilioneshwa kulipwa na Benki kutoka akaunti iliyohamisha.

Aidha, ukaguzi ulipofatilia uhamishaji huo wa fedha katika taarifa za Benki (Bank Statement) na kitabu cha fedha (Cash Book) upande wa mapokezi wa akaunti zilikohamishiwa fedha hizo hazikuwa zimepokelewa, hali hii inabainisha kuwa kiasi cha Sh.1,957,659,279 kilichukuliwa fedha taslimu na watumishi Halmashauri wakishirikiana na watumishi wa Benki wasio waaminifu ambao wametajwa katika matukio ya ubadhirifu yaliyoainishwa katika aya namba 2.6 ya taarifa hii.

### 5.5 Uhamisho wa fedha kwenda kwenye akaunti zisizofahamika Sh.452, 379,678

Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Halmashauri ilifanya uhamisho wa fedha wenye jumla ya Sh.452, 379,678 kutoka akaunti moja kwenda katika akaunti zisizofahamika.

Uchambuzi uliofanywa katika daftari za malipo (System Cash Books) na taarifa za Benki (Bank Statements) za akaunti zilizolipa zikionesha kutoa fedha hizo lakini zilipofuatiliwa katika daftari za fedha na taarifa za benki fedha hizo hazikuonesha kupokelewa katika akaunti yeyote au kutumika kama matumizi halali ya Halmashauri.

Hivyo kiasi cha fedha chenye jumla ya Sh. 452,379,678 kilichohamishwa toka akaunti moja kwenda kusikojulikana zilichukuliwa fedha taslimu na Mtunza Fedha wa Halmashauri akishirikiana na watumishi wa Benki.

### 5.6 Malipo yaliyofanyika kwa walipwaji wasiofahamika Sh.689, 551,042

Katika kupitia daftari la fedha (cash books) na taarifa za Benki (Bank statements) za mwaka 2009/2010 kulibainika kuwepo kwa malipo yenye jumla ya Sh.689,551,042 yaliyofanyika benki kwa walipwaji wasiojulikana ambao hawakutajwa majina yao. Malipo hayo yaliingizwa katika daftari la fedha ikiwa ni kusuluhisha malipo yaliyoghushiwa ambayo yalilipwa na Benki toka akaunti mbalimbali za Halmashauri. Halmashauri imeweza kuibiwa fedha nyingi kupitia kwa watumishi wa Halmashauri Bw. Walugu Mussa Limbe

ambaye alikuwa Mtunza Fedha na Mweka Hazina Bw. Muhidini Muhamed wakishirikiana na watumishi wa Benki ya NMB Tawi la Manonga. Halmashauri inatakiwa kuwachukulia hatua za kisheria watumishi hao ambao walihusika katika ubadhirifu huo wa fedha.

## 6.0 MIRADI YA MAJI (NRWSSP)

### 6.1 Fedha ambazo hazikuhamishiwa toka akaunti ya Maendeleo kwenda akaunti ya mradi Sh.88,700,000

Mnamo tarehe 10/12/2009 Halmashauri ilipokea kupitia akaunti ya Maendeleo kiasi cha Sh.88, 700,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za miradi ya Maji. Wakati wa ukaguzi maalum uliofanyika mwezi Juni 2011 takribani miezi sita tangu kupokelewa fedha hizo zilikuwa hazijahamishwa katika akaunti ya mradi wa Maji wa NRWSSP ili zitumike kwa shughuli za mradi zilizokusudiwa.

### 6.2 Matumizi yaliyofanywa kinyume na Malengo yaliyokusudiwa Sh. 338,974,569.14

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu Na.DED/KDC/CPF.8/05 ya tarehe 19/10/2010 iliyoandikwa na Mhandisi wa Maji Wilaya Ndugu Said Lukas kwenda kwa Mkurugenzi wa Halmashauri yenye kichwa cha habari "Matumizi ya Fedha za Programme ya Maji kinyume na malengo yaliyokusudiwa" ikitanabaisha kuwepo kwa matumizi yenye jumla ya Sh.286,092,000 yaliyofanyika kupitia akaunti ya Benki kwa matumizi yasiyokusudiwa na Idara ya Maji kama mtumiaji na msimamiaji wa Mradi haikuhusishwa, ikimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri afanye uchunguzi wa ubadhirifu huo. Lakini mpaka tarehe za ukaguzi huu maalum hakuna hatua yoyote iliyokuwa imechukuliwa na Uongozi wa Halmashauri dhidi ya barua hiyo.

Katika mahojiano na Mhandisi wa Maji, alisema kuwa kulikuwa na matumizi mengine zaidi ya yaliyotajwa katika barua yake yenye jumla ya Sh. 52,882,569.14 ambayo pia yalifanyika benki kwa matumizi yasiyokusudiwa na Idara ya Maji kama mtumiaji na msimamiaji wa Mradi hakuhusishwa hivyo kufanya matumizi yaliyofanywa nje ya malengo ya mradi kuwa jumla ya Sh.338, 974,569.14 kutokana na taaarifa za benki (Bank statements).

Ukaguzi ulipofuatilia ili kupata Hati za malipo husika kuweza kubainisha malipo hayo yaliidhinishwa na nani na yalikuwa yanahusu nini hazikuweza kutolewa na uongozi wa Halmashauri na hivyo kushindwa kutoa maelezo yanayoeleweka kuhusu hoja hii.

### 6.3 Taarifa za benki zilizoghushiwa Sh.106,092,000

Timu ya Ukaguzi katika kupitia na kufanya ulinganisho wa taarifa za benki (Bank Statements) pamoja na cheti cha Salio (Certificate of Balance) ya akaunti ya RWSSP kwa 2008/2009 ambazo ilizipata toka NMB Tawi la Manonga na kuoanisha na zile zilizotumika kufanya usuluhisho wa benki na

kufunga hesabu za mwisho za mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2009 iligundulika kuwa zimeghushiwa na kusainiwa na Mweka Hazina Ndugu Muhidini Mohamedi na kupelekea salio la akaunti hiyo kuwa na tofauti ya Sh.106,092,000 ambazo tayari zilikuwa zimeshaibwa toka katika akaunti hiyo ikiwa ni malipo yaliyofanyika benki bila kuwa na hati za malipo.

### 6.4 Hundi zilizoghushiwa na kulipwa zaidi ikilinganishwa na vibutu Sh.69,487,000

Ukaguzi uliofanyika kwa kulinganisha rekodi za Halmashauri na zile za Benki, ulibaini kuwepo malipo yenye mashaka yaliyaotokana na kugushiwa kwa hundi katika akaunti namba 30712000113. Malipo hayo ni kama ifuatavyo:

| Na. | Mlipwaji | Namba ya Hundi | Kiasi cha malipo kwenye vitabu vya malipo ( Sh.) | Tarehe ilipolipwa benki | Kiasi cha malipo kwenye Hundi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | DED – Kishapu | 114613 | 895,000 | 8/4/2009 | 15,000,000 |
| 2 | DED – Kishapu | 114614 | 161,630 | 09/3/2009 | 15,000,000 |
| 3 | DED – Kishapu | 114619 | 90,000 | 11/4/2009 | 20,000,000 |
| 4 | DED – Kishapu | 114620 | 625,000 | 01/6/2009 | 19,487,000 |
| **Jumla** | | | **1,771,630** | | **69,487,000** |

Hundi No.114614 inaonesha kwenye vitabu vya malipo (Cash book) kuwa ilifutwa (Cancelled) na kukatiwa risiti namba 0126862 tarehe 30/8/2009 lakini katika taarifa za benki (Bank statement) inaoneshwa ililipwa tarehe 09/03/2009.

### 6.5 Shughuli zilizoathirika na ubadhirifu wa fedha za Mradi wa Maji

Shughuli zenye jumla ya Sh.176,569,400 ziliathirika kutokana na ubadhirifu wa fedha za mradi. Halmashauri ilishindwa kumlipa mzabuni M/S Netwas Tanzania LTD kwa Mkataba Na.LGA/108/NRWSSP/01 kiasi kilichobakia cha malipo ya Dola za Kimarekani 108,725 sawa na shilingi 176,569,400 za Tanzania (Dola 1 ya Marekani sawa na Sh.1624 za Tanzania) ambazo zimetoweka katika akaunti ya mradi huo kutokana na ubadhirifu, hivyo kukwamisha maendeleo ya mradi katika awamu ya pili.

## 7.0 Mfuko wa Afya wa Pamoja

### 7.1 Fedha ambazo hazikuhamishwa toka akaunti ya Maendeleo kwenda akaunti ya Afya Sh.244, 358,000

Ilibainika kuwa tarehe 10/9/2009 Halmashauri ilipokea kiasi cha Sh.244, 358,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Afya. Wakati wa

ukaguzi huu maalum uliofanyika mwezi Juni 2011 fedha hizo zilikuwa hazijahamishiwa katika akaunti ya Afya ili zitumike kwa shughuli za mradi zilizokusudiwa na fedha hizo ziliibwa toka akaunti ya maendeleo kwa njia mbali mbali kama zilivyoainishwa katika aya ya 2.6 ya taarifa hii.

Aidha, kwa kutokuhamisha fedha hizo toka akaunti ya Maendeleo kwenda akaunti Afya Halmashauri haikuweza kutekeleza kikamilifu shughuli zenye jumla Sh. 244,358,000 zilizoainishwa katika Mpango Kazi wa mwaka 2009/2010.

Pia, ilibainika kuwa jumla ya Sh.183,288,230 zilihamishwa kutoka akaunti ya Afya kwenda katika akaunti mbalimbali bila idhini ya Mkurugenzi wa Halmashauri.

## 7.2 Mradi wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM)

### 7.2.1 Fedha ambazo hazikuhamishiwa toka akaunti ya Maendeleo kwenda akaunti ya mradi wa MMAM Sh.338,372,112

Kiasi cha Sh.338,372,112 zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Afya ya Msingi (MMAM) mpaka wakati wa ukaguzi huu mwezi June 2011 takribani miezi 16-27 tangu kupokelewa katika akaunti ya Maendeleo fedha hizo zilikuwa hazijahamishiwa katika akaunti ya Afya ili zitumike kwa shughuli za mradi zilizokusudiwa.

Timu ya ukaguzi maalum ilibaini Hati ya malipo Na. 6/10 /2009 na hundi Na. 113874 ikionesha kuhamisha fedha Sh. 81,730,026 kutoka akaunti ya maendeleo kwenda akaunti ya Afya. Kiasi hicho cha fedha zilizoombwa kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/BS/2 VOL/34 tarehe 21/10/2009 na baadaye kukatiwa stakabadhi Na.0126666 ya terehe 26/10/2009 ili kuficha ukweli, katika kufuatilia uhamishaji huo, timu ya ukaguzi ilibaini kutohamishwa kwa fedha hizo kwani hundi hiyo haikuwasilishwa benki.

Pia katika kupitia taarifa za utekelezaji za Mwaka 2009/2010 ilibainika kuwa shughuli zenye jumla ya Sh.145,914,235 ziliathirika kutokana na ubadhirifu wa fedha za mradi hivyo kuifanya Halmashauri kushindwa kutekeleza shughuli zilizokusudiwa.

### 7.2.2 Ukiukaji wa miongozo na taratibu za Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi – MMAM/JRF

Halmashauri ya Kishapu katika mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010 ilipokea jumla ya Sh.338,372,112 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa pamoja wa ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya (JRF)/ Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi(MMAM). Aidha, kinyume na mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM- TAMISEMI) rekebisho la mwezi Agosti 2006, sehemu ya pili

kipengele cha 11 na 21 cha mfuko, Halmashauri haikupeleka fedha hizo katika akaunti za Kamati za Afya za Vituo na badala yake Halmashauri iliingia mikataba ya ukarabati wa Vituo vya Afya na Zahanati bila kuzishirikisha Kamati za Afya za Vituo ambapo ni kinyume kabisa na taratibu zilizopo.

### 7.3 Mradi wa Ukimwi (TACAIDS)

Katika kupitia nyaraka mbalimbali zikiwemo taarifa za Benki, hundi zilizolipwa, vibutu vya hundi, mipango kazi na taarifa za utekelezaji zinazohusu mapato na matumizi ya fedha za mradi wa Ukimwi (TACAIDS) ukaguzi uligundua kuwepo ubadhirifu wa jumla ya kiasi cha Sh. 227,752,000 wa fedha za mradi uliofanywa na watumishi wa Halmashauri akiwemo Mtunza Fedha wa Halmashauri ambao wametajwa katika kila tukio la ubadhilifu kama ifuatavyo:

#### 7.3.1 Fedha ambazo hazikuhamishwa kwenda katika akaunti ya mradi Sh. 53,202,000

Ilibainika kuwa kiasi cha Sh.53,202,000 zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Ukimwi kwa maana ya TACAIDS na Global Fund mpaka wakati wa ukaguzi huu mwezi June 2011 takribani miezi 12-24 tangu kupokelewa kwa fedha hizo katika akaunti ya Maendeleo hazijahamishiwa katika akaunti ya Ukimwi ili zitumike kwa shughuli za mradi zilizokusudiwa.

Pia, katika kupitia daftari la fedha 2009/2010 ilibainika jumla ya Sh.66,700,000 zilihamishwa kutoka akaunti ya Ukimwi Na.3071200102 kwenda katika akaunti mbalimbali bila idhini ya Mkurugenzi wa Halmashauri kama ilivyoainishwa katika aya namba 2.6.4.

#### 7.3.2 Malipo yasiyojulikana kwa walipwaji wasiojulikana Sh.20,800,000

Katika kupitia daftari la fedha la mwaka 2009/2010 ilibainika jumla ya Sh. 20,800,000 zililipwa kutoka akaunti ya Ukimwi Na. 3071200102 ikiwa ni malipo yasiyojulikana kwa walipwaji wasiojulikana bila idhini ya Mkurugenzi wa Halmashauri ambayo yalihusisha malipo yaliyofanyika bila hati za malipo, kulipwa kwa hundi zilizofutwa lakini zikalipwa na Benki, malipo yaliyolipwa zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa katika hati za malipo n.k.

Vile vile malipo haya yamehusisha malipo ya hundi zilizolipwa na benki wakati zikiwa zimesainiwa na watia sahihi ambao siyo walioidhinishwa.

#### 7.3.3 Hundi zilizoghushiwa na kulipwa zaidi ikilinganishwa na vibutu Sh.42,450,000

Ukaguzi uliofanyika kwa kulinganisha rekodi za Halmashauri na zile za Benki, ulibaini kuwepo malipo nyenye mashaka yaliyotokana na kugushiwa hundi katika akaunti namba  30712000102. Malipo hayo ni kama yafuatayo:

| Na. | Mlipwaji | Namba ya Hundi | Kiasi cha malipo kwenye vitabu vya malipo | Tarehe ilipolipwa benki | Kiasi cha malipo kwenye Hundi Sh |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | DED - Kishapu | 005688745 | 250,000 | 20/6/2009 | 16,250,000 |
| 2 | DED - Kishapu | 005688746 | 100,000 | 2/6/2009 | 10,000,000 |
| 3 | DED - Kishapu | 005688747 | 110,000 | 14/6/2009 | 11,000,000 |
| 4 | DED - Kishapu | 005688749 | 200,000 | 12/6/2009 | 5,200,000 |
| **Jumla** | | | **660,000** | | **42,450,000** |

Aidha, katika kupitia taarifa za utekelezaji za mwaka 2009/2010 ilibainika kuwa shughuli za Global Fund na Ukimwi(TACAIDS) zenye jumla ya Sh.57,454,000 ziliathirika kutokana na ubadhirifu wa fedha za mradi hivyo Halmashauri kushindwa kutekeleza shughuli zake kama zilivyokusudiwa.

## 7.4 Mradi wa Elizabeth Glacier Paediatric Aids Funds (EGPAF)

Katika kupitia nyaraka mbalimbali zikiwemo taarifa za Benki, hundi zilizolipwa, vibutu vya hundi, mipango kazi na taarifa za utekelezaji zinazohusu mapato na matumizi ya fedha za mradi wa Elizabeth Glacier Paediatric Aids Funds (EGPAF) ukaguzi uligundua kuwepo ubadhirifu wa jumla ya kiasi cha Sh.81,628,000 wa fedha za mradi uliofanywa na watumishi wa Halmashauri ambao wametajwa katika kila tukio la ubadhirifu.

Katika kupitia daftari la fedha la mwaka 2009/2010 ilibainika jumla ya Sh.53,000,000 zilihamishwa kutoka akaunti ya Elizabeth Glacier Paediatric Aids and Funds (EGPAF) Na. 3071200119 kwenda katika akaunti mbalimbali bila idhini ya Mkurugenzi wa Halmashauri. Aidha, fedha hizi zilihamishwa kuziba mapengo kwenye akaunti ambazo fedha zake zilikuwa zimeshatumika kwa malengo yasiyokusudiwa au kuibwa na watumishi wasio waaminifu ambao wametajwa katika matukio hayo ya ubadhirifu yaliyoainishwa katika aya namba 2.6.4 ya taarifa hii.

Vile vile, ukaguzi uliofanyika kwa kulinganisha rekodi za Halmashauri na zile za Benki, ulibaini kuwepo malipo yenye mashaka yaliyotokana na kugushiwa kwa hundi katika akaunti namba 30712000119 kwa kulipwa zaidi ikilinganishwa na vibutu kiasi cha Sh.28,628,000. Malipo hayo ni kama ifuatavyo:

| Na. | Mlipwaji | Namba ya Hundi | Tarehe iliyolipwa Benki | Kiasi cha malipo kwenye Kibutu na vitabu vya malipo | Kiasi cha malipo kwenye Hundi Sh |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KDC | 112066 | 29/4/2009 | Ilifutwa | 28,628,000 |
| | **Jumla** | | | | **28,628,000** |

Hundi Na. 112066 inaonesha kwenye vitabu vya malipo (Cash book) na vibutu kuwa ilifutwa (Cancelled) lakini katika taarifa za benki (Bank Statements) inaoneshwa imelipwa jumla ya Sh.28,628,000 tarehe 29/04/2009.

### 7.5 Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)

#### 7.5.1 Utunzaji wa hesabu zinazohusiana na mapato ya Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)

Kwa mujibu wa barua yenye Kumb. Na. KDC/CHF/VOL.1/1/39 ya tarehe 15/3 2008 ikieleza kuwa Halmashauri ilipata mgawo wa kiasi cha Sh. 27,000,000 uliotoka Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini mwezi Februari 2008, ukaguzi ulipofuatilia mapokezi ya fedha hizi haikuweza kufahamika zilipokelewa katika akaunti ipi ya Halmashauri kwani katika taarifa za Benki akaunti ya CHF hazikuonekana.

Katika kupitia nyaraka mbalimbali zikiwemo taarifa za Benki, Hundi zilizolipwa, vibutu vya hundi, mipango kazi na taarifa za utekelezaji zinazohusu mapato na matumizi ya fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ukaguzi uligundua kuwepo ubadhirifu wa jumla ya kiasi cha Sh.213,565,500 wa fedha za mradi uliofanywa na watumishi wa Halmashauri ambao wametajwa katika kila tukio la ubadhilifu kama ifuatavyo:

#### 7.5.2 Matumizi ya Fedha ya mfuko yasiyoidhinishwa na kwa malengo yasiyokusudiwa Sh.126,806,000

Kinyume na Kanuni za mfuko wa Afya ya jamii, matumizi yenye jumla ya Sh.126,806,000 yalifanyika kulipia matumizi mbalimbali yasiyolenga malengo ya Mfuko wa Afya ya Jamii kinyume na Kifungu Na. 5 cha Sheria ndogo ya Mfuko wa Afya ya Jamii kinachosisitiza matumizi yafanyike katika nyanja zifuatazo:

- Kutoa huduma bora ya Afya ya jamii kwa wanachama.
- Kuboresha huduma za Afya kwa jamii kwa kugawa madaraka na kuiwezesha jamii kutoa maamuzi katika mambo yanayoathiri afya ya jamii.

### 7.5.3 Uhamishaji wa fedha bila idhini Sh.12,358,000

Katika kupitia daftari la fedha 2009/2010 ilibainika jumla ya Sh.12,358,000 zilihamishwa kutoka akaunti ya CHF Na. 3071200091 kwenda katika akaunti mbalimbali bila idhini ya Mkurugenzi wa Halmashauri kama inavyooneshwa hapo chini:

| Tarehe | Nambari ya hati | Namba ya Hundi | Akaunti zilikohamishiwa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 16/10/2009 | GLP02467 | 108664 | G/Fund | 358,000 |
| 02/12/2009 | GLP02468 | 108666 | Barabara | 12,000,000 |
| **Jumla** | | | | **12,358,000** |

### 7.5.4 Hundi zilizoghushiwa na kulipwa zaidi ikilinganishwa na vibutu Sh.53,621,500

Ukaguzi uliofanyika kwa kulinganisha Daftari la fedha (Cash book) taarifa za Benki (Bank Statements) na hundi zilizolipwa (paid cheques), ulibaini kuwepo malipo yenye mashaka yaliyotokana na uwezekano wa kughushi hundi katika akaunti namba 30712000091 – CHF. Malipo hayo ni kama ifuatavyo:

| Na. | Mlipwaji | Namba ya Hundi | Kiasi cha malipo kwenye Hundi na vitabu vya malipo | Kiasi cha malipo kwenye Hundi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Amazon Stationary | 108662 | 200,000 | 14,620,000.00 |
| 2. | DED- KDC | 108663 | 640,000 | 6,118,000.00 |
| 3. | DED- KDC | 108651 | | 13,626,000.00 |
| 4. | DED- KDC | 108658 | | 19,257,500.00 |
| **Jumla** | | | | **53,621,500.00** |

Hundi Na. 108651 na 105658 zinaoneshwa kwenye vitabu vya malipo (Cash Book) na vibutu kuwa zilifutwa (Cancelled) lakini katika taarifa za benki (Bank Statements) inaoneshwa zililipwa tarehe 16/10/2007 na tarehe 12/03/2008.

### 7.5.5 Taarifa za benki zilizoghushiwa Sh.20,780,000

Katika kupitia na kufanya ulinganisho wa taarifa za benki (Bank Statements) pamoja na cheti cha Salio (Certificate of Balance) ya akaunti hiyo kwa mwaka 2008/2009 ambazo timu ya ukaguzi ilizipata toka NMB Tawi la Manonga na ile iliyotumika kufunga hesabu za mwisho za mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2009 ilibainika kuwa imeghushiwa na kutumika kufanya usuluhisho wa benki ambao ulisainiwa na Mweka Hazina Ndugu Muhidini

Mohamedi na kupelekea salio la akaunti hiyo kuwa na tofauti ya Sh. 20,780,000 ambazo tayari zilikuwa zimeshaibiwa toka katika akaunti hiyo ikiwa ni malipo yaliyofanyika benki bila kuwa na hati za malipo wala hundi kama inavyoonesha hapa chini:

| Namba ya akaunti | Jina la akaunti | Salio halisi (Sh) | Salio lililoghushiwa (Sh) | Tofauti (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| CA 3071200091 | CHF | 178,325.75 | 20,958,325.75 | 20,780,000 |
| **Jumla** | | | | **20,780,000** |

## 8.0 Mapungufu katika Hati za Malipo zilizopatikana

### 8.1 Hati za Malipo ambazo hazikuidhinishwa Sh.221,805,777.43

Katika kupitia hati za malipo, ilibainika kwamba hati za malipo zenye thamani ya Sh. 221,805,777.43 hazikuidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ambaye kwa mujibu wa kifungu namba 33 cha Sheria ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 yeye ndiye Afisa Masuuli ambapo malipo yote yanatakiwa ayaidhinishe. Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2009 aliyekuwa Mhasibu wa TASAF kwa kipindi hicho Bwana H. Makokola hakusimamia vizuri utaratibu wa uidhinishaji hivyo hati hizo malipo hazikuwa zimesainiwa na Mkurugenzi. Aidha, kwa mujibu wa Mweka Hazina wa sasa Bwana Oscar Msalikwa na Mhasibu wa TASAF Bwana Masatu E. Mnyoro malipo hayo yalifika kule yalikokusudiwa kwa shughuli mbalimbali baada ya kufanya ufuatiliaji.

Ukaguzi maalum ulibaini pia kiasi cha Sh. 12,050,000 kililipwa kama fidia kwa wamiliki wa eneo ambalo limetwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda katika akaunti ya Ardhi. Katika kupitia orodha ya malipo hakukuwa na uthibitisho wa Mtendaji wa Kijiji kuthibitisha utambuzi wa wafidiwa halali.

### 8.2 Mapungufu ya nyaraka na Udhaifu katika usimamizi wa Mikataba yenye jumla ya Sh.4,258,312,634

Katika mafaili ya Miradi ambayo ilichaguliwa kwa ajili ya uhakiki yenye thamani ya Sh. 4,258,312,634 yalibainika kuwa na mapungufu ya nyaraka muhimu hivyo kuzuia ukaguzi kupata taarifa na takwimu muhimu zinazohusu miradi, katika maeneo ya usimamizi wa miradi na mikataba, usahihi wa malipo kwa wakandarasi na uhalali wa malipo ya ongezeko la gharama za bei za mikataba kulitokana na kutokuwemo kwa nyaraka na mapungufu mbalimbali katika mafaili husika.

## 9.0 Kutokamilika kwa miradi ya ujenzi wa Maabara 21 iliyogharamiwa na LGCDG

Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Halmashauri ya wilaya ya Kishapu ilipeleka Sh.260,803,765 katika Kata 20 kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa Maabara 21 za shule za Sekondari. Maabara hizo zilipangwa kujengwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilihusu ujenzi wa msingi na sehemu ya ukuta kabla ya lenta. Katika awamu ya pili ya ujenzi wa Maabara, Halmashauri ilingia mikataba na wakandarasi ambayo ilijumuisha ujenzi wa ukuta tokea madirishani, lenta, uezekaji wa mabati, uwekaji wa milango na madirisha, sakafu na kupaka rangi ndani na nje. Kati ya maabara hizo 21, Maabara 12 zilitembelewa na timu ya ukaguzi maalum. Kati ya hizo 12, maabara 11 hazikuwa zimekamilika katika viwango mbalimbali. Maabara moja tu ya shule ya Sekondari Mipa, ndiyo ambayo ujenzi wake ulikuwa unaridhisha kulingana na mkataba.

**Mapungufu ya jumla katika Miradi ya Ujenzi**

- Ukaguzi uligundua uwepo wa maongezeko ya kazi katika miradi mbalimbali ambayo yanatokana na aidha ukosefu wa umakini au wa makusudi katika kuandaa makadirio ya kazi na gharama (BOQs), hivyo kukosekana ushindani katika kazi hizo.
- Katika miradi ambayo imeelekezwa kwa jamii ilionekana kuwa Ushirikishwaji wa Watumiaji wa miradi husika ni mdogo hasa katika miradi iliyokwenda katika shule mbalimbali.
- Uchelewaji mkubwa wa ukamilishaji wa miradi ambao unatokana na wakandarasi kuchelewa kulipwa kwa kisingizio cha kuchelewa kwa fedha lakini hali halisi ni kutokana na ubadhirifu wa fedha za miradi husika kama ilivyoainishwa katika Aya 2.6.4 ya taarifa hii.

## 10.0 Mapungufu katika Kitengo cha Usafiri na Usafirishaji:

Timu ya ukaguzi maalum iligundua kuwa Halmashauri ina kitengo cha Usafirishaji lakini Afisa Usafirishaji hatumiwi ipasavyo katika majukumu yanayomhusu kama vile kufuatilia mienendo ya matumizi ya Mafuta kwa kutoa vibali vya mafuta, kuratibu Matengenezo ya Magari, kuratibu safari za magari na ununuzi wa vipuri yakiwemo matairi na usalama wa magari badala yake majukumu hayo yanafanywa na Wakuu wa Idara wenye magari badala ya Afisa Usafirishaji hivyo kupelekea magari kutumika pasipo udhibiti wowote.

Katika kupitia leja za mafuta kwa mwaka 2008/2009 na 2009/2010 ukaguzi ulibaini kuwepo kwa salio la mafuta yenye thamani ya Sh.42,198,300 lakini kimsingi mafuta hayo hayakuwepo na yalikwishatumika ila taarifa za matumizi ya mafuta haikuonyeshwa katika leja ya mafuta.

## 11.0 Makato ya mishahara ambayo hayajalipwa kwenye Taasisi husika

Katika kupitia Hesabu za mwaka 2009/2010 akaunti ya Amana (Deposit), orodha ya mishahara na kulinganisha na daftari la fedha (Cash Book) ilibainika kuwa kiasi cha Sh.281,954,806.30 ikiwa ni makato ya mishahara ya watumishi ambayo hayakuwasilishwa katika Taasisi husika kinyume na Agizo Na. 309 la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 1997 na Fedha hizi kutumika katika matumizi mengine.

## 12.0 Sababu mbali mbali za ujumla zilizosababisha ubadhirifu wa fedha katika Halmashauri:

- Katika hali isiyo ya kawaida Mtunza fedha (Cashier) Ndugu Walumu Musa Limbe ambaye cheo chake ni Mhasibu Msaidizi na elimu yake ni kidato cha IV alitambulishwa kwa meneja wa Benki na kuidhinishwa kwa barua isiyo na kumbukumbu Namba ya tarehe 20/07/2005 iliyoandikwa na Mkurugenzi Mtendaji kwenda kwa Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Manonga, iliyompa mamlaka ya kushughulikia masuala yote yanayohusu fedha katika akaunti za benki. Kwa idhini hiyo, aliweza kufanya kazi za kuweka na kutoa fedha katika Benki kwa wakati wowote bila kizuizi na alitumia mwanya huo kuchota fedha za Halmashauri kwa kushirikiana na watumishi wengine wa Halmashauri pamoja na Benki.
- Mabadiliko ya uongozi ya mara kwa mara katika vipindi vifupi vifupi. Pamoja na kuwa Halmashauri ilikuwa mpya, mabadiliko haya hayakuwawezesha wale waliokuwa na nyadhifa mbalimbali katika Halmashauri, kujenga mfumo wa kudumu na imara wa udhibiti wa ndani na kuhakikisha unaendelezwa, kwa sababu ya kutokuwepo kwa kipindi kirefu kwenye nafasi yoyote kikazi na hivyo kukosa uendelezaji wa yaliyoanzishwa (Continuty).
- Mapungufu na udhaifu wa udhibiti wa ndani na kutokuwepo kwa mfumo Funganishi wa Usimamizi wa Fedha- IFMS na kutokuwepo kwa mgawanyo wa kazi za wahasibu unaokidhi uwiano wa mgawanyo wa majukumu yanayomfanya mhasibu mmoja asiwe na kazi za mwendelezo zinazoweza kumpa nafasi ya kufanya ubadhirifu bila kugundulika.

## 13.0 Mapendekezo ya jumla kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu

Kufuatia mambo yaliyoonekana wakati wa ukaguzi huu maalum ikiwa ni pamoja na hatua za kiutawala na kisheria zitakazochukuliwa dhidi ya wahusika na Mamlaka husika, nashauri mambo yafuatayo kwa ajili ya kuboresha hali ya utendaji kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu:

- Halmashauri inatakiwa kuimarisha udhibiti wa ndani ili kupunguza au kuondoa kabisa ubadhirifu wa fedha kwa kuwa na mgawanyo wa kazi katika kitengo cha Uhasibu ambao hautaruhusu mtumishi mmoja kushughulikia malipo kuanzia mwanzo hadi mwisho. Pia mtumishi asikae katika sehemu moja ya kazi kwa muda mrefu bila kubadilishwa na kazi

inayofanywa na mtumishi mmoja ni lazima ipitiwe na mtumishi mwingine ili kuthibitisha uhalali wa malipo yanayotakiwa kulipwa.

- Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kiimarishwe kwa kuongezewa watumishi na vitendea kazi kama vile gari na Kompyuta. Hii itasaidia Mkaguzi wa Ndani kuweza kupanua uwigo wa kufanya kazi ambao unaweza kubainisha mapungufu mapema na kuushauri Uongozi wa Halmashauri kwa ajili ya kuchukua hatua na kudhibiti kasoro zilizojitokeza.

- Halmashauri ihakikishe kuwa taarifa za vitabu vilivyotumika na visivyotumika inaandaliwa kila mwezi ili kubainisha uwepo wa vitabu vyote na kama kuna mapungufu hatua za haraka zichukuliwe na uongozi wa Halmashauri. Pia, vitabu vya kukusanyia mapato ambavyo havijatumika na vilivyotumika vihifadhiwe kwenye chumba imara (Strong Room) na Uongozi wa Halmashauri uteuwe Mhasibu mmoja kwa maandishi ambaye atawajibika na kutunza vitabu vya risiti na kitabu cha kumbukumbu (Counterfoil register).

- Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuhakikisha kuwa hati zote za malipo zinakuwa na viambatanisho vyake na hati hizo zinatunzwa katika hali ya usalama. Pia Halmashauri itayarishe chumba maalum kwa ajili ya kuhifadhi hati za malipo na kuwa na Mhasibu ambaye atawajibika na upotevu wowote utakaojitokeza.

## 14 .0 Maeneo yenye ubadhirifu Sh.6,711,609,356.64

Matokeo ya Ukaguzi huu maalum yamebainisha matukio kumi na nne(14) yenye jumla ya Sh.6,725,694,256.64 ambayo yana kila dalili za ubadhirifu kama ifuatavyo:

| Na. | Aya | Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | 2.5.6 | Makusanyo ya Fedha ambayo hayakufika Benki | 8,147,412 |
| 2. | 2.6.2 | Kughushiwa kwa Salio katika Akaunti za Benki | 235,057,185.64 |
| 3. | 2.6.3 | Hundi zilizoghushiwa na kulipwa zaidi ya vibutu kaika Akaunti za CHF, Maendeleo,EGPAF,TACAIDS na DASIP | 502,155,820 |
| 4. | 2.6.4 | Fedha zilizohamishwa bila idhini ya Mkurugenzi na kutumika kinyume na malengo | 1,676,246,259 |
| 5. | 2.6.5 | Uhamisho wa Fedha ambazo hazikufika kwenye Akaunti husika | 1,957,659,279 |
| 6. | 2.6.6 | Uhamisho wa Fedha kwenda Akaunti zisizofahamika | 452,379,678 |
| 7. | 2.6.7 | Malipo yaliyofanyika kwa walipwaji wasiofahamika | 689,551,042 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8. | 2.7.1.2 | Fedha ambazo hazikuhamishwa kutoka Akaunti ya Maendeleo kwenda Akaunti ya RWSSP | 88,700,000 |
| 9. | 2.7.1.3 | Matumizi yaliyofanywa kinyume na malengo katika Akaunti ya RWSSP | 338,974,569 |
| 10. | 2.7.2.1.1 | Fedha ambazo hazikuhamishwa kutoka Akaunti ya Maendeleo kwenda Akaunti ya Mfuko wa Afya wa Pamoja | 244,358,000 |
| 11. | 2.7.2.2.1 | Fedha ambazo hazikuhamishwa kutoka Akaunti ya Maendeleo kwenda Akaunti ya MMAM. | 338,372,112 |
| 12. | 2.7.2.3.1 | Fedha ambazo hazikuhamishwa kutoka Akaunti ya Maendeleo kwenda Akaunti ya TACAIDS. | 53,202,000 |
| 13. | 2.7.2.6 | Matumizi ya Fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii(CHF) yasiyoidhinishwa | 126,806,000 |
| **Jumla** | | | **6,711,609,356.64** |

## TAARIFA YA UKAGUZI MAALUM ULIOFANYIKA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU KWA KIPINDI CHA 2007/2008-2009/2010.

### SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ni moja kati ya Halmashauri 8 zinazounda Mkoa wa Shinyanga na ilianzishwa rasmi mwaka 2005 chini ya kifungu cha 5 cha Sheria za Serikali za Mitaa Na.7 ya mwaka 1982.

Ukaguzi huu umetokana na maamuzi yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya kubainika kwa mapungufu makubwa katika utunzaji wa nyaraka na kutokamilika kwa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na kusababisha Halmashauri hiyo kupata Hati ya Ukaguzi isiyoridhisha (Adverse Opinion) . Hivyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliamua ukaguzi huu maalumu ufanyike kwa kina ili kubaini kama kuna ubadhirifu wowote na kubaini wahusika. Zaidi ya hayo, ukaguzi huu umefanyika kwa mujibu wa kifungu cha 36 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya 2008 ambacho kinatoa mamlaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalumu pale atakapoona kuwa inafaa katika masuala yanayohusiana na fedha na mali za umma.

Kwa barua yenye Kumb. Na. BE. 27/366/07/11 ya tarehe 27 April, 2011, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliunda Timu ya Wakaguzi kufanya ukaguzi maalumu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu katika Miradi ya maendeleo iliyotelekezwa katika mwaka ya fedha ya 2008/2009 na 2009/2010.

### 1.1 MADHUMUNI YA UKAGUZI

Madhumuni ya kufanya Ukaguzi huu maalumu ni kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa mapendekezo yake kuhusiana na Hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu. Ili kufanikisha lengo hili, ukaguzi huu ulitakiwa kujikita katika mambo yafuatayo:

- Kuhakiki usahihi wa mapato ya miradi yaliyopokelewa na Halmashauri kama yamekatiwa risiti na kuingizwa katika vitabu vya hesabu za Halmashauri.
- Kuhakiki usahihi wa matumizi mbalimbali na utekelezaji wa miradi ya Halmashauri kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia tarehe 01/07/2008 hadi 30/06/2010.
- Kuhakiki uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu za utunzaji wa fedha za Umma.

- Kufanya uhakiki wa miradi iliyotelekezwa kwa kulinganisha na michanganuo ya gharama (BOQs) iliyotayarishwa.
- Aidha, ukaguzi ulikuwa na majukumu ya kuchunguza na kukusanya ushahidi ili:
  (i) Kubaini kama kuna udanganyifu (fraud) katika mapato na matumizi ya Halmashauri na kubainisha wahusika wa udanganyifu huo kama upo.
  (ii) Kubainisha kiwango cha upotevu wa fedha za Halmashauri kama kipo na kubainisha namna udanganyifu ulivyotekelezwa.
  (iii) Kubainisha kama menejimenti ya Halmashauri ina ufahamu juu ya udanganyifu huo na hatua zilizochukuliwa.

## 1.4 HADIDU ZA REJEA ZILIZOTUMIKA WAKATI WA UKAGUZI

Ukaguzi ulifanyika katika maeneo mbali mbali na hadidu za rejea zifuatazo zilitumika katika ukaguzi huu maalum katika kubaini ubadhirifu wa fedha za Umma katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu:

- Kukusanya ushahidi katika kuthibitisha namna Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu inavyosimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukaguzi maalum pia uliwajibika katika kukagua kwa kina miradi ya maendeleo.

- Kufanya uhakiki wa kina kuhusiana na hati za malipo zilizokosekana wakati wa ukaguzi uliopita wa mwaka wa fedha 2009/2010 na kufanya mahojiano na viongozi na wahasibu ambao wanahusika na utunzaji wa nyaraka za malipo ili kubaini ukweli wa kuhusiana na upotevu wa hati hizo za malipo.

- Kufanya uhakiki wa kina kuhusiana na malipo yaliyolipwa katika Akaunti mbalimbali za benki kwa walipwaji ambao hawafahamiki ili kujua uhalali wa malipo hayo pamoja na kufanya mahojiano na watumishi ambao walihusika na kuandaa taarifa za Usuluhisho wa Benki kwa kila mwezi ili kubaini ukweli wa malipo hayo.

- Kupitia hati zote za malipo ili kujua uhalali wa malipo yaliyofanywa na Halmashauri bila kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri. Pia kufanya mahojiano na viongozi mbali mbali wa Halmashauri ili kupata maoni yao.

- Kuhakiki Stakabadhi zilizopokelea fedha katika Halmashauri ili kubaini kuwa kiasi chote cha fedha kilichotokana na makusanyo ya fedha kimeingizwa katika daftari la fedha na kupelekwa Benki.

- Kupitia hati zote za malipo ili kubaini kama kweli malipo yalilipwa bila kuwa na viambatanisho. Pia kufanya mahojiano na watumishi

wanaohusika na utayarishaji wa hati za malipo na wanaohusika na kupitisha malipo.

- Kupitia taarifa zote za mishahara ili kubaini kiasi kilichokatwa kutoka katika mishahara ya watumishi mwaka wa fedha 2009/2010 na kufanya uhakiki wa kina ili kujua ni kiasi gani kimelipwa katika Taasisi husika na kiasi gani hakijalipwa .

- Kupitia hati za malipo katika akaunti mbalimbali za Halmashauri kubaini kama kuna hati za malipo zilizohusika na kuhamisha fedha kutoka akaunti moja kwenda akaunti nyingine. Pamoja na kupitia stakabadhi zote za mapato ya Halmashauri ili kubaini kama kuna marejesho ya fedha kutoka akaunti moja kwenda akaunti nyingine.

- Kufanya uhakiki wa kina na kubaini tofauti ya malipo yaliyofanyika kwenye daftari la fedha na malipo yaliyofanyika Benki (NMB Manoga) kama imesababishwa na nini.

## 1.5 KIPINDI CHA UKAGUZI

Ukaguzi huu ulitakiwa kufanyika katika maeneo husika kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010. Timu ya ukaguzi iliamua kurudi nyuma mwaka mmoja hadi mwaka 2007/2008 ili kuweza kupata ushahidi wa kutosha kwa yale mapungufu yaliyobainika katika ukaguzi huu maalum.

**SURA YA PILI**

## 2.0 MAMBO YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI MAALUM

Ukaguzi maalum ulipitia nyaraka mbalimbali za Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu pamoja na kuwahoji baadhi ya watumishi, wakuu wa idara, watendaji wa kata na vijiji, waheshimiwa madiwani na wajumbe wa Bodi ya Zabuni. Mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi maalum ni haya yafuatayo:

## 2 .1 MIFUMO DHAIFU YA UDHIBITI WA NDANI

Katika kupitia mtiririko wa Uongozi wa Halmashauri tangu ilipoanzishwa mwaka 2005, timu ya Ukaguzi ilibaini kuwa ni moja ya sababu kubwa ya matatizo yaliyotokea hivyo kuathiri uwekaji wa Mfumo wa Udhibiti wa Ndani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, uwepo kwa mabadiliko ya uongozi ya mara kwa mara yaliyokuwa yakitokeza ndani ya vipindi vifupi vifupi, pia wengi wa Wakuu wa Idara na Wakuu wa Vitengo Kukaimu kwa muda mrefu hivyo kutowajibika ipasavyo kama inavyoonekana katika mtiririko ufuatao:

### 2.1.1 Mabadiliko ya Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri kila baada ya muda mfupi

Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu imekuwa na mabadiliko ya Wakurugenzi Watendaji mara kwa mara na hadi ukaguzi maalumu unafanyika, imeshakuwa na Wakurugenzi Watendaji wanne tangu ianzishwe mwaka 2005 .

Mkurugenzi Mtendaji wa kwanza wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, alikuwa Ndugu Christine Midello, ambaye alihamia kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, mkoani Kigoma tarehe 16/6/ 2004. Baada ya miaka miwili (2) alihamishiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa.( **Angalia Kielelezo A1(i) na A1 (ii)**

Mkurugenzi Mtendaji wa pili wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu alikuwa Ndugu Limbakisye E. S. Shimwela, aliyekuwepo kwa mwaka mmoja tu tangu Julai, 2006 hadi Julai, 2007.

**Comment [m1]:** Vielelezo havipo kwenye Faili kwa ajili ya Ng.Limbakisye E.S.Shimwela na Elly Jesse Mlaki.

Mkurugenzi Mtendaji wa tatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu alikuwa Ndugu Elly Jesse Mlaki, aliyekuwepo kwa mwaka mmoja na miezi saba (7) tu tangu Agosti, 2007 mpaka Machi, 2009.

Mkurugenzi Mtendaji aliyepo kwa sasa ni Theonas Aron Nyamhanga amekuwepo katika Halmashauri hiyo kuanzia tarehe 20.4.2009. (**Angalia Kielelezo A2 (i) na A2 (ii).**

### 2.1.2 Mabadiliko ya mara kwa mara katika Idara ya Fedha (Mweka Hazina)

Idara ya Fedha nayo imekuwa na mabadiliko ya mara kwa mara kama ilivyokuwa kwa Wakurugenzi Watendaji . Halmashauri ilishakuwa na waweka Hazina sita (6) katika vipindi mbalimbali tangu ianzishwe mwaka 2005.

Mweka Hazina wa kwanza wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu alikuwa ndugu Emmanuel S. Masele ambaye alikuwa Mkaguzi wa ndani wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Alichukuliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu tarehe 20.04 2005 kama Mtaalam wa kusimamia uanzishaji wa Idara ya Fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu iliyokuwa ikitarajia kuanza rasmi. **Angalia Kielelezo A3(i) .**

Mnamo tarehe 03.05.2005 aliandikiwa barua na Mkurugnzi Mtendaji wa Halmashauri ya Shinyanga kuwa alitakiwa kuhamia Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kusimamia uanzishwaji wa Idara ya Fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu na kuwa Mkaguzi wa Ndani. **Angalia Kielelezo A3 (ii) .**

**Comment [m2]:** Ulisema alihamia mwezi April na sasa unasema Mwezi Mei. Je ipi ni sahihi/ TAREHE HIZI NI KWA MUJIBU WA BARUA ZILZOTAJWA.

Idara ya fedha ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu iliongozwa na kaimu Mweka Hazina Bw. Hashim Lukwenda Luholela kwa mwezi mmoja tu kuanzia Juni, 2005 hadi Julai, 2005 na aliteuliwa kwa Barua zenye Kumb. Na. HB: 3/69/01B/82 ya tarehe 23/06/2005 na Kumb. Na. SDC. PF. 3984/38 ya tarehe 05/07/2005. **Angalia Kielelezo A4 na A5.**

Kuanzia Julai, 2005, Idara ya Uhasibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ilikuwa ikiongozwa na Mweka Hazina Ndugu Emmanuel S. Masele ambaye ndiye aliyekuwa kama Mtaalam wa kusimamia uanzishwaji wa Idara ya Fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ambaye aliteuliwa kwa barua yenye Kumb. Na. 3/69/01B ya tarehe 19/07/2005 na barua yenye Kumb.Na.HB:3/69/01B/81. **Angalia Kielelezo A6 na A7.**

Kuanzia Septemba 2008 hadi April, 2010 Mweka Hazina wa Halmashauri alikuwa Ndugu Muhidini Mohamedi aliyeripoti kazini tarehe 15.9.2008 ambaye alihamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kwa barua yenye Kumb Na. CHB: 348/355/07 ya tarehe 23/06/2008. **(Angalia Kielelezo A8 (i) na Kielelezo A8(ii).)**

**Comment [m3]:** Mbona hujazungumzia suala la kusimamishwa kazi kwa Mweka Hazina huyo?

Mweka Hazina Ndugu Muhidin Mohamed amesimamishwa kazi tangu April, 2010 kwa tuhuma za kushindwa kusimamia na kumshauri Afisa Masuuli juu ya masuala ya fedha za miradi ya DASIP na kutowajibika ipasavyo na kusababisha uhamisho wa Sh.300,000,000 za mradi kwa matumizi yasiyojulikaka na baadaye kufunguliwa Hati ya Mashtaka tarehe 10.3.2010. (**Angalia Kielelezo A8(iii).)**

Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu aliyekuwa akikaimu wakati wa ukaguzi huu maalum ni Ndugu Oscar Msalikwa, tangu mwezi Aprili, 2010.

### 2.1. 3 Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kutokuwa na Mkuu wa Kitengo

Halmashauri tangia ianzishwe mwaka 2005 ilishakuwa na makaimu Wakaguzi wa Ndani watatu. Idara hii haijawahi kuwa na Mkaguzi wa Ndani (Chief Internal Auditor) aliyeteuliwa na TAMISEMI kwa ajili ya ukaguzi wa ndani.

Ndugu Emmanuel S. Masele, aliteuliwa kuwa Kaimu mkaguzi wa ndani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kwa muda wa mwezi mmoja tu, tangu Juni, 2005 hadi Julai, 2005 kama inavyoonekana katika barua zenye Kumb. Na. HB. 3/69/01B/81 ya tarehe 20/06/2005, Kumb. Na. HB: 3/69/01B/82 ya tarehe 23/06/2005, Kumb. Na. SDC. PF. 3984/38 ya tarehe 05/07/2005 na Kumb. Na. 3/69/01B ya tarehe 19/07/2005. **Angalia vielelezo A4, A5, A6 na A7.**

Kuanzia Julai, 2005 hadi Oktoba, 2007 Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu haikuwa na Mkaguzi wa Ndani. Hatimaye tarehe 16.10. 2007 ndugu Exaud Massawe (Mhasibu Daraja I) aliteuliwa kuwa kaimu Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/PF/1354/13 ya tarehe 16/10/2007. **Angalia Kielelezo A9.**

Mwezi Januari, 2010 Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ilipata Mkaguzi wa Ndani, Bi. Vumilia Saimanga, aliyehamishwa toka Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi kwa barua ya Uhamisho yenye Kumb. Na. CBA.176/297/01/07 ya tarehe 13/11/2009 na barua ya kuripoti kazini yenye Kumb. Na. KDC/PF.1791/12 ya tarehe 13/01/2010 kimsingi yeye ni mwajiriwa kama Mkaguzi wa Ndani lakini yuko chini ya kaimu Mkaguzi wa Ndani ndugu Exaud Massawe ambaye ameajiriwa kama Mhasibu ambaye bado anakaimu nafasi ya Mkaguzi wa ndani. **Angalia Kielelezo A10.**

**Comment [m4]:** Mbona haieleweke kama ND. EXAUD MASSAWE ALIHAMA AU NDIYE HEAD WA IT UNIT HADI SASA.

### 2.1.4 Mabadiliko katika Idara ya Mipango

Afisa Mipango wa kwanza Ndugu Festo. D. Mbezi alihamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu toka Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga tarehe 3.5.2005 kwa barua Kumb. S.2/50/12 na alitumikia nafasi hiyo katika Halmashauri ya Kishapu hadi 20.8 2008. Afisa Mipango mwingine Bw. K.S.C Makonda alihamishiwa katika Halmashauri ya Kishapu kwa barua ya uhamisho yenye Kumb. Na.CBA 176/297/01/107 ya tarehe 20.8.2008 akitokea katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe mpaka alipohamishwa mwaka 2009 na nafasi yake kuchukuliwa na ndugu Richius Bilakwata Domisian aliyehamia kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kwa barua yenye Kumb. Na.CHA.215/355/01 ya tarehe 04/11/2009. **Angalia Kielelezo A11, A12 na A13.**

### 2.1.5 Idara ya Utumishi kukaimiwa

Afisa Utumishi wa kwanza wa Halmashauri Ndugu Emmanuel J. Jalla aliajiriwa tarehe 10.5.2006 kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/PF.5/5 ambaye baadaye alisimamishwa kazi na safasi yake kukaimiwa na Ndugu Bless D. Mwakyusa . Mnamo tarehe 18.10.2010 Ndugu Bless D. Mwakyusa aliondolewa kukaimu kwa kukosa sifa zinazotakiwa (Rejea barua zenye Kumb. Na. KDC/CS/10/I/78 ya terehe 17/07/2008 na Kumb. Na. KDC/CPF/64/05 ya tarehe 13/10/2010. **Angalia Kielelezo A14 na A15 (1)**.

Baada ya hapo Idara ya utumishi ilikuwa inaongozwa Ndugu Nico A. Kayange ambaye pia alikuwa anakaimu na aliondolewa katika nafasi hiyo kwa barua yenye Kumb.Na. KDC/PF.1515/31 ya tarehe 14/02/2011 na Kumb. Na. KDC/PF.1515/31 ya tarehe 07/03/2011). **Angalia Kielelezo A16(1) na 16 (2)**.

Kuanzia Febrari, 2011 Idara ya utumishi inaongozwa na Ndugu Hamisi Juma Mpume, aidha tangu kuanzishwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mwaka 2005, nafasi ya Afisa Utumishi wa Wilaya imekuwa inakaimiwa kwa muda wote.

### 2.1.6 Uongozi katika Idara ya Kilimo.

Afisa Kilimo wa kwanza wa Halmashauri Ndugu Ali Juma Lugendo alihamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu toka Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Mwezi Mei, 2005 na aliitumikia Halmashauri hiyo hadi Agosti, 2008 alipohamia Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kwa barua yenye

Kumb. Na. S.2/50/12 ya tarehe 03/05/2005, Kumb. Na. KDC/PF.3703/55 ya tarehe 17/06/2006, Kumb. Na. KDC/PF/3703/56 ya tarehe 19/06/2006 na Kumb. Na. CBA 176/297/01/103 ya tarehe 14/8/2008. **Angalia vielelezo A17(i) - A17(iv).**

Kuanzia Agosti, 2008, Idara ya Kilimo ilikuwa inaongozwa na Ndugu Herman Kadigi, aliyehamia kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kwa barua yenye Kumb. Na. CBA 176/297/01/102 ya tarehe 14/08/2008, mpaka aliposimamishwa kazi mwezi Mei, 2010 kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/CS.10/2/97 ya tarehe 05/05/2010. **Angalia Kielelezo A18.**

### 2.1.7 Uongozi katika Idara ya Afya.

Mkuu wa Idara ya Afya, Dr. Alex Kapula aliteuliwa June, 2009 kwa barua yenye Kumb. Na DED/HDC/CPF. 12/3 ya tarehe 29/6/2009 na kukubali uteuzi huo kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/A/101/18 ya tarehe 06/07/2009. Kabla uteuzi alikuwa akikaimu shughuli za Mganga Mkuu wa Wilaya kwa miaka minne kuanzia tarehe 6.5.2005 kwa barua yenye Kumb. Na. SDC. PF.2503/80. **Angalia Kielelezo A19(i) – A19(iii).**

### 2.1. 8 Uongozi katika Idara ya Ujenzi

Mhandisi wa ujenzi wa Kwanza wa Halmashauri alipatikana kwa ajira ya moja kwa moja mwezi Agosti, 2006 kwa barua ya ajira ni ya tarehe 18/04/2006 yenye Kumb. Na. KDC/PF 65 baada ya kuhitimu shahada ya kwanza ya Uhandisi katika Chuo kikuu cha Dar es Salaam. Alithibitishwa kazini kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/PF.65/10 ya tarehe 25/06/2007. Aliteuliwa kuwa Mkuu wa Idara kwa barua yenye Kumb. Na. DED/KDC/CPF.25/8 ya tarehe 01/08/2007 na kuthibitishwa kama mkuu wa Idara ya ujenzi kuanzia tarehe 11/11/2006, kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/CPF.25/10 ya tarehe 15/05/2009. **Angalia Kielelezo A20(i) - A20(v).**

### 2.1.9 Uongozi katika Idara ya Maji

Mhandisi wa Maji wa Kwanza wa Halmashauri apatikana kwa ajira ya moja kwa moja toka chuoni tarehe 14.8.2006 kwa barua ya ajira yenye kumb. Na. PF.85/5 baada ya kuhitimu shahada ya kwanza ya Uhandisi katika Chuo kikuu cha Dar es Salaam. Mwaka mmoja baada ya kuajiliwa akiwa Mhandisi Daraja la pili, aliteuliwa kuwa Mkuu wa Idara ya Maji kwa barua yenye Kumb. Na. DED/KDC/CPF.8/02 ya tarehe 01/08/2007 kabla hajathibitishwa kazini. Alithibitishwa kama Mkuu wa Idara kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/CPF.8/04 ya tarehe 15/05/2009. **Angalia Kielelezo A21(i) -.A21(iii)**

### 2.1.10 Uongozi katika Idara ya Elimu

Afisa Elimu (Msingi) wa kwanza wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Ndugu Patrick P. Musira alihamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu toka Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Mwezi Mei, 2005 kwa barua yenye Kumb. Na. S.2/50/12 ya tarehe 03/05/2005 na kuendelea hadi Januari, 2006 **Angalia Kielelezo A22.**

Kuanzia Januari, 2006 Idara ya Elimu (Msingi) ilikuwa inaongozwa na Mwl. Reuben C. Kaduri aliyeripoti Kishapu Januari, 2006 kwa uhamisho toka Kanda ya kusini kwa barua ya uhamisho yenye Kumb. Na. CHA/24/100/01/H ya tarehe 18/01/2006 na aliteuliwa kuwa Mkuu wa Idara ya Elimu kwa barua ya uteuzi yenye Kumb. Na. ED.3801/5 ya tarehe 17/06/2006 na kuidhinishwa kwa barua yenye Kumb. Na. DED/KDC/CPF 3/10 ya tarehe 20/11/2007. **Angalia Kielelezo A23.**

Afisa Elimu huyo alifanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu hadi Novemba, 2010 na kuanzia muda huo Idara ya Elimu (Msingi) inaongozwa na Mwl. Underson Mwalongo aliyeteuliwa kwa barua yenye Kumb Na. CHA: 24/100/01.N/177 ya tarehe 04/11/2010. **Angalia Kielelezo A24.**

Afisa Elimu (Sekondari) wa Halmashauri ya Kishapu Mwl. Nicholaus Besisila aliteuliwa mwezi Mei, 2009 kwa barua yenye Kumb Na. CHA: 24/100/02/47 ya tarehe 01/05/2009 na alikubali uteuzi huo kwa barua ya kukubali uteuzi yenye Kumb. Na ED. 1561/7 ya tarehe 04/09/2009 na kuripoti mwezi Septemba, 2009. **Angalia Kielelezo A25.**

### 2.1.11 Uongozi katika Kitengo cha Ugavi

Tangu Halmashauri imeanzishwa kitengo cha Ugavi kimekuwa chini ya maafisa ugavi watano katika vipindi mbalimbali vifupi. Afisa ugavi wa kwanza wa Halmashauri, Ndugu Auston Mutahyabarwa aliyeazimwa toka Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga tangu tarehe 2.3. 2006 kwa barua ya yenye kumb. Na. SDC/PF.547/133 na alifanya kazi kwa muda wa miezi mitatu (3) alitakiwa kukabithi Ofisi kwa Bw. Elias Simiyu kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/P.40/3 ya tarehe 09/06/2006 . **Angalia Kielelezo B1(i) na B(ii)**

Bw. Elias Simiyu alikuwa katika nafasi hiyo hadi tarehe 27.6. 2008 na nafasi yake ilichukuliwa na Ndugu Faraji M. Murebere aliyehamishiwa toka Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kwa barua ya uhamisho yenye Kumb. Na. CHB. 222/355/02 ya tarehe 09/06/2008 na aliripoti kazini kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/PF. 14/9/2 ya tarehe 28/6/2008 na alifanya kazi mpaka April, 2010 alipostaafu. **Angalia Kielelezo B2(i) - B2 (ii)**

Kuanzia April, 2010, ofisi ya ugavi ilikuwa inaongozwa tena na Ndugu Elias Simiyu hadi May, 2011 baada ya uteuzi wake kutenguliwa kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/PF.66 ya tarehe 27/05/2011. **Angalia Kielelezo B3.**

Kuanzia May, 2011 hadi wakati wa ukaguzi huu, kitengo cha ugavi kinaongozwa na Ndugu Medson Matarana aliyeteuliwa kwa barua ya uteuzi yenye Kumb. Na. KDC/PF.1513/5 ya tarehe 27/05/2011. **Angalia Kielelezo B4.**

**Mapendekezo ya ukaguzi**

Kuwepo kwa mabadiliko ya wakuu wa idara mara kwa mara na kukaimu kwa muda mrefu imekuwa ni kiini cha kupunguza uwajibikaji na umeathiri mtiririko katika ufanisi kiutendaji.

Mamlaka ya ajira na uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuhakikisha kunakuwepo na utaratibu mzuri wa kuhamisha wakuu wa Idara usiwe wa mara kwa mara, pia nafasi zinapoachwa wazi zisikae muda mrefu bila kujazwa kwa kuwathibitisha wanaozikaimu au kujazwa mapema na wenye sifa.

### 2.1.12 Udhaifu katika utendaji wa kazi katika Idara ya Uhasibu

#### 2.1.12.1 Kutokuwepo kwa Mgawanyo wa kazi.

Mgawanyo wa kazi katika Idara ya Uhasibu ulioanza kutumika tarehe 29/12/2008 ukionesha idadi ya Wahasibu 13 na Maafisa Ugavi 2 ambapo kabla ya hapo Halmashauri haikuwa na mgawanyo wowote wa kazi kinyume na Agizo Na.10 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997. Hivyo tangu mwaka wa fedha 2005/2006 hadi 2006/2007, na mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2007/2008 hakukuwepo na mgawanyo wa kazi kimaandishi ulio rasmi katika Idara ya Uhasibu kama inavyoonekana katika Kielelezo cha barua ya mgawanyo wa kazi yenye Kumb. Na. KDC/F.10/1/25 ya tarehe 29/12/2008 **Angalia Kielelezo C.1**

Hii pia inaonesha kwamba mchanganuo na mipaka ya utendaji wa kazi na mzunguko wa majukumu ya kazi (Job description, specification and rotation) havikuwepo. Watendaji katika kitengo cha uhasibu walifanya kazi zao bila kubadilisha kwa kipindi chote tangu Halmashauri ianzishwe.

#### 2.1.12.2 Udhaifu ndani ya Idara ya uhasibu

Mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani, uliruhusu baadhi ya watendaji hasa katika Idara ya uhasibu, kufanya kazi ambazo zingekuwa nje ya majukumu ya kazi zao au kuwa na mjukumu zaidi ya ambayo yangekuwa ndani ya majukumu yao. Hii ni pamoja na:

- Kuidhinisha malipo bila kuwa na uhakika wa fedha kuwepo.
- Kutumia makusanyo ya fedha kabla ya kupelekwa Benki.
- Kuandika vocha na kulipa fedha taslimu bila idhini.

Mapungufu katika usimamizi wa fedha pia yaliainishwa na Mkurugenzi Mtendaji Ndugu C.K.Midello kwa kumwandikia barua Mweka Hazina wake Ndugu E. Masele, yenye Kumb. Na. KDC/PF.18/10 ya tarehe 01/06/2006. **Angalia Kielelezo C.2**

#### 2.1.12.3 Utunzaji wa nyaraka ulio na mapungufu

Ukaguzi huu maalumu ulipitia mgawanyo wa kazi na ulitembelea maeneo ambayo yanatumika kuhifadhia hati za malipo na kubaini kuwa:

- Kulingana na mgawanyo wa kazi, hakuna mtu maalum wa kutunza nyaraka za malipo. Hati za malipo huifadhiwa katika makabati ambayo hayana milango.

- Halmashauri haina sehemu maalumu ya kuhifadhia hati za malipo. Kuna sehemu tofauti ambazo hutumika kuhifadhi hati za malipo ambazo zikiwemo ofisi ya mapato na ofisi ya malipo (cash office). Nyaraka hizo uhifadhiwa katika makabati yaliyoko katika ofisi hizo.

- Kuna uwezekakano wa kuchukuliwa kwa hati za malipo bila idhini, kwa vile hazina udhibiti wa aina yeyote mbali na kwamba ofisi zinapotunzwa hati hizo zina ufunguo. Pia Hakuna "movement register "ya hati za malipo ili kuhakiki mwenendo wa hati hizo zinapochukuliwa.

- Hakuna Kasiki ya kutunza nyaraka muhimu kama hundi na nyaraka nyingine muhimu kama vitabu vya risiti za mapato.

Ukaguzi maalum pia umebaini kuwa Mweka Hazina wa Halmashauri Ndugu A.R. Bashaula katika barua yake kwa watumishi wa Idara ya fedha yenye Kumb. Na. KDC/F 10/1/2 ya tarehe 26/10/2007, aliwahi kukiri uwepo wa tatizo la hujuma dhidi ya Hati za malipo na viambatanisho vyake ndani ya Idara ya Fedha, unaopelekea upotevu mkubwa wa nyaraka hizo. **Angalia Kielelezo C.3.**

Kutokana na kuwepo upotevu mkubwa wa nyaraka, Mweka Hazina wa Halmashauri Ndugu A.R. Bashaula katika barua yake kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, alipendekeza kuwepo na chumba maalum cha kuhifadhia nyaraka na kumbukumbu za fedha na awepo mtumishi mmoja atakayewajibika kuhakikisha nyaraka hizo zinatunzwa na kudhibitiwa kwa usalama mkubwa na zinapatikana zinapohitajika. (Rejea barua yenye Kumb. Na. KDC/25/02/2008 isiyokuwa na tarehe). **Angalia Kielelezo C.4**

**Mapendekezo ya Ukaguzi**

Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuteua Mhasibu mmoja ambaye atahakikisha hati zote za malipo zinakuwa na viambatanisho vyake na Hati hizo zinatunzwa katika hali ya usalama na kuhakikisha kunakuwa na chumba maalum kwa ajili ya kuhifadhi Hati za malipo na Mhasibu huyo atawajibika kwa upotevu wowote utakaojitokeza.

### 2.1.12.4. Nyaraka ambazo hazikupatikana wakati wa ukaguzi

Nyaraka mbalimbali hazikuweza kupatikana wakati wa ukaguzi huu maalumu, hivyo kusababisha wakaguzi kushindwa kupata taarifa muhimu zilizomo ndani ya nyaraka hizo na kwa hali hiyo kuathiri matokeo ya ukaguzi huu maalumu. Nyaraka hizo ni kama Sampuli za watia saini katika akaunti 20 za Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu zilizopo NMB Tawi la Manonga katika mwaka wa fedha 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010.

- Orodha ya hundi mpya zilizochukuliwa kutoka Benki – NMB Manonga katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010.

- Vibutu vya hundi zilizolipwa kwa akaunti zote kwa mwaka wa fedha 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010.

- Orodha ya hundi zilizokuwa zinapelekwa Benki – NMB Manonga, kwa ajili ya malipo (Bank Check list) katika mwaka wa fedha 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010.
- Hundi 158 zilizotumika (paid cheques) katika malipo yaliyopita kwa mwaka wa fedha 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010. Hundi hizi ni kati ya zile ambazo hazikuchukuliwa na PCCB na Polisi kutoka Benki – NMB Tawi la Manonga.

- Mikataba ya miradi ujenzi iliyotembelewa na timu ya ukaguzi, Madaftari ya fedha (Cash book) yaliyandikwa kwa mkono kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na 2008/2009, Usuluisho wa Benki wa kila mwezi kwa mwaka wa fedha 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010. Baadhi ya Hati za malipo za mwaka wa fedha 2009/2010 na Mafaili ya baadhi ya watumishi.

- Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu imekiri kulishughulikia tatizo hili bila mafanikio, hii inatokana na kutokuwepo uwajibikaji katika maswala ya udhibiti na utunzaji wa nyaraka za malipo hivyo kuzuia timu ya Ukaguzi kujiridhisha katika maeneo mbalimbali yanayohusika na nyaraka hizo. **Angalia Vielelezo C.5, C6 na C7**

**Mapendekezo**

- Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuchukua hatua stahiki kwa Mweka Hazina Ndugu Muhidini Mohamed kwa kushindwa kusimamia nyaraka za fedha.
- Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuhakikisha Mweka Hazina wa Halmashauri anahusika na usimamizi wa Hati za malipo kama ilivyo katika agizo Na.96 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa,1997.
- Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuteua Mhasibu mmoja ambaye atahakikisha hati zote za malipo zinakuwa na viambatanisho vyake na Hati hizo zinatunzwa katika hali ya usalama na kuhakikisha kunakuwa na chumba maalum kwa ajili ya kuhifadhi Hati za malipo na Mhasibu huyo atawajibika kwa upotevu wowote utakaojitokeza.
- Kuwe na kitabu kinachoonesha mahali zilipo hati za malipo na aliyenazo,
- ili kurahisisha utafutaji pindi zinapohitajika.

### 2.1.12.5 Udhaifu katika ofisi ya Malipo (Cash Office)

Ofisi ya malipo ilikuwa inaongozwa na Mtunza fedha Ndugu Walumu Musa Limbe aliyeajiriwa kama Afisa Mtendaji Kata I katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Januari, 1999. Na kuhamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mwezi Mei, 2005 kama Mhasibu Msaidizi, mpaka aliposimamishwa kazi mwezi Aprili, 2010 kwa barua yenye Kumb. Na. PF.3692/4 ya tarehe 25/02/1999 baadaye alihamishiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kwa barua ya uhamisho yenye Kumb. Na. S 2/50/12 ya tarehe 03/05/2005. **Angalia Kielelezo C8, C9**

Mtunza fedha alisimamishwa kazi tarehe 6/4/2010 kwa barua yenye kumbukumbu Na.KDC/CS.20/2/69 kupisha uchunguzi wa tuhuma za kugushi saini, hati za malipo kwa kuongeza viwango vya tarakimu za fedha kwenye hundi hivyo kusababisha uhamisho wa kiasi cha Sh.300,000,000 kwa matumizi yasiyokusudiwa kama inavyosomeka katika hati ya mashitaka ya tarehe 10/3/2010**.** Kutokana na kurundikiwa kazi mtunza fedha kulisababisha kuwepo kwa mwanya ubadhirifu wa fedha kupitia benki bila kugundulika mapema. **Angalia Kielelezo C1, C10 na C11**

Mtunza fedha (Cashier) Ndugu Walumu Musa Limbe alitambulishwa kwa meneja wa Benki na kuidhinishwa kwa barua isiyo na kumbukumbu Namba ya tarehe 20/07/2005 iliyoandikwa na Mkurugenzi Mtendaji kwenda kwa Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Manonga, iliyompa mamlaka ya kushughulikia masuala yote yanayohusu fedha katika akaunti za benki. Kwa idhini hiyo, aliweza kufanya kazi za kuweka na kutoa fedha katika Benki kwa wakati wowote bila kizuizi. Angalia **kielelezo C.12**

Kwa mujibu wa mgawanyo wa kazi mtunza fedha alikuwa na majukumu ya Kufunga vitabu vyote vya fedha kila siku (Cash books), kuandaa na kutoa taarifa ya bakaa ya fedha ya kila siku, kuchukua credit advice za fedha zilizoingia benki kila siku, kuchukua Bank Statements na Bank Certificates na kuzitunza, Kutunza paylist zote baada ya kufanya malipo, kutunza vitabu vya hundi za akaunti zote, Kutunza daftari za fedha (cash book) zote za Halmashauri na Kupeleka "cheque list" benki. **Angalia Kielelezo C1 na C13.**

Pia, Barua yenye Kumb. Na. KDC/PF.15/3696/39 ya tarehe 06/11/2006 aliyoandikiwa na Mweka Hazina wa Halmashauri, inaonesha kuwa alishindwa kutoa taarifa ya fedha alizokuwa akipokea na jinsi alivyokuwa akizipeleka Benki. **Angalia Kielelezo C.14**

Vile vile barua yenye Kumb. Na. KDC/PF.30/45 ya tarehe 20/08/2008 aliyoandikiwa na Mweka Hazina wa Halmashauri, ikimtaka kutoa maelezo kuhusu hundi iliyoandikwa kinyume na taratibu kwa nia ya kuchukua fedha Benki bila idhini. **Angalia Kielelezo C.15**

Katika kupitia jarada la Mtunza fedha Ndugu Walumu Musa Limbe, ilibainika kwamba hajawahi kuomba likizo ya muda mrefu tangu amehamia Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mwezi Mei, 2005 mpaka aliposimamishwa kazi mwezi April, 2010. Pia ilibainika kuwa alikuwa cheti cha elimu ya Kidato cha IV tu, chenye jina la Walumu Mashine chenye No S.0367-121, kinachoonesha kuwa alihitimu kidato cha nne Kilosa Sekondari, Novemba, 1990. Hakuwa na taaluma ya uhasibu ambayo ingemuwezesha kujua taratibu wa kutunza taarifa za fedha, kwa hiyo kazi aliyopewa ilikuwa na majukumu makubwa ikilinganishwa na elimu aliyokuwanayo. **Angalia Kielelezo C16**

**Mapendekezo ya ukaguzi**

Halmashauri unatakiwa kuandaa mgawanyo wa kazi wenye ulingano unaokidhi uimarishaji wa udhibiti wa mfumo wa ndani na kusiwepo mrundikano wa kazi kwa mhasibu mmoja.

### 2.1.13 Mapungufu katika Mfumo wa Teknolojia ya Mawasiliano (Quick Use Accounting Package)

Mnamo mwaka wa Fedha 2009/2010 Halmashauri ilianza kutumia Mfumo wa Teknolojia ya Mawasiliano (Quick Use Accounting Package) kwa maelekezo ya barua yenye kumb Na. BA.176/270/01/70 ya tarehe 24/8/2009 toka kwa Katibu Tawala Mkoa, Mkoa wa Shinyanga. **Angalia Kielelezo D1**

Imebainika kuwa Mfumo wa Teknolojia ya Mawasiliano (Quick Use Accounting package) hauna udhibiti kwani mtumiaji mmoja amewezeshwa kufanya taratibu zote za malipo kuanzia kuanzisha malipo uandikaji wa hati za malipo, kuingiza taarifa (Data), kufanya usuluhisho wa benki na kufanya marekebisho (Adjustments). Hali hii inaonesha mapungufu katika mfumo mzima wa malipo na udhibiti wa ndani.

Pia imebainika kuwa mfumo huu haukidhi udhibiti wa matumizi ya fedha kwa maana ya Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) kwani matumizi yanapoidhinishwa hayaendani na fedha zilizopo (salio) katika kifungu husika cha matumizi hivyo kufanya akaunti husika kutumia fedha zaidi ya iliyopo. Hali hii inaonesha udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani ambao unaweza kupelekea matumizi mabaya ya mfumo huo bila udhibiti wowote katika matumizi ya fedha za umma.

**Mapendekezo ya ukaguzi**

Halmashauri inatakiwa kuhakikisha kuwa inawasiliana na TAMISEMI ili kupatiwa Mfumo Funganishi wa Udhibiti wa Fedha (IFMS - Epicor). **Angalia kielelezo D.2**

### 2.1.14 Mapungufu katika Utendaji kazi wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Tangu kuanzishwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mwaka 2005 haijawahi kuwa na Mkuu wa kitengo cha Ukaguzi wa ndani muda wote huo amekuwepo Mhasibu Ng. Exaud Massawe anayekaimu na muda mwingi amekuwa mmoja peke yake, hivyo kuifanya Halmashauri kukosa huduma ya udhibiti wa mfumo wa ndani kuwa dhaifu. Yafuatayo ni mapungufu yaliyobaoinika:

Ilipofika Januari, 2010, Halmashuri ilipata Mkaguzi wa Ndani mmoja aliyehamia kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi na kufanya wakaguzi wa ndani kuwa wawili, ingawa
mahitaji ya Halmashauri ni wakaguzi wa ndani watatu kulingana na barua yenye Kumb. Na.KDC F./1/138 ya tarehe 12/08/2009 iliyoandikwa na Mkurugenzi Mtendaji kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Uchumi. **Angalia Kielelezo E1.** Hata hivyo, kwa mujibu wa Ikama Halmashauri inatakiwa kuwa na wakaguzi wa ndani wanne.

Timu ya ukaguzi imebaini kuwa Mawanda ya utendaji wa mkaguzi wa ndani hayakuwa yameainishwa katika barua yake ya uteuzi na mpango wa kazi wa mkaguzi wa ndani haukuweza kuwasilishwa. Hii ilisababisha mkaguzi wa ndani afanye kazi hata zile zisizomhusu au zenye kustahili kufanywa na mhasibu/ mkaguzi wa awali (Pre-Audit) kama vile kupitia na kusaini hati za malipo kabla ya malipo kupitishwa, kinyume na Agizo Na. 13 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa (LAFM) ya 1997. **Angalia Kielelezo E2 -E5**

**Mapendekezo ya ukaguzi**
Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu inatakiwa kuzingatia maelekezo katika Agizo Na 12 – 16 la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 katika utendaji wa kazi wa wakaguzi wa ndani ili kuweza kuishauri na kuisaidia Halmashauri katika kuthibiti matumizi mabaya ya fedha za Umma.

### 2.1.15 Mapungufu Katika Uundaji wa Bodi ya Zabuni katika Halmashauri ya Kishapu

Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ina Bodi ya Zabuni, ambayo iliundwa mwaka, 2007. Wajumbe wa Bodi ya kwanza ya Zabuni ya Halmashauri waliteuliwa Septemba, 2007. Katika kufuatilia utendaji wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri, timu ya ukaguzi maalum ilibaini mapungufu yafuatayo**:**
Hakukuwa na muhtasari wa uwasilishaji wa majina ya wajumbe wa Bodi ya Zabuni kwenye Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri, kinyume na kanuni ya 7 (4) ya Kanuni za Bodi ya Zabuni ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2007 (The Local Government Authorities' Tender Boards Regulations, 2007).

Kanuni ya 7 (2) (a) Kanuni za Bodi ya Zabuni ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2007 inataka mwenyekiti wa Bodi ya zabuni awe anatoka idara isiyo na manunuzi ya mara kwa mara. Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni ya Wilaya ya Kishapu ni Mhandisi wa Maji wa Wilaya, Eng Said J. Lucas, ambapo idara yake ina manunuzi mengi. Uteuzi wake ulifanyika kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/B.20/6/256 ya tarehe 10/12/2007 na Kumb. Na. KDC/CS.10/3/66 ya tarehe 14/12/2010. Kwa mapungufu haya Bodi ya

zabuni haitakuwa na maamuzi yaliyosahihi kuhusiana na manunuzi yanayohusu Idara ya Maji**. Angalia Kielelezo E6.**

**Mapendekezo ya ukaguzi**

Halmashauri iteuwe Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni ambaye hatoki katika Idara yenye manunuzi mengi ili kuepuka kukiuka taratibu za manunuzi.

### 2.1.16 Mapungufu ya kitengo cha manunuzi na Timu za Tathimini

Timu ya manunuzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu iliundwa kwa mara ya kwanza October, 2007 kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/S.30/13/07 ya tarehe 30/10/2007. Kabla ya hapo Halmashauri ilikuwa ikifanya manununuzi bila kuwa na timu ya manunuzi. **Angalia Kielelezo E.7 na E8.**

Katika kufuatilia uundwaji wa Timu ya Tathimini ya Manunuzi ilithihilika kwamba timu mbalimbali za tathimini ya manunuzi (Evaluation Committees) zimekuwa zikiundwa bila kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 26 (6) ya Kanuni za Bodi ya Zabuni ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2007, kwani wajumbe hawakuwa wakijaza fomu ya maadili ya kukiri na kuthibitisha kuwa hawana mgongano wa maslahi kwenye mikataba ya manunuzi wanayotathimini. Kutojaza fomu kuthibitisha mgongano wa kimaslahi kunaweza kupelekea maamuzi yakafanywa kwa upendeleo.Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi.

## 2.2 Mapungufu katika Malipo mbali mbali

### 2.2.1 Hati za malipo hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi Shs.1,171,735,534.33

Baada ya kupitia majibu ya Halmashauri ya ripoti ya ukaguzi kuwa hati za malipo ambazo hazikuwasilishwa kwa ukaguzi zenye thamani ya Sh.1,393,123,804 za mwaka wa fedha 2009/2010, hati za malipo zenye kiasi cha Sh.226,412,192.17 zilipatikana na kuwasilishwa kwa ukaguzi, hivyo kubakia hati za malipo zenye jumla ya Sh.1,171,735,534**.** kama inavyooneshwa katika **Kiambatanisho “A”** Kwa kukosekana hati hizo za malipo uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitishwa.

**Mapendekezo ya ukaguzi**

Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuhakikisha Mweka Hazina wa Halmashauri anahusika na usimamizi wa nyaraka hizi muhimu kama ilivyo katika Agizo Na.96 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya 1997. Pia unatakiwa kuteua Mhasibu mmoja ambaye atahakikisha hati zote za malipo zinakuwa na viambatanisho vyake na zinatunzwa katika hali ya usalama na

kuhakikisha kunakuwa na chumba maalum kwa ajili ya kuhifadhi hati za malipo na Mhasibu huyo atawajibika kwa upotevu wowote utakaojitokeza.

### 2.2.2 Uwepo malipo ya hundi yaliyofanywa kwa sahihi moja kinyume na taratibu za malipo Sh.6, 455,080

Ukaguzi maalum ulibaini kuwepo kwa malipo ya hundi zenye thamani ya Sh.6,455,080 yaliyolipwa kwa saini moja kutoka akaunti namba 3071200077 ya Elimu iliyopo NMB tawi la Manonga – Shinyanga, kinyume na Agizo Na. 181 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997. Malipo hayo ni kama yalivyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

| Na | JINA LA MLIPWAJI | NAMBA YA HUNDI | KIASI (SH.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Mwl. Hildergarda Luhosho | 097033 | 1,570,280 |
| 2 | Mwl. Wilson Lukonge | 097034 | 1,599,800 |
| 3 | Mwl. Nyaswe Stanslaus | 097030 | 1,095,000 |
| 4 | Mwl. Herry Kamarara | 097031 | 1,095,000 |
| 5 | Mwl. Mahola John | 097032 | 1,095,000 |
| | **JUMLA** | | **6,455,080** |

Kutozingatia matakwa ya kanuni za fedha kunapelekea kulipwa kwa malipo yasiyokuwa na uhalali kwa sahihi ya mtu mmoja. **Angalia Kielelezo F.**

**Mapendekezo ya ukaguzi**

Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuzingatia Sheria na Kanuni za fedha ili kuepusha mianya ya ubadhirifu wa fedha.

## 2.3 Manunuzi ya Vifaa na Huduma

### 2.3.1 Kutozingatia Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma

Katika kufanya tathmini ya taratibu za manunuzi kulingana na Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2005 ukaguzi huu maalum umebaini kasoro na mapungufu mbali mbali kama vile Mkuu wa kitengo cha usimamizi wa manunuzi (PMU) kimakosa anaripoti na yupo chini ya Mweka Hazina. Hii ni kinyume na Kanuni Na. 22 (5) za Kanuni za Manunuzi ya Serikali za Mitaa (GN 177) ya mwaka 2007 ambayo inamtaka Mkuu wa Kitengo hicho aripoti moja kwa moja kwa Afisa Masuuli (Accounting Officer).

Pia, mpango wa mwaka wa manunuzi haukutayarishwa kulingana na kufuata mwongozo (templates) zilizotolewa na PPRA. Mpango huo hauoneshi muda wa Zabuni, unaoonesha aina ya Zabuni na bajeti tu na Halmashauri haitumii nyaraka za tenda mahsusi zenye viwango (Standard Tender Documents) ambazo hutolewa na PPRA kinyume na Kanuni 83 (3) ya G.N. No. 97 ya mwaka 2005.

Kanuni Na.54 (1) ya G.N. Na. 97 ya mwaka 2005 inataka nyaraka za Zabuni (Bidding documents) na aina za manunuzi (Procurement methods) kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni, kabla ya kutolewa kwa washindani (Wazabuni). Kinyume na kanuni hiyo, kitengo cha usimamizi wa manunuzi na Idara zinazofanya manunuzi ndiyo zinazofanya uidhinishaji.

Afisa Masuuli hajateua Kamati za kukagua na kukubali (Good Inspection/(Acceptance) bidhaa na vifaa vilivyonunuliwa na kulikuwa hakuna taarifa yeyote ya ukaguzi wa vifaa/bidhaa zilizonunuliwa kinyume na kanuni 126 na 127 ya tangazo la Serikali (G.N) Na. 97 la mwaka 2005 na taarifa za maendeleo na utekelezaji wa mikataba za siku, wiki na mwezi hazikutayarishwa kinyume na Kanuni Na. 125 ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2005.

Uchambuzi wa Zabuni haufuati miongozo ya tathmini (Evaluation Guidelines inayotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) na vilevile mihtasari ya ufunguzi wa Zabuni haiambatanishwi kwenye taarifa za uchambuzi. Pia, wakati mwingine wajumbe wa timu ya uchambuzi hawasaini fomu za kiapo (Covenant forms) kinyume na kanuni Na. 25 (6) ya manunuzi katika Serikali za Mitaa ya mwaka 2007 na kifungu 37 (6) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004.Kutofuata sheria na kanuni za manunuzi ya umma kunaweza kupelekea fedha za Halmashauri kutumika kufanya manunuzi yasiyopangwa na yasiyohalali.

**Mapendekezo ya ukaguzi**

Ninapendekeza Halmashauri kuwa na Mpango wa mwaka wa manunuzi utayarishwe kulingana na mwongozo wa PPRA kwa kuonyesha muda wa zabuni na mengineyo. Pia Halmashauri itumie nyaraka za tenda mahsusi zenye viwango (Standard Tender Documents) zilizotayarishwa na PPRA.

Vile vile nyaraka za Zabuni (Bidding documents) na aina za manunuzi (Procurement methods) ziidhinishwe na Bodi ya Zabuni kabla ya kutolewa kwa Wazabuni na Afisa Masuuli awe anateua Kamati za kukagua na kukubali (Goods inspection/ acceptance) bidhaa na vifaa vinavyonunuliwa.

**Mapendekezo ya ukaguzi**

Pamoja na mapendekezo hayo hapo juu, taarifa za maendeleo na utekelezaji wa mikataba za siku, wiki na mwezi zitayarishwe kulingana na

kanuni husika na uchambuzi wa zabuni ufuate miongozo ya tathmini (Evaluation Guidelines) inayotolewa na PPRA.

### 2.4 Masuala Ya Mishahara

#### 2.4.1 Mishahara ya watumishi ambao hawako kazini kiasi cha sh. 66,325,161.88

Katika kupitia malipo ya Mishahara ukaguzi maalumu uligundua kuwepo Mishahara ya watumishi ambao hawako kazini kuwa katika orodha ya Mishahara kiasi cha Sh. 66,325,161.88. Kati ya kiasi hicho Sh. 43, 854,576.66 zilihusu watumishi ambao hawako kazini kwa sababu za kustaafu, malipo yaliyolipwa mara mbili, kufariki, kufukuzwa, kuacha kazi na kutoripoti kazini na majina yao kuendelea kuwemo katika orodha ya mishahara (Pay roll) bila kufutwa na hakuna uthibitisho kama fedha hizi zinarudishwa Hazina kupitia Ofisi ya katibu Tawala wa Mkoa kama inavyotakiwa na waraka wa Hazina wenye kumb. Na. EB/AG/5/03/01/Vol. iv/136 wa tarehe 31/8/2007.

Mishahara kwa wafanyakazi waliobainika kuwa watoro kwa takribani kati ya miezi mitatu hadi saba yenye jumla ya Sh. 22,470,585.22 na hakuna hatua zozote stahiki za kinidhamu zilizochukuliwa na mamlaka za nidhamu kinyume na Kifungu F.16 (1) cha kanuni za kudumu (standing orders) ya Mwaka 2009 za wafanyakazi wa Serikali. Hali hii inatokana na udhaifu katika udhibiti wa masuala ya mishahara hivyo Kupelekea fedha za mishahara isiyolipwa kutumika katika mtumizi yasiyokusudiwa. **Angalia kiambatanisho "B" na Angalia kielelezo F.2 na F.3**

**Mapendekezo ya ukaguzi**

Kitengo cha mishahara kiimarishwe kwa lengo la kushughulikia masuala ya mishahara ili kuzuia mapungufu yaliyojitokeza, na Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuhakikisha mishahara ya kiasi cha Sh.66,325,161.88 inarejeshwa na kulipwa Hazina.

#### 2.4.2. Makato ya mishahara ambayo hayajalipwa kwenye Taasisi husika Sh.281,954,806

Katika kupitia hesabu za mwaka 2009/2010 akaunti ya Amana (Deposit), orodha ya mishahara na kulinganisha na daftari la fedha (Cash Book) ilibainika kuwa kiasi cha Sh. 281,954,806.30 ikiwa ni makato ya mishahara ya watumishi ambayo hayakuwasilishwa katika Taasisi husika kinyume na Agizo Na. 309 la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 1997 kama ilivyoonesha katika **Kiambatanisho "C".** Hali hii inatokana na udhaifu katika udhibiti wa masuala ya mishahara hivyo kupelekea fedha za

makato yasiyolipwa kutumika katika mtumizi yasiyokusudiwa na Halmashauri kudaiwa na Taasisi husika.

**Mapendekezo:**
Menejimenti ya Halmashauri ihakikishe kwamba makato haya yanalipwa katika Taasisi husika.

## 2.5 Mapato ya Halmashauri

### 2.5.1. Mapungufu katika mikataba ya ukusanyaji ushuru wa masoko na Magulio

Katika kupitia mikataba ya uwakala wa ukusanyaji ushuru wa masoko na magulio Halmashauri haikuweza kutoa orodha na mikataba ya mawakala wa kukusanya ushuru katika vyanzo mbalimbali yakiwemo masoko na magulio kwa miaka ya 2007/2008 na 2008/2009 ili iweze kupitiwa wakati wa Ukaguzi.

Katika kupitia mikataba ya 2009/2010 iliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, mapungufu kadhaa yamebainika ikiwa ni pamoja na kutoonesha, kumbukumbu namba za mikataba, pia haina dhamana ya usalama (Security Bond). Hali hii inatokana na utunzaji usiofaa wa kumbukumbu na kutohusishwa kwa Mwanasheria. **Angalia vielelezo G.1.**

**Mapendekezo ya ukaguzi**
Napendekeza kuwa Halmashauri kupitia Wanasheria na atendaji wake kuhakikisha kwamba mikataba inakuwa na vipengele vyote muhimu kwa manufaa ya Halmashauri na
kuimarisha kitengo cha utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka zote ili kuzuia upotevu.

### 2.5.2. Madeni ya ushuru wa pamba ambayo hayajawasilishwa Sh.63,060,363

Kulingana na Sheria ya Fedha Na. 9 ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (Local Government Finances Act, 1982) kifungu cha 7(1) (c) inayozitaka Halmashauri za Wilaya kukusanya mapato yake kutokana na ushuru mbalimbali ikiwemo ushuru wa pamba. Aidha Halmashauri iliingia mikataba ya ununuzi wa pamba na makampuni mbalimbali kwa makubaliano ya kutoza asilimia tano (5%) kwa bei ya kununulia.

Timu ya ukaguzi maalum ilibaini kuwa kiasi cha Sh.63, 060,363 hadi kufikia mwezi
Juni 2011 kilikuwa hakijawasilishwa katika Halmashauri kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini na katika barua yenye Kumb. Na. KDC/f10/1/VOLII/87 ya tarehe 17/06/2010. **Angalia kielezo G.2.**

| Na. | Maelezo | Kiasi ( Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | Shirecu (1994) Ltd | 34,992,223 |
| 2. | Jambo oil mill & Gineries | 20,283,140 |
| 3. | MSK Solutions Co. Ltd | 7,785,000 |
| | **Jumla** | **63,060,363** |

Kutokusanywa kwa mapato haya kunatokana kutokuwepo kwa juhudi madhubuti za kufuatilia na kudai madeni ya Halmashauri kutokana na vyanzo vilivyopo. Hali hii inapelekea kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa kutokana na upungufu wa mapato.

**Mapendekezo:**
Halmashauri iweke mikakati madhubuti ya kufuatilia mapato yatokanayo na ushuru wa pamba ili kuhakikisha kuwa kiasi hicho kinawasilishwa ikiwa ni pamoja na kufuatilia mikataba hiyo ili kutoza tozo itokanayo na ucheleweshwaji.

### 2.5.3 Mapato yasiyowasilishwa na Mawakala wa kukusanya mapato Sh.32, 230,000.

Comment [u5]: Weka Sababu, Athari na Mapendekezo.

Katika kupitia nyaraka mbalimbali za halmashauri ikiwemo mikataba ya ukusanyaji ushuru pamoja na rejista mbalimbali kwa mwaka 2009/2010 mawakala wa kukusanya ushuru wa masoko na magulio hawajawasilisha kiasi cha Sh.32,230,000. Hali hii inatokana na ufuatiliaji dhaifu wa mawakala walioidhinishwa na Halmashauri katika kukusanya ushuru wa masoko na magulio hivyo kupoteza mapato yanayotokana na ushuru wa masoko na magulio, kama inavyoonekana kwenye **kiambatanisho “D”**

**Mapendekezo:**
Halmashauri ihakikishe inakusanya fedha zitokanazo na ushuru wa masoko na magulio pamoja na tozo.

### 2.5.4 Udhaifu wa uandishi wa rejista ya vitabu vya mapato.

Memoranda ya fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 (Local authority Financial Memorandum 1997), Agizo Na. 109 – 119 linaeleza utaratibu unaotakiwa katika mapokezi ya fedha na vitabu vya mapato.Katika kupitia rejista ya vitabu vya mapato ilibainika kwamba vitabu vya mapato vimekuwa vikirekodiwa katika utaratibu usio sahihi kama ifuatavyo:

- Vitabu kutorekodiwa na kutolewa katika mtiririko maalum wa namba (serial number).
- Kutoonesha majina ya watu au maafisa waliochukua vitabu hivyo pamoja na sahihi zao wakati wanaporudisha vitabu hivyo.
- Kufutwafutwa kwa rejista ya kupokelea vitabu bila kufuata utaratibu maalum.

- Uandishi usio sahihi wa risiti za kupokelea mapato mfano kutoandika maelezo ya yanayothibitisha shughuli ambayo pesa hiyo imekusudiwa.
- Mweka hazina kutosimamia utunzaji wa rejista ya vitabu vya mapato ambapo

kunaweza kusababisha upotevu wa vitabu vya mapato **Angalia kielelezo. G.3**

**Mapendekezo ya ukaguzi**

Halmashauri ya Kishapu ihakikishe kuwa rejista ya vitabu vya mapato inatunzwa vizuri ili kuwa na kumbu kumbu nzuri za mapato ya Halmashauri na kuzuia upotevu wa fedha.

### 2.5.5 Vitabu 43 vya risiti havikupatikana wakati wa ukaguzi

Timu ya ukaguzi ilipofanya zoezi la ukaguzi wa vitabu vya kupokelea fedha na rejista ya kumbukumbu ya vitabu vya mapato (counter foil regester) ilibaini kuwa kulikuwepo na jumla ya vitabu 43 ambavyo havikupatikana kwa ajili ya ukaguzi.Vitabu vinapotea kwa kutokuwa makini katika utunzaji na upokeaji wa vitabu vya mapato hivyo kutoweza kujua kama mapato yaliyokusanywa yamepokelewa na Halmashauri. **Angalia Kiambatanisho "E" na Kielelezo C.6.**

**Mapendekezo ya ukaguzi**

Halmashauri kupitia mhasibu wa mapato na mtunza fedha ihakikishe kuwa vitabu hivyo vinapatikana ili kuweza kujua kiasi cha fedha kilichokusanywa kutokana na vitabu hivyo.

### 2.5.6 Makusanyo ya fedha yaliyoonekana kwenye daftari la fedha (Cash Book) lakini hayakufika benki Sh.8,147,412

Uhakiki uliofanyika katika stakabadhi zilizopokelea fedha, taarifa za benki na usuluhisho wa benki pamoja na daftari la fedha kwa mwaka 2009/2010, ulibaini kwamba kiasi cha fedha cha jumla ya Sh.8, 147,412 hakikupelekwa benki kinyume na Agizo namba 111 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997. Katika mahojiano na wahusika Bwana Abimael Kilasi na Bwana Saidi Benta walibainisha kuwa makusanyo hayo hayakupelekwa benki kama ifuatavyo:

| Jina la Akaunti | Cheki Namba. | Tarehe | Maelezo | Kiasi (Shs) |
|---|---|---|---|---|
| General fund | 0127655/100923 | 15/9/2009 | Meneja NMB Manonga- Pesa iliyorudishwa baada ya kutolipwa wafanyakazi | 540,241 |
| " | 0127694 | 8/10/2009 | Halmashauri ya wilaya kishapu- Pango la nyumba Septemba, 2009 | 159,816 |
| " | 0131305/132 | 10/6/2010 | Roko Investment Co. – | 3,000,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 363 | | malipo ya awali ya ushuru wa pamba | |
| " | 0131321/081 098 | 18/6/2010 | Vearrian TZ Ltd-Cotton malipo ya awali ya ushuru wa pamba | 3,750,000 |
| **Jumla ndogo (Sh)** | | | | **7,450,057** |
| Cash | 0123380/205 062 | 29/6/2010 | Mchango wa mfuko wa afya ya jamii kutoka NHF | 90,790 |
| | 0123381/205 085 | 29/6/2010 | Mchango wa mfuko wa afya ya jamii kutoka NHF | 606,565 |
| **Jumla ndogo (Sh)** | | | | **697,355** |
| **Jumla kuu (Sh.)** | | | | **8,147,412** |

Mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani ndio chanzo cha fedha kutopelekwa benki huu ni ubadhirifu wa fedha za umma.

**Mapendekezo ya ukaguzi**
Halmashauri ihakikishe kuwa fedha hizo zinarudishwa na kupelekwa benki kama sheria na taratibu za fedha zinavyotaka.

## 2.6 Ubadhirifu wa fedha uliofanyika katika Halmashauri Sh. 5,513,049,264

Katika kupitia taarifa za fedha zilijumuisha daftari za fedha (cash books) hundi zilizolipwa, taarifa za benki (Bank Statements, vitabu vya hundi) Timu ya ukaguzi ilibaini matukio ya ubadhirifu yenye jumla ya Sh.5,513,049,264. Watuhumiwa wa hujuma zilizoainishwa ni Cashier Walugu Mussa Limbe Watumishi/Mtumishi wa NMB Tawi la Manonga Shinyanga Mweka Hazina Muhidini Mohamedi Boniface Nkumiming na Mhandisi Leonard Mashamba ambao wametajwa katika barua yenye Kumb.Na. KDC/C.A/30/3/32 ya tarehe 3/9/2010 iliyoandikwa na Mkurugenzi wa Halmashauri kwenda kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga. **Angalia Kielelezo H1.** Ubadhirifu ni kama unvyoonyeshwa katika aya ndogo zifuatazo:

### 2.6.1 Ubadhirifu wa fedha Katika Akaunti za Halmashauri Sh.754,064,591

Timu ya ukaguzi ilipitia nyaraka mbalimbali zikiwemo taarifa za Benki statements, hundi zilizolipwa, vibutu vya hundi, daftari za fedha (cash books), mipango kazi, taarifa za utekelezaji na mapato na matumizi ya fedha za mradi.

Pia ilifanya mapitio ya kitabu cha mahesabu cha mfumo wa mahesabu wa elektroniki (System Cash book) za Akaunti za Halmashauri kwa Mwaka 2009/2010 na mahojiano na kaimu Mweka Hazina ndugu Oscar Msalikwa pamoja na Mhasibu mkuu wa anayesimamia kitengo cha Mfumo wa

Hesabu wa Kielekitroniki Ndugu Abimaeli Kilasi ilibainika kuwapo na malipo yenye jumla ya Sh.754,064,591 yaliyoainishwa kama malipo yasiyojulikana (Unknown Payments) yaliingizwa kwenye kitabu cha hesabu kama malipo yaliyokuwa yakifanyika kupitia NMB Tawi la Manoga bila idhini ya Mkurugenzi na kinyume Na. Agizo 181 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa za 1997.

Ukaguzi maalum ulibaini kuwa ubadhirifu ulifanywa kwa mbinu na njia mbalimbali kama vile malipo kufanyika bila kuidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na njia nyinginezo kama ifuatavyo:

- Malipo yaliyofanyika bila hati za malipo hivyo kulipwa na benki bila kuidhinishwa.
- Malipo ya hundi zilizolipwa na benki wakati zikiwa zimesainiwa na watia sahihi ambao sio walioidhinishwa kusaini hundi za akaunti husika.
- Malipo yaliyolipwa zaidi na benki kuliko kiasi kilichoandikwa kwenye hati za Malipo.
- Malipo yaliyolipwa zaidi na benki kuliko kiasi kilichoandikwa kwenye vibutu vya hundi na kiasi kilichoonyeshwa katika daftari za fedha (cash books).
- Malipo yaliyolipwa kupitia hundi zilizo futwa (Cancelled cheques)
- Uhamishaji wa fedha toka akaunti moja kwenda nyingine kwa lengo la kuziba pengo la fedha zilizoibiwa au kuhamishia fedha kwenye akaunti ambazo ni rahisi huzihujumu.
- Kutohamisha fedha toka akaunti ya miradi zinazofikia akaunti ya Maendeleo hivyo kuchotwa kupitia akaunti ya maendeleo.

Timu ya Ukaguzi kupitia Barua zenye Kumbukumbu Na. KDC/S.10/4/14 ya tarehe 3/6//2011 , KDCC/CS.10/4/32 ya tarehe 9/6/2011, KDC/AM/VOL III/3 ya terehe 3/6/2011, KDC/AM/VOL III/7 ya tarehe 22/6/2011 na KDC/AM/VOL III/6 ya tarehe 21/6/2011 ziliandikwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kishapu kumtaka Meneja - NMB Tawi la Manonga ili Timu ya Ukaguzi iweze kukutana na Meneja kwa Mahojiano na kupatiwa nyaraka mbali mbali kama vile hundi zilizolipwa (paid cheques, orodha za watia sahihi katika akaunti za Halmashauri ( Specimen Signature ) na vyeti vya kuonesha salio ( Certificate of balance) kwa ajili ya uhakiki. **Angalia Kielelezo Na. H1-H6**

Pia timu ya ukaguzi iliombwa orodha za watia sahihi wa akaunti 20 za Halmashauri zilizoko NMB, lakini Meneja wa Benki hakuweza kuzitoa kwa ajili ya ukaguzi.

Timu ya Ukaguzi ilifanikiwa kupata Hundi zilizolipwa 188 kati ya hundi 346 (paid cheques), toka kwa Afisa wa Polisi toka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi anayeendelea na upelelezi wa tuhuma za Halmashauri ya Kishapu na hundi zingine zilipatikana toka Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga, hivyo kubakia hundi 158 ambazo benki imeshindwa kuzitoa kwa ajili ya ukaguzi.

Hata hivyo uongozi wa Benki NMB Tawi la Manonga lililoko Shinyanga Mjini kwa barua yake yenye Kumbukumbu Na NMB/KDC/AC/01/06 ya tarehe 21/6/2011 ikibainisha kuwa Uongozi wa Benki hauko tayari kumpatia Mkurugenzi wa Halmashauri hundi zilizolipwa.

Nyaraka zilizohitajika na timu ya ukaguzi hazikuweza kupatikana toka kwa Meneja wa Benki hivyo kufanya zoezi zima la ukaguzi wa kuhakiki uhalali wa malipo husika kushindikana. **Angalia Kielelezo H.7**

### 2.6.2 Taarifa za benki zilizoghushiwa Sh.235,057,185.64

Katika kupitia na kufanya ulinganisho wa taarifa za benki (Bank Statements) pamoja na vyeti vya Salio (Certificates of Balances) za akaunti mbalimbali za Halmashauri kwa 2008/2009 ambazo Timu ya ukaguzi ilizipata toka NMB Tawi la Manonga na zile zilizotumika kufunga hesabu za mwisho za mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2009 ilibainika kuwa zimeghushiwa na kutumika kufanya usuluhisho wa benki ambazo zilisainiwa na Mweka Hazina Ndugu Muhidini Mohamedi na kupelekea salio la akaunti hizo kuwa na tofauti ya Sh.235,057,185.64 ambazo tayari zilikuwa zimeshaibiwa toka katika akaunti hizo kwa njia mbalimbali kama vile malipo yasiyo na hati za malipo lakini yaliweza kulipwa Benki na kuongezwa kwa tarakimu katika hundi ikilinganishwa na vibutu vya hundi husika.

Akaunti zilizohusika kughushiwa kwa taarifa za Benki ni kama zinavyooneshwa hapo chini:

| Na. | Namba ya akaunti | Jina la akaunti | Salio halisi (Shs) | Salio lililoghushiwa (Shs) | Tofauti (Shs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | CA 3071200113 | RSWSSP | 13,881,731.20 | 119,973,731.20 | 106,092,000.00 |
| 2 | CA 3071200104 | DEVELOPMENT II | 712,532.54 | 83,951,842.54 | 83,239,310.00 |
| 3 | CA 3071200077 | ELIMU | -3,841,501.42 | 9,268,498.58 | 13,110,000.00 |
| 4 | CA 3071200081 | Misc DEPOSIT | -8,964,464.51 | 2,871,411.13 | 11,835,875.64 |
| 5 | CA 3071200091 | CHF | 178,325.75 | 20,958,325.75 | 20,780,000.00 |
| | | | **1,966,623.56** | **237,023,809.2** | **235,057,185.64** |

**Angalia vielelezo vifuatavyo**: Taarifa za Benki (Banki statements) zilizohalisi **J1 - J5**.Taarifa za Benki (Banki statements) zilizogushiwa **J6 - J10** .Vyeti vya salio (Certificate of balances) vilivyohalisi **K1 - K5**.Vyeti vya salio (Certificate of balances) vilivyogushiwa **K6- K10.** Usuluhisho wa Benki (Bank Reconciliation satatements) zilizogushiwa **L1- L5.**

Hata hivyo uongozi wa Halmashauri ulikwisha baini kuwepo kwa tatizo katika taarifa za benki zilizoghushiwa na hatua zilizochukuliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ni kuiandikia benki ya NMB Tawi la Manonga kwa barua zenye Kumb. KDC/S.10/27/130 ya tarehe 6/08/2010, KDC/S.10/27/119 ya tarehe 09/7/2010 na KDC/S.10/27/120 ya tarehe 29/07/2010. **Angalia vielelezo M 1, M 2 na M 3**

Comment [a6]: Barua za DED

Aidha kulikuwepo na mrejesho kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kwa barua ya tarehe 5/6/2010 na zenye Kumb. Na. NMB/KDC/OP ya tarehe 29/7/2010 na NMB/KDC/21/08 ya tarehe 21/8/2010 zikisisitiza kuwa taarifa za Benki (Bank Statements) zilizotumika kufunga hesabu zinazoishia tarehe 30/6/2010 kwa akaunti zilizotajwa hapo juu hazikuwa halisi. **Angalia vielelezo M4, M5, M6**

### 2.6.3 Hundi zilizoghushiwa na kulipwa zaidi ikilinganishwa na vibutu Sh.502,155,820

Ukaguzi uliofanyika kwa kulinganisha rekodi za Halmashauri na zile za Benki, ulibaini kuwepo malipo nyenye mashaka yenye jumla ya Sh.502,155,820 yaliyotokana na uwezekano wa kugushi hundi katika akauti mbalimbali za Halmashauri. Malipo hayo ni kama ifuatavyo:

| Mlipwaji | Namba ya Hundi | Kiasi cha malipo kwenye na Hundi vitabu vya malipo(Sh.) | Tarehe fedha zilipolipwa na Benki | Kiasi cha malipo kwenye Hundi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| **A: CHF A/c** | | | | |
| Amazon Stationary | 108662 | 200,000 | | 14,620,000 |
| DED- KDC | 108663 | 640,000 | | 6,118,000 |
| DED- KDC | 108651 | Ilifutwa | 16/10/2007 | 13,626,000 |
| DED- KDC | 108658 | Ilifutwa | 12/03/2008 | 19,257,500 |
| **Jumla ndogo** | | | | **53,621,500** |
| **B: Akaunti ya Maendelo** | | | | |
| Ally Hamad Hillal | 113740 | 184,500 | 15/07/2009 | 10,500,000 |
| Ponsiani Kuhabwa | 113741 | 70,000 | 15/07/2009 | 4,240,000 |
| DED - Kishapu | 113743 | 240,000 | 15/07/2009 | 9,270,000 |
| DED - Kishapu | 113658 | 367,000 | 20/3/2009 | 3,670,000 |
| DED - Kishapu | 113674 | 260,000 | 8/7/2009 | 22,008,050 |
| DED - Kishapu | 113675 | 625,000 | 22/4/2009 | 7,000,000 |
| DED - Kishapu | 113715 | 150,000 | 15/6/2009 | 5,150,000 |
| DED - Kishapu | 113739 | 240,000 | 14/7/2009 | 5,400,000 |
| Amazon Stationery | 113665 | 459,800 | | 5,000,000 |
| Ally Hamad Hillal | 113676 | 450,000 | 4/4/2009 | 6,614,000 |
| Farles Mwenura | 113716 | 850,000 | 15/6/2009 | 5,850,000 |
| **Jumla ndogo** | | | | **196,185,050** |
| | | | | |
| **C: EGPAF A/c** | | | | |
| KDC | 112066 | ilifutwa | 29/4/2009 | 28,828,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Jumla ndogo** | | | | **28,828,000** |
| | | | | |
| **D: NRWSSP A/c** | | | | |
| DED - Kishapu | 114613 | 895,000 | 8/4/2009 | 15,000,000 |
| DED - Kishapu | 114614 | 161,630 | 09/3/2009 | 15,000,000 |
| DED - Kishapu | 114619 | 90,000 | 11/4/2009 | 20,000,000 |
| DED - Kishapu | 114620 | 625,000 | 01/6/2009 | 19,487,000 |
| **Jumla ndogo** | | | | **69,487,000** |
| | | | | |
| **D.TACAIDS A/c** | | | | |
| DED - Kishapu | 005688745 | 250,000 | 20/6/2009 | 16,250,000 |
| DED - Kishapu | 005688746 | 100,000 | 2/6/2009 | 10,000,000 |
| DED - Kishapu | 005688747 | 110,000 | 14/6/2009 | 11,000,000 |
| DED - Kishapu | 005688749 | 200,000 | 12/6/2009 | 5,200,000 |
| DED - Kishapu | 112851 | 250,000 | 12/6/2009 | 4,200,000 |
| DED - Kishapu | 005688748 | 400,000 | 3/4/2009 | 40,400,000 |
| **Jumla ndogo** | | | | **87,050,000** |
| | | | | |
| **E. DASIP A/c** | | | | |
| DED - Kishapu | 005724539 | 350,000 | 22/12/2008 | 98,000,000 |
| DED - Kishapu | 112261 | ilifutwa | 31/03/2009 | 15,000,000 |
| DED - Kishapu | 112262 | ilifutwa | 4/03/2009 | 20,000,000 |
| DED - Kishapu | 112251 | ilifutwa | 17/02/2009 | 53,453,000 |
| DED - Kishapu | 112253 | ilifutwa | 13/02/2009 | 13,731,270 |
| **Jumla ndogo** | | | | **200,184,270** |
| **Jumla Kuu** | | | | **502,155,820** |

Hundi Na. 112066,114614, 108651, 105658, 112261, 112262, 112251, na 112253 zinaonesha kwenye vitabu vya malipo (Cash book) na vibutu kuwa zilifutwa (Cancelled) lakini katika taarifa za benki (Bank Statements) zinaoneshwa zililipwa katika mtiriko wa tarehe 29/4/2009, 09/3/2009, 16/10/2007, 12/03/2008, 31/03/2009, 4/03/200917/02/2009 na 13/02/2009. **Angalia vielelezo ;Akaunti ya CHF- N1- N 6, Akaunti ya Maendeleo - P1 - P19, EGPAF- Q1 na Q2 , NRWSSP- R1 -R4, TACAIDS - R5 - R11, DASIP – R12 - R20.**

### 2.6.4 Uhamisho wa fedha toka akaunti Moja kwenda nyingine bila idhini ya Mkurugenzi na kutumika kinyume na malengo Sh.1,676,246,259

Katika kupitia hati za malipo na daftari la fedha kwa mwaka 2009/2010 ilibainika kuwa jumla ya Sh.1, 676,246,259 zilihamishwa kutoka akaunti moja kwenda nyingine bila idhini ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na zikatumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa , kwani fedha hizi zilitakiwa kutumika katika akaunti husika kwa shughuli zilizokusudiwa na zilizoidhinishwa katika bajeti ya Halmashauri ambapo fedha zilihamishwa kutoka katika akaunti za miradi ambazo kimsingi hazitakiwi kufanya uhamisho wa fedha isipokuwa kwa kibali maalum cha Afisa Masuuli na idhini ya Kamati ya Fedha na Mipango kwa mujibu wa kifungu cha 10 (3) cha

Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya 1982. **Kiamabatanisho "F", pia angalia vielelezo T1 - T20 vyahusika.**

Aidha, Uhamisho huo ulifanywa kwa malengo ya kuficha ubadhirifu katika akaunti ambazo fedha zake zilikwishatumika isivyo halali kwa kulipwa hati za malipo ambazo hazikuidhinishwa na Mkurugenzi, malipo yaliyofanyika bila hati za malipo kulipwa na benki, Malipo ya hundi zilizolipwa na benki wakati zikiwa zimesainiwa na watia sahihi ambao sio walioidhinishwa kusaini hundi za akaunti husika na Malipo yaliyolipwa zaidi na benki kuliko kiasi kilichoandikwa kwenye hati za Malipo.

Akaunti ambazo zilihusishwa kuhamisha fedha ni kama zinavyoonekana katika jedwali hapa chini:

| Jina la Akaunti iliyohamisha fedha | Kiasi kilichohamishwa (Sh.) |
|---|---:|
| UJENZI | 8,000,000 |
| Maji Mjini | 480,000 |
| DASIP | 149,906,500 |
| LGCDG | 60,068,000 |
| VIJIJI | 29,800,000 |
| Elimu | 381,331,282 |
| Maendeleo | 271,176,500 |
| Mfuko wa Elimu | 12,500,000 |
| Maboresho | 171,000 |
| Maji | 10,360,000 |
| Rwssp | 174,482,569 |
| CHF | 12,358,000 |
| Barabara | 224,660,000 |
| Kilimo | 9,110,000 |
| EGPAF | 53,000,000 |
| Ukimwi | 66,700,000 |
| G/Fund | 213,399,336 |
| Sekondari | 2,930,000 |
| Afya | 170,295,641 |
| **Jumla Kuu** | **1,676,246,259** |

### 2.6.5 Uhamisho wa fedha ambao haukufika katika akaunti zilikohamishiwa Sh.1,957,659,279

Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Halmashauri ilifanya uhamisho wa fedha wenye jumla ya Sh.1, 957,659,279 Kutoka akaunti moja kwenda nyingine. Uchambuzi ulifanywa katika daftari za malipo (System Cash Books) na taarifa za Benki (Bank Statements) za akaunti zilizolipa zikionesha kutoa fedha hizo kuhamishiwa akaunti zingine lakini zilipofuatiliwa katika daftari za fedha na Taarifa za Benki fedha hizo hazikuwa zimepokelewa kama inavyooneshwa katika **kiambatanisho "G"** na **Angalia vielelezo T1 - T20**

**Comment [a7]:** KANUNI, vielelezo

Hali hii inadhihirisha kuwa kiasi cha fedha chenye jumla ya Sh.1,957,659,279 kilichohamishwa toka akaunti moja kwenda nyingine zilichukuliwa fedha taslimu na Mtunza fedha wa Halmashauri.

### 2.6.6 Uhamisho wa fedha kwenda kwenye akaunti zisizofahamika Sh.452,379,678

Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Halmashauri ilifanya uhamisho wa fedha wenye jumla ya Sh.452,379,678 kutoka akaunti moja kwenda katika akaunti zisizofahamika bila kuidhinishwa na Mkurugenzi na ulifanyika bila hati za malipo hivyo kulipwa na benki bila kuidhinishwa. Wahusika ni watumishi Bw. Walugu Musa Limbe ambaye ni Mtunza Fedha, Watumishi /Mtumishi wa benki ya NMB tawi la Manonga Shinyanga na Mweka Hazina Bw. Muhidini Mohamedi ambao wametajwa katika barua yenye kumb. Na. KDC/C.A/30/3/32 ya tarehe 3/9/2010 iliyoandikwa na Mkurugenzi wa Halmashauri kwenda kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga.

Uchambuzi ulifanywa katika daftari za malipo (System Cash Books) na taarifa za Benki (Bank Statements) za akaunti zilizolipa zikionesha kutoa fedha hizo lakini zilipofuatiliwa katika daftari za fedha na taarifa za Benki fedha hizo hazikuonesha kupokelewa katika akaunti au kutumika katika matumizi ambayo hayakuelezwa kama inavyoonekana katika **kiambatanisho "H" na Angalia vielelezo T1 - T20 Na Angalia vielelezo J.**

Comment [a8]: KANUNI, vielelezo

### 2.6.7 Malipo yaliyofanyika kwa walipwaji wasiofahamika Sh.689,551,042

Katika kupitia daftari la malipo (cash books) na taarifa za Benki (Bank statements) za mwaka 2009/2010 kulibainika kuwepo kwa malipo yenye jumla ya Sh.689,551,042 yaliyofanyika kwa walipwaji wasiojulikana. **Angalia vielelezo: U1 - U8.**

Aidha,malipo hayo yaliingizwa katika daftari la fedha ikiwa ni kuanisha malipo yaliyoghushiwa ambayo yalilipwa na Benki toka akaunti mbalimbali za Halmashauri. Zifuatazo ni mbinu mbalimbali zilizotumika kuhujumu fedha hizo za Halmashauri:

- Kulipwa kwa malipo yasiyokuwa na hati za malipo.
- Benki ya NMB tawi la Manonga Shinyanga kulipa malipo zaidi ya yaliyoidhinishwa katika hati za malipo na vibutu vya hundi, hivyo kuwepo na malipo yasiyoidhinishwa na yaliyo zaidi ya yaliyoingizwa katika vitabu vya Halmashauri.
- Malipo kufanyika kwa hundi kusainiwa na watumishi wasioidhinishwa kusaini hundi za akaunti husika hivyo kupelekea malipo hayo kulipwa na Benki na kuwa ni malipo batili na hatimaye kutoingizwa katika daftari la fedha kama inavyoonekana katika **kiambatanisho "I".**

Ubadhirifu wa Sh.5,513,049,264 uliobainika katika aya 2.6 ulifanywa na wahusika waliotajwa kwa barua yenye kumb. Na. KDC/C.A/30/3/32 ya

tarehe 3/9/2010 iliyoandikwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kishapu kwenda kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga ambao ni:

- Mtunza Fedha Bw. Walugu Mussa Limbe.
- Watumishi/Mtumishi wa NMB Tawi la Manonga Shinyanga.
- Mweka Hazina Muhidini Mohamedi na
- Mhandisi Leonard Mashamba
- Boniface Nkumingi
- Mussa Kilulya na
- Sarai Pura

Kukosekana kwa uaminifu na uadilifu wa baadhi ya watumishi wa idara ya fedha na maafisa wengine na Mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani baada ya kuanzishwa kwa Halmashauri mpya. Ubadhirifu huu umesababisha kutotekelezwa kwa shughuli na malengo yaliyokusudiwa hasa miradi ya maendeleo katika nyanja mbalimbali. **Angalia vielelezo H1**

**Mapendekezo**

- Mamlaka husika iwachukulie hatua zinazofaa watumishi waliohusika na upotevu wa fedha jumla ya Sh.5,513,049,264 kwa kughushi nyaraka za Benki. Pia, Halmashauri inatakiwa kufanya taratibu kwa kuwasiliana na Benki ya NMB Tawi la Manonga kuhakikisha fedha zilizochukuliwa kutokana uzembe uliotokanana Benki zinarejeshwa.
- Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuhakikisha Mweka Hazina wa Halmashauri anahusika na usimamizi wa Hati za malipo kama ilivyo katika Agizo Na.5(c) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya 1997.
- Menejimenti ya halmashauri inatakiwa kuhakikisha mfumo wa udhibiti wa ndani unaboreshwa ili kuzuia uwezekano wa wizi wa fedha.
- Halmashauri inatakiwa kurudisha fedha zote zilizotumika kinyume na taratibu haraka iwezekanavyo ili ziweze kutumika katika malengo yaliyokusudiwa.
- Menejimenti ya halmashauri inatakiwa kuhakikisha mfumo wa udhibiti wa ndani unaboreshwa ili kuzuia uwezekano wa wizi wa fedha zake.

## 2.7 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Katika kupitia kumbukumbu za fedha za miradi ya Halmashauri katika mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010 ulibaini udhaifu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo husika kama inaonyeshwa katika aya ndogo zifuatazo:

### 2.7.1 Mpango wa Taifa wa Maji Safi na usafi wa Mazingira Vijijini (NRWSSP)

#### 2.7.1.1 Matumizi ya Fedha kinyume na malengo katika mradi wa NRWSSP Sh.427,674,569

Katika kupitia stakabadhi za mapokezi na taarifa za Benki (Bank Statements) za mwaka wa fedha 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010 ilibainika kuwa Halmashauri ilipokea jumla ya Sh.1,215,919,799 kapitia akaunti ya Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi wa Mpango wa Taifa wa Maji Safi na usafi wa Mazingira Vijijini (NRWSSP) kama inavyooneshwa hapa chini:

| Tarehe zilipopokelewa Akaunti ya Maendeleo | Kiasi (Sh) | Tarehe zilipohamishiwa akaunti ya Mradi | Kiasi (Sh) | Kiasi ambacho hakihamishiwa akaunti ya mradi (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| **A: Akaunti ya Maendeleo** | | | | |
| **2008/2009** | 0 | | | |
| 17/09/2008 | 71,000,000 | 07/11/2008 | 71,000,000 | 0 |
| 30/10/2008 | 208,170,000 | 03/01/2009 | 208,170,000 | |
| 11/06/2009 | 41,212,121 | 03/07/2009 | 41,212,121 | |
| **2009/2010** | 0 | - | 0 | |
| 2/7/2009 | 198,786,828 | 30/09/2009 | 198,786,828 | |
| 10/12/2009 | 88,700,000 | - | 0 | 88,700,000 |
| | 0 | | 0 | |
| 24/06/2010 | 437,000,000 | 01/07/2010 | 437,000,000 | |
| **Jumla ndogo** | **1,044,868,949** | | **956,168,949** | **88,700,000** |
| **B: Akaunti ya Mradi - NWSSP** | | | | |
| **Tarehe zilipopokelewa Akunti ya mradi - NSSWP** | **Kiasi (Sh)** | | | |
| **2007/2008** | | | | |
| 22/5/2008 | 57,000,000 | | 57,000,000 | |
| | 0 | | 0 | |
| **2008/2009** | 0 | | 0 | |
| 2/7/2008 | 111,229,000 | | 111,229,000 | |
| **2009/2010** | 0 | | 0 | |
| 29/01/2010 | 2,821,850 | | 2,821,850 | |
| **Jumla ndogo** | **171,050,850** | | **171,050,850** | |
| **Jumla Kuu** | **1,215,919,799** | | **1,127,219,799** | **88,700,000** |

Katika kupitia nyaraka mbalimbali zikiwemo taarifa za Benki, hundi zilizolipwa, vibutu vya hundi, mipango kazi na taarifa za utekelezaji

zinazohusu mapato na matumizi ya fedha za mradi wa NRWSSP ukaguzi iligundua kuwepo ubadhirifu wa jumla ya kiasi cha Sh.603,253,569 wa fedha za mradi uliofanywa na watumishi wa Halmashauri ambao wametajwa katika kila tukio la ubadhirifu. **Angalia Kielelezo H1.**

#### 2.7.1.2 Fedha ambazo hazikuhamishwa toka akaunti ya Maendeleo kwenda akaunti ya mradi Sh.88,700,000

Mnamo tarehe 10/12/2009 Halmashauri ilipokea kupitia akaunti ya Maendeleo kiasi cha Sh.88,700,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za miradi ya Maji mpaka wakati wa ukaguzi huu mwezi Juni, 2011 takribani miezi sita tangu kupokelewa katika akaunti ya Maendeleo haijahamishiwa katika akaunti ya Mradi wa maji NRWSSP ili itumike kwa shughuli za mradi zilizokusudiwa. **Angalia kielelezo V**

#### 2.7.1.3 Matumizi yaliyofanywa kinyume na Malengo yaliyokusudiwa Sh.338,974,569

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu Na.DED/KDC/CPF.8/05 ya tarehe 19/10/2010 iliyoandikwa na Mhandisi wa Maji Wilaya Ndugu Said Lukas kwenda kwa Mkurugenzi wa Halmashauri yenye kichwa cha habari "Matumizi ya Fedha za Programme ya Maji kinyume na malengo yaliyokusudiwa" ikitanabaisha kuwepo kwa matumizi yenye jumla ya Sh.286,092,000 yaliyofanyika kupitia akaunti ya Benki kwa matumizi yasiyokusudiwa na Idara ya Maji kama mtumiaji na msimamiaji wa Mradi haikuhusishwa, ikimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri afanye uchunguzi wa ubadhirifu huo. Lakini mpaka tarehe za ukaguzi huu maalum hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na Uongozi dhidi ya barua hiyo. **Angalia Kielelezo W.**

Pia kufuatia mahojiano na Mhandisi wa Maji, ilibainika kuwa kulikuwa na matumizi mengine zaidi ya yaliyotajwa katika barua yake yenye jumla ya Sh. 52,882,569.14, ambayo pia yalifanyika benki kwa matumizi yasiyokusudiwa na Idara ya Maji kama mtumiaji na msimamiaji wa Mradi haikuhusishwa hivyo kufanya matumizi yaliyofanywa nje ya malengo ya mradi kuwa jumla ya Sh. 338,974,569.14 kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

| Tarehe | Hundi Na. | Mlipwaji | Kiasi (shs) |
|---|---|---|---|
| 09/03/2009 | 114614 | KDC - Kishapu | 15,000,000.00 |
| 08/04/2009 | 114613 | DED - Kishapu | 15,000,000.00 |
| 11/04/2009 | 114619 | Kishapu District Council | 20,000,000.00 |
| 18/05/2009 | 0 | Miscellaneous Dedit | 18,350,000.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 20/05/2009 | 114649 | KDC - Kishapu | 8,250,000.00 |
| 29/05/2009 | 114648 | KDC - Kishapu | 28,250,000.00 |
| 29/05/2009 | 114640 | KDC - Kishapu | 33,755,000.00 |
| 01/06/2009 | 114620 | KDC - Kishapu | 19,487,000.00 |
| 01/10/2009 | 114653 | KDC - Kishapu | 47,648,000.00 |
| 01/10/2009 | 114654 | KDC - Kishapu | 42,890,000.00 |
| 01/10/2009 | 114652 | KDC - Kishapu | 37,462,000.00 |
| **JUMLA NDOGO** | | | **286,092,000.00** |
| | | | |
| 15/09/2009 | 114647 | Check paid | 8,500,000.00 |
| 27/10/2009 | 114651 | KDC - Kishapu | 34,382,569.14 |
| 28/10/2009 | 114656 | KDC - Kishapu | 10,000,000.00 |
| **JUMLA NDOGO** | | | **52,882,569.14** |
| **JUMLA KUU** | | | **338,974,569.14** |

**Angalia vielelezo X1 - X7**

Ukaguzi ilipofatilia ili kupata Hati za malipo husika ili kubainisha malipo hayo yaliidhinishwa na nani na yalikuwa yanahusu nini hati hizo hazikuweza kutolewa na uongozi wa Halmashauri.

**2.7.1.4 Shughuli zilizoathirika na ubadhirifu wa fedha za Mradi**

Zifuatazo ni shughuli zenye jumla ya Sh.176,569,400 zilizoathirika kwa kutokana na ubadhirifu wa fedha za mradi, kwa Halmashauri kushindwa kuwalipa wakandarasi ambao tayari wameshaingia mikataba na Halmashauri au kutotekelezwa kabisa kwa shughuli hizo kama zilivyoainishwa katika mpango kazi ni kama ifuatavyo:

- Halmashauri ya wilaya ya Kishapu ilifunga hatua ya kwanza ya mkataba wenye thamani ya Dola za Marekani 217,450 sawa na Shilingi 353,138,800 za Tanzania (Dola 1 ya Marekani sawa na Sh. 1624 za Tanzania) na mzabuni M/S Netwas Tanzania LTD kwa Mkataba Na.LGA/108/NRWSSP/01 ili kutoa ushauri wa kitaalam na kuviwezesha vijiji 13 ndani ya Halmashauri kujiandaa kupokea miradi ya maji safi na usafi wa mazingira. Mkataba huu ulianza Oktoba, 2009 na ulitarajiwa kukamilika Januari, 2011, ili kuruhusu hatua ya pili kuanza

na hatimaye ujenzi wa miundombinu ya maji kufanyika. **Angalia kielelezo X 8.**

- Katika kufuatilia maendeleo ya mradi, wakati wa ukaguzi maalum, ilidhihirika kwamba, mkandarasi alikwishalipwa Dola za Marekani 108,725 sawa na shilingi za Tanzania 176,559,400 ikiwa ni nusu ya malipo yote. Hivyo Halmashauri haikuweza kuwa na fedha kwa ajili ya malipo ya mkandarasi kwa ajili ya awamu ya pili ambacho ni kiasi cha Dola za Kimarekani 108,725 sawa na shilingi 176,569,400 za Tanzania (Dola 1 ya Marekani sawa na Sh. 1624 za Tanzania) ambazo nazo zimetoweka katika akaunti ya mradi kutokana na ubadhirifu.

- Mkandarasi kupitia ankra Na. 3 ya tarehe 5/10/2009 akidai kulipwa malipo yake Dola za Kimarekani 43,490 bila VAT ambayo ni sawa na Shilingi za Kitanzania 70,627,760 haikuweza kulipwa kutokana na Halmashauri kuwa haina fedha za kumlipa Mkandarasi hivyo hali hii kupelekea kutokuendelea kwa awamu ya pili ya mradi ambayo kama ingekamilika, ingeruhusu ujenzi wa miundombinu ya maji safi katika vijiji husika. **Angalia kielelezo X 9.**

**Comment [u9]:** JN WEKA SHILINGI ZA TZ KWA CONTRACT SUM. Rate ya sasa ni Sh.1624

**Comment [u10]:** JN TENGENEZA TABLE INAYOONESHA WAKANDARASI AMBAO HAWAJALIPWA NA ACTIVITIES AMBAZO HAZIJATEKELEZWA KWA 2007 TO 2010

Watuhumiwa wa hujuma zilizoainishwa hapo ni, Watumishi/Mtumishi wa benki ya NMB tawi la Manonga Shinyanga na watumishi hao wametajwa katika barua yenye Kumb.Na. KDC/C.A/30/3/32 ya tarehe 3/9/2010 iliyoandikwa na Mkurugenzi wa Halmashauri kwenda kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga. **Angalia Kielelezo H1**

**Mapendekezo**

- Menejimenti ya Halmashauri iwachukulie hatua zinazofaa Bw. Walugu Mussa Limbe (Mtunza fedha na Bw. Muhidini Mohamed ambaye ni Mweka Hazina.
- Menejimenti ya halmashauri inatakiwa kuhakikisha mfumo wa udhibiti wa ndani unaboreshwa ili kuzuia uwezekano wa wizi wa fedha zake.

### 2.7.1.5 Ukarabati mradi wa maji ya bomba kijiji cha Mwamashele

Mnamo tarehe 27/02/2009 Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu iliingia mkataba namba LGA/108/2008/2009/QUICKWIN/01/C.01 na M/s Duma Works Ltd wa S.L.P 19626, Dar es Salaam, kwa ajili ya ukarabati wa bomba la maji katika kijiji cha Mwamashele. Thamani ya mkataba ilikuwa ni Sh. 66,647,000 na mkataba huu ulianza Februari 2009 na ulitegemewa kumalizika mwezi Mei 2009. **Angalia kielelezo X 10**

Mkandarasi alitakiwa kufanya kazi za ukarabati wa mradi wa bomba kama zilivyoainishwa katika BOQ.

| Na | Kazi aliyotakiwa kufanya | Thamani ya kazi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | Ukusanyaji wa vifaa | 2,000,000 |
| 2. | Ukarabati wa visima katika chanzo cha maji | 3,660,000 |
| 3. | Ukarabati wa kibanda cha pampu | 4,922,000 |
| 4. | Kununua na kufunga mabomba | 53,365,000 |
| 5. | Utengenezaji wa vioski vya maji (DP) | 2,700,000 |
| | **Jumla** | **66,647,000** |

**Angalia kielelezo X 11**

**Malipo kwa mkandarasi**

Mkandarasi huyu kwa ujumla alilipwa kiasi cha shilingi 65,147,000 kati ya gharama ya mkataba wa Sh.66,647,000, kama inavyooneshwa hapa chini:

| Namba ya Cheti cha malipo | Kiasi (Sh.) | Tarehe ya Cheti |
|---|---|---|
| Na. 01 | 60,487,000 | 03/06/2009 |
| Na. 02 | 4,660,000 | 28/10/2009 |
| **Jumla** | **65,147,000** | |

**Angalia kielelezo X 13 na X 14**

**Mapungufu yaliyojitokeza**

i. Cheti cha kumaliza kazi (certificate of completion) kilitolewa kabla ya kukamilika kwa kazi na kabla mkandarasi hajaomba kukaguliwa kwa ajili ya malipo ya mwisho. Hatimaye cheti chenye kumbukumbu namba KDC/RWSSP/10 kilitolewa tarehe 27/06/2009 na kikionesha kwamba kazi hii ilikuwa imekamilika tarehe 27/06/2009. **Angalia Kielelezo X 12.**

ii. Pia maombi ya kuongezewa muda wa kukamilisha kazi kwa wiki nne zaidi yalitolewa na mkandarasi tarehe 25/06/2009 kwa barua yenye kumbukumbu namba DWL/WP/KP/2009/001 ya tarehe 25/06/2009. **Angalia Kielelezo X 13**
Ripoti ya ukaguzi kwa ajili kutoa cheti cha pili na cha mwisho (second certificate) ilitolewa tarehe 28/10/2009 na mhandisi wa maji wa wilaya.

iii. Katika kupitia machakato wa manunuzi ilibainika kuwa tangazo la zabuni halikuidhinishwa na Bodi ya Zabuni kinyume na Kanuni Na. 80 za kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005. (**Angalia kilelezo X15).**

iv. Katika kupitia Mkataba imebainika haujaonesha tarehe maalum ya kuanza na kumalizika kwa kazi kinyume na Kanuni Na.105 za kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005.**(Angalia kilelezo Na X 16)**

v. Ukaguzi maalum ulipohitaji kupatiwa taarifa ya kamati ya tathmini, barua ya mwaliko kwa ajili ya vikao vya eneo la mradi (site) pamoja na taarifa ya vikao havikuweza kutolewa kwa uhakiki.

vi. Gharama za maji kwa matumizi ya zahanati ya Mwamashele inalipwa na wauguzi kutoka katika mifuko binafsi badala ya Serikali ya Kijiji, Uongozi wa Zahanati na Kikundi cha Watumiaji wa maji kukaa pamoja na kukubaliana utaratibu ambao utaruhusu Zahanati kutumia maji na kulipa kwa mwezi.

vii. Uvunjaji wa kanuni unatokana na kutokuwa makini kwa Watendaji wa Halmashauri katika kufuata taratibu za manunuzi na kutokuwepo kwa tarehe maalum ya kuanza na kumalizika kwa mradi kunapelekea Halmashauri kushindwa kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mkandarasi endapo mkandarasi huyo atashindwa kumaliza kazi ndani ya muda wa makubaliano na uwezekano wa Halmashauri kuingia mikataba isiyo na tija.

**Mapendekezo ya Ukaguzi**

- Mikataba inayoandaliwa izingatie taratibu zilizopo ili kuepuka gharama zisizo za lazima zinazoweza kutokea kutokana na udhaifu katika mikataba.
- Gharama za matumizi ya maji katika zahanati Mwamashele na zinginezo zigharimiwe na Halmashauri kupitia mfuko wa afya ya jamii (CHF) badala ya watumishi wa afya kununua maji kwa kutumia fedha zao binafsi.

### 2.7.1.6 Mradi wa ukarabati wa Lambo la Mwamanota uliotekelezwa kwa kutumia mfuko OC - MAJI

Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Halmashauri ilitekeleza kazi ya dharura ya kuziba Lambo la Mwamanota kwa kutumia mfuko OC - MAJI kwa mkataba Na. LGA/108/2009/10/MWD/07, iliyofanywa na mkandarasi Libra Construction Co. Ltd kwa gharama ya Sh.13, 240,050. Kazi hii ilitokana na kubomoka kwa Lambo hilo baada ya mafuriko. Nia ya ujenzi wa Lambo hilo ni kukabiliana na tatizo la ukosefu wa maji kwa ajili ya matumizi ya watu, mifugo na kilimo cha umwagiliaji.

**Angalia Kielelezo X16**

Mkandarasi alitakiwa kufanya kazi zifuatazo:

| Na | Maelezo ya kazi | Kiasi (shs) |
|---|---|---|
| 1 | Maandalizi ya vifaa | 2,700,000 |
| 2 | Kuandaa eneo la kazi | 220,000 |
| 3 | Kuchimba na kumwaga kifusi | 3,570,000 |
| 4 | Kuchimba coretreach | 135,000 |
| 4 | Kusambaza na kushindilia kifusi | 1,767,000 |
| 5 | Kurekebisha tuta | 48,000 |
| 6 | Kukinga mmomonyoko wa tuta kwa mawe | 4,800,000 |
| | **JUMLA** | **13,240,000** |

**Angalia Kielelezo X17**

**Malipo kwa mkandarasi**

Mkandarasi huyu kwa ujumla alilipwa kiasi cha shilingi 13,240,000, kama inavyooneshwa hapa chini:

| Namba ya Cheti cha malipo | Kiasi (Sh.) | Tarehe ya Cheti |
|---|---|---|
| Na. 01 | 5,000,000 | 31/05/2010 |
| Na. 02 | 4,000,000 | 30/06/2010 |
| Na. 03 | 4,240,000 | 10/08/2010 |
| **Jumla** | **13,240,000** | |

**Angalia Kielelezo X18, X19 na X20**

Timu ya ukaguzi maalum ilitembelea mradi huo na kubaini mapungufu yafuatayo:

- Lambo halikuwa na eneo rafiki kimazingira inayoliwezesha kuhimili ukosefu wa mvua kwa muda mrefu au kutoweza kuvumilia mvua nyingi.

- Lambo limevamiwa na magugu maji yanayopunguza uwezo wake wa kuhifadhi maji kwa muda mrefu.

- Mradi haukuwa na vyanzo vya maji vya kudumu, kuwa na uwezekano wa kukauka kunapokuwa na vipindi virefu vya upungufu/ukosefu wa mvua.

- Lambo linakabiliwa na mmomonyoko wa udongo uliotumika kutengeneza tuta, mmomonyoko huo unasababishwa na watu pamoja na mifugo kupita juu ya tuta pia mmomonyoko wa ardhi unatokea kutokana na tuta lililojengwa kuzunguka lambo kukosa nyasi za kulihifadhi, kiasi kwamba wakati wa mvua, udongo wa tuta unachukuliwa kwa urahisi na kupelekwa ndani ya Lambo ambalo limejaa magugu maji kama inavyooneshwa katika picha hapa chini:



*Lambo la Mwamanota likiwa linakaribia kukauka, mwezi Juni, 2011*

Sababu ni kukosa uhamasishaji wa kutunza mazingira yanayozunguka lambo na vyanzo vya maji hali ambayo inapelekea lambo kukauka na kina chake kupungua.

**Mapendekezo**

- Miradi yote ya maji inatakiwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira rafiki kwa utunzaji wa vyanzo vya maji, ili kuifanya iwe endelevu na idumu kwa vipindi vyote vya mwaka.
- Kuwe na udhibiti wa shughuli za wanadamu na mifugo ili kuzuia mmomonyoko wa ardhi unaoweza kupunguza eneo na kina cha Lambo.
- Nyasi zipandwe kenye tuta linalozunguka Lambo, ili kuzuia mmomonyoko wa ardhi usipunguze kina na ukubwa wa Lambo.
- Magugu maji yaliyoota ndani ya Lambo yaondolewe ili kuruhusu kina cha maji kuendelea kuwa kirefu na kufanya uwezo wa Lambo kuhifadhi maji uwe wa kuridhisha na wa muda mrefu.

### 2.7.2 Utekelezaji wa Miradi ya Afya

#### 2.7.2.1 Mfuko wa fedha za Afya (Health Basket Fund)

Katika kupitia stakabadhi za mapokezi na Taarifa za Benki ( Bank Statements) za mwaka wa fedha 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010 ilibainika kuwa, mnamo tarehe 10/09/2009 Halmashauri ilipokea jumla ya

Sh.1,118,993,087 kupitia akaunti ya Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi wa Mfuko wa Afya wa pamoja (Health Basket Fund) kama inavyooneshwa hapo chini:

| **Tarehe zilipopokelewa Akunti ya Maendeleo** | **Kiasi (Sh)** | **Tarehe zilipohamishiwa akaunti ya Mradi** | **Kiasi (Sh)** | **Kiasi ambacho hakikuhamishiwa akaunti ya mradi (Sh)** |
|---|---|---|---|---|
| **A: Akaunti ya Maendeleo** | | | | |
| **2007/2008** | | | | |
| 11/10/2007 | 161,532,875 | | 161,532,875 | 0 |
| 21/6/2008 | 85,800,000 | | 85,800,000 | 0 |
| **Jumla ndogo** | **247,332,875** | | **247,332,875** | |
| **2008/2009** | | | | |
| 30/10/2008 | 171,707,125 | 12/12/2008 | 171,707,125 | 0 |
| 5/2/2009 | 175,364,000 | 18/9/2009 | 175,364,000 | 0 |
| 11/6/2009 | 35,873,087 | 2/7/2009 | 35,873,087 | 0 |
| **Jumla ndogo** | **382,944,212** | | **382,944,212** | |
| **2009/2010** | | - | 0 | |
| 10/9/2009 | 244,358,000 | 4/2/2010 | 244,358,000 | |
| 2/2/2010 | 244,358,000 | - | 0 | 244,358,000 |
| **Jumla ndogo** | **488,716,000** | | **244,358,000** | **244,358,000** |
| | | | | |
| **Jumla Kuu** | **1,118,993,087** | | **874,635,087** | **244,358,000** |

Katika kupitia nyaraka mbalimbali zikiwemo taarifa za Benki, hundi zilizolipwa, vibutu vya hundi, mipango kazi na taarifa za utekelezaji zinazohusu mapato na matumizi ya fedha za mradi wa Mfuko wa Afya wa Pamoja ukaguzi iligundua kuwepo ubadhirifu wa jumla ya kiasi cha Sh.427,646,230 wa fedha za mradi uliofanywa na watumishi wa Halmashauri ambao wametajwa katika kila tukio la ubadhirifu kama inavyoainishwa katika aya ndogo zifuatazo. **Angalia Kielelezo H1**

**2.7.2.1.1 Fedha ambazo hazikuhamishiwa toka akaunti ya Maendeleo kwenda akaunti ya mradi Sh.244, 358,000**

Ilibainika kuwa kiasi cha Sh. 244,358,000 zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Afya wa pamoja mpaka wakati wa ukaguzi huu mwezi Juni 2011 takribani miezi 16-20 tangu kupokelewa katika akaunti ya Maendeleo hazijahamishiwa katika mfuko wa Afya ili zitumike kwa shughuli za mradi zilizokusudiwa kama inavyoonesha katika jedwali hapo juu. **Angalia kielelezo Y 1 na Y2.**

Hata hivyo ukaguzi uliweza kubaini kuandikwa kwa hati ya malipo Na. 1/10 ya mwaka 2009 kwa hundi Na.113868 ikionesha kuhamisha fedha Sh.

244,358,000 kutoka akaunti ya maendeleo kwenda akaunti ya Afya na kukatiwa stakabadhi Na. 0126665 ya terehe 15/10/2009, katika kufuatilia uhamishaji huo, timu ya ukaguzi ilibaini kutohamishwa kwa fedha hiyo kwani hundi Na. 113868 iliyoandikwa ilitumika kuhamisha fedha mnamo tarehe 4/2/2010 kwa fedha iliyoingia tarehe 2/2/2010 kiasi cha Sh. 244,358,000. **Angalia vielelezo Y 2 - Y 5**

Aidha, kwa kutokuhamisha fedha hizo toka akaunti ya Maendeleo kwenda Afya, Halmashauri haikuweza kutekeleza kikamilifu shughuli zenye jumla ya Sh. 244,358,000 katika Mpango kazi wa mwaka 2009/2010, hali hii imesababishwa na udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani na watumishi wa Uhasibu kutumia mbinu za hila na kutokuwa waaminifu katika mali na fedha za umma hivyo kumepelekea baadhi ya shughuli na miradi ya halmashauri kutotekelezwa kama ilivyokusudiwa. **Angalia kielelezo Y6**

**Mapendekezo**

- Menejimenti ya Halmashauri inatakiwa kuhakikisha mfumo wa udhibiti wa ndani unaboreshwa ili kuzuia uwezekano wa wizi wa fedha na kuhakikisha kuwa fedha zote zinarejeshwa kwenye mradi husika na miradi mingine ili zitekeleze shughuli zilizokusudiwa.
- Mweka Hazina Ndugu Muhidini Mohamed awajibike kwa kutosimamia kikamilifu uhamisho wa Fedha za Mradi.

### 2.7.2.2 Mradi wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM)

Katika kupitia stakabadhi za mapokezi na Taarifa za Benki (Bank Statements) za mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010 ilibainika kuwa, mnamo tarehe 10/09/2009.

Halmashauri ilipokea jumla ya Sh. 338,372,112 kupitia akaunti ya Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi wa Mpango wa Afya ya Msingi (MMAM) kama inavyooneshwa hapo chini:

| Tarehe zilipopokelewa Akaunti ya Maendeleo | Kiasi (Sh.) | Tarehe zilipohamishiwa akaunti ya Mradi | Kiasi (Sh.) | Kiasi ambacho hakikuhamishiwa akaunti ya mradi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| **A: Akaunti ya Maendeleo** | | | | |
| **2008/2009** | | | | |
| 21/2/2009 | 29,450,930 | - | - | 29,450,930 |
| 11/6/2009 | 35,873,087 | - | - | 35,873,087 |
| **Jumla ndogo** | **65,324,017** | | | **65,324,017** |
| **2009/2010** | | - | - | |
| 08/06/2010 | 2,155,000.00 | - | - | 2,155,000.00 |
| 26/02/2010 | 100,000,000.00 | - | - | 100,000,000.00 |
| 03/02/2010 | 20,000,000.00 | - | - | 20,000,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 06/11/2009 | 69,163,069.00 | - | - | 69,163,069.00 |
| 10/9/2009 | 81,730,026.00 | - | - | 81,730,026.00 |
| **Jumla ndogo** | **273,048,095** | - | - | **273,048,095** |
| **Jumla Kuu** | **338,372,112** | - | - | **338,372,112** |

#### 2.7.2.2.1 Fedha ambazo hazikuhamishiwa toka akaunti ya Maendeleo kwenda akaunti ya mradi wa MMAM Sh. 338,372,112

Ilibainika kuwa kiasi cha Sh.338,372,112 zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Afya ya Msingi mpaka wakati wa ukaguzi huu mwezi Juni 2011 takribani miezi 16-27 tangu kupokelewa katika akaunti ya Maendeleo hazijahamishiwa katika akaunti ya Afya ili zitumike kwa shughuli za mradi zilizokusudiwa kama inavyoonesha katika jedwali hapo juu. **Angalia kielelezo Z1- Z6**

Hata hivyo ukaguzi uliweza kubaini kuwa hati ya malipo Na. 6/10 ya 2009 kwa hundi Na. 113874 ikionesha kuhamisha fedha Sh. 81,730,026 kutoka akaunti ya maendeleo kwenda akaunti ya Afya zilizoombwa kwa barua yenye Kumb. Na. KDC/BS/2 VOL/34 tarehe 21/10/2009 na baadaye kukatiwa stakabadhi Na.0126666 ya terehe 26/10/2009 ili kuficha ukweli, katika kufuatilia uhamishaji huo, timu ya ukaguzi ilibaini kutohamishwa kwa fedha hizo kwani hundi hiyo haikuwasilishwa benki. **Angalia vielelezo Z 7- Z10**.

Kwa mujibu wa barua zenye kumbukumbu Na. KDC/BS/2 VOL/34 ya tarehe 21/10/2009, KDC/BS/2 VOL/35 ya tarehe 21/10/2009 na KDC/MMAM/AI/04 ya tarehe 25/05/2010 zilizoandikwa na Mganga Mkuu wa Wilaya Dr. Alex Kapula na Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya Dr. E Ngosso kwenda kwa Mkurugenzi wa Halmashauri zikiomba kuhamishwa kwa fedha za MMAM kutoka Akaunti ya Maendeleo kwenda ya Afya ili ziweze kutekeleza shughuli mbalimbali kulingana na Mpango Kazi. Lakini mpaka tarehe za ukaguzi huu maalum hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na Uongozi dhidi ya barua hizo. **Angalia Vielelezo Z11, Z12 na Z13.**

#### 2.7.2.2.2 Shughuli zilizoathirika na ubadhirifu wa fedha za Mradi

Katika kupitia taarifa za utekelezaji za Mwaka 2009/2010 ilibainika kuwa shughuli zenye jumla ya Sh.145,914,235 ziliathirika kutokana na ubadhirifu wa fedha za mradi hivyo kuifanya Halmashauri kushindwa kutekeleza shughuli zilizokusudiwa kama ilivyoainishwa katika mpango kazi, aidha Halmashauri ilishindwa kuwalipa wakandarasi waliopewa kazi za ujenzi na ukarabati wa Vituo na Zahanati kwani salio la fedha katika akunti ya Afya kulingana na taarifa za Benki kwa tarehe 30/6/2010 lilikuwa ni Sh.112,662 hivyo kuonesha fedha za MMAM katika akaunti wa Afya hazikuwepo. Zifuatazo ni fedha zilizokuwa hazijalipwa kwa wakandarasi Sh. 23,834,084 kulingana na mikataba na shughuli ambazo hazikutekelezwa kabisa Sh.122, 080,151 Kama zilivyooneshwa hapa chini:

| Lengo la Mradi | Jina la Mkandarsi | Namba ya Mkataba | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|
| Ujenzi wa nyumba ya mtumishi Zahanati ya Mwajidalala | M/S Mwifombo Investment Co. Ltd | LGA/108/2010/11/MMAM/ MWKD/11 | 3,834,084 |
| Ujenzi Idara ya wagonjwa wa nje (OPD) katika Zahanati ya Mhunze | M/S ZUBBEN CO. LTD, P.O BOX 2061 | LGA.108/KDC-OPD/DEV-FUND/2009/2010/C.01 | 20,000,000 |
| **Jumla ndodo** | | | **23,834,084** |
| **Miradi ambayo haikutekelezwa kabisa** | | | |
| Uezekaji wa jengo la Idara ya Wagonjwa wa nje (OPD) katika Hospitali ya Wilaya ya Kishapu | - | - | 423,820 |
| Ujenzi wa OPD katika Zahanati ya Idushi | - | - | 20,000,000 |
| Ujenzi wa OPD Mwigumbi H/C | - | - | 20,000,000 |
| Ujenzi wa OPD katika zahanati ya Bubiki H/C | - | - | 81,656,331 |
| **Jumla ndogo** | | | **122,080,151** |
| **Jumla Kuu** | | | **145,914,235** |

Hali hii imesababishwa na udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani na watumishi wa uhasibu kutumia mbinu za hila na kutokuwa waaminifu kwa mali na fedha za umma hivyo kumepelekea baadhi ya shughuli na miradi ya halmashauri kutotekelezwa kama ilivyokusudiwa. **Angalia kielelezo Z14**

**Comment [a11]:** Shilinde- weka Unimplemented activities

**Mapendekezo**
Menejimenti ya halmashauri inatakiwa kuhakikisha mfumo wa udhibiti wa ndani unaboreshwa ili kuzuia uwezekano wa wizi wa fedha na kuhakikisha kuwa fedha zote zinarejeshwa kwenye mradi husika na zitekeleze shughuli zilizokusudiwa.

### 2.7.2.2.3 Ukiukaji wa miongozo na taratibu za Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi -MMAM/JRF

Kulingana na mwongozo wa mfuko wa pamoja wa ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya uliotolewa na Ofisi ya Waziri mkuu Tawala za Mikoa na serikali za mitaa (OWM- TAMISEMI) rekebisho la Agosti 2006, sehemu ya pili kipengele cha 11 na 21 vya mwongozo huu unafafanua taratibu katika ngazi ya Halmashauri /ngazi za chini za Serikali za Mitaa kwamba Halmashauri itapeleka fedha iliyokasimiwa kwenda kwenye akaunti ya kituo iliyofunguliwa kwenye Halmashauri kama mgawo wa kwanza na taarifa itapelekwa kwa katibu wa kamati ya kituo ambaye ndiye

mganga mfawidhi wa kituo na baadaye kamati hiyo itaanza kazi za ukarabati mara baada ya kupokea fedha na kufanya mikutano ya usimamizi na kuandaa mihutasari (minutes). **Angalia kielelezo AA**

Halmashauri katika mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010 ilipokea jumla ya Sh.338,372,112 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa pamoja wa ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya (JRF) na Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM). Aidha, kinyume na mwongozo wa mfuko, Halmashauri haikupeleka fedha hizo katika akaunti za Kamati za Afya za Vituo na badala yake Halmashauri iliingia mikataba ya ukarabati wa Vituo vya Afya na Zahanati bila kuzishirikisha Kamati za Afya za Vituo. Sababu za kutopeleka fedha inatokana na Kutofuata miongozo na taratibu zilizopo hali ambayo inaweza kupelekea fedha hiyo kutumika isivyo kusudiwa na pia kuondoa uwajibikaji wa kamati za afya zilizoundwa na wananchi.

**Mapendekezo**

Halmashauri inatakiwa kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa katika matumizi ya fedha na kuhakikisha fedha zinatumwa katika zahanati.

### 2.7.2.2.4 Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi wa afya zahanati ya Bulima

Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu iliingia mkataba na M/s Batimba Engineering & Building Contractors Co. Ltd S.L.P 588, Shinyanga kwa mkataba namba LGA/108/2009/10/W/DEV23 kupitia fedha za mpango wa Afya ya Msingi (MMAM) kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mtumishi wa afya katika zahanati ya Bulima. Thamani ya mkataba ilikuwa ni shs. 17,000,210 na mkataba huu ulianza tarehe 28/07/2010 na ulitegemewa kumalizika 10/09/2010. **Angalia Kielelezo AB.**

Timu ya ukaguzi maalum ilipopitia kumbukumbu mbalimbali katika Halmshauri pamoja na kutembelea miradi iliyotekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 ilibaini mapungufu yafuatayo:

"Ceiling board", shimo la maji taka ambavyo ni muhimu katika nyumba ya makazi havikuoneshwa kwenye mkataba huu (BOQ) na mlango wa uani ulikuwa haujawekwa wenye gharama ya Sh.190, 000.

Mkataba huu ulivunjwa na Halmashauri kwa kuzingatia matakwa ya kipengele Na.28 na 29 cha Mkataba kwa sababu Mkandarasi hakuwepo kwa muda mrefu. Ilibainika kwamba mkandarasi alikuwa amekwishalipwa kiasi cha shilingi 13,391,886 kulingana na cheti cha malipo Na. 05 cha tarehe 27/12/2010 kilichoidhinishwa na Mhandisi wa Wilaya Eng. Leonard Mashamba pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri Mr. Theonas Nyamhanga. Hata hivyo wakati wa kuvunjwa kwa mkataba huo muda wa kuisha kwa mkataba ulikuwa umepita kwa miezi mitano (5). Mtiririko wa malipo kwa mkandarasi ni kama ifuatavyo:

| Namba ya Cheti cha malipo | Kiasi (Sh.) | Tarehe ya Cheti |
|---|---|---|
| Na. 01 | 3,410,060 | 03/06/2010 |
| Na. 02 | 2,079,000 | 20/08/2010 |
| Na. 03 | 2,348,650 | 30/09/2010 |
| Na. 04 | 2,554,176 | 20/10/2010 |
| Na. 05 | 3,000,000 | 27/12/2010 |
| **Jumla** | **13,391,886** | |

**Angalia Kielelezo AC1 - AC5.**



*Nyumba ya mtumishi katika zahanati ya Bulima - MMAM*

Sababu ya matatizo ni ukosefu wa umakini katika kuteua mkandarasi wa kufanya kazi hii na kutokuwa makini kwa watumishi wa Halmashauri, kitengo cha ujenzi, katika usimamizi wa kazi hivyo kupelekea Halmashauri kupata hasara kwa kumlipa mkandarasi kwa kazi ambayo iko chini ya kiwango tarajiwa na haijakamilika.

**Mapendakezo**

Halmashauri ihakikishe mradi huu unakamilika ili kutoa huduma tarajiwa kwa walengwa pia Halmashauri imchukulie hatua Mhandisi Bwana Leonard Mashamba kwa kusababisha hasara ya kumlipa mkandarasi kwa kazi ambayo haikufanyika ipasavyo.

### 2.7.2.3 Mradi wa Ukimwi (TACAIDS)

Katika kupitia stakabadhi za mapokezi na Taarifa za Benki ( Bank Statements) za mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010 ilibainika kuwa Halmashauri ilipokea jumla ya Sh.196,402,000 kupitia akaunti ya Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi wa Ukimwi kama inavyooneshwa hapa chini:

| Tarehe zilipopokelewa Akaunti ya Maendeleo | Kiasi (Sh.) | Tarehe zilipohamishiwa akaunti ya Mradi | Kiasi (Sh.) | Kiasi ambacho hakikuhamishiwa akaunti ya mradi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| **A: Akaunti ya Maendeleo** | | | | |
| **2008/2009** | | | | |
| 15/1/2009 | 39,559,000 | | | |
| **Jumla ndogo** | **39,559,000** | | | |
| **2009/2010** | | | | |
| 28/9/2009 | 32,194,000 | | | |
| 24/6/2010 | 24,649,000 | | | |
| | | 9/10/2009 | 5,000,000 | |
| | | 16/10/2009 | 33,200,000 | |
| | | 16/10/2009 | 5,000,000 | |
| **Jumla ndogo** | | | **43,200,000** | |
| **Jumla Kuu** | **96,402,000** | | **43,200,000** | **53,202,000** |
| **B. Global Fund** | | | | |
| **2009/2010** | | | | |
| 8/7/2009 | 100,000,000 | 8/7/2009 | 100,000,000 | |
| | | | | |
| **Jumla ndogo** | **100,000,000** | | | |
| **Jumla Kuu** | **196,402,000** | | **143,200,000** | **53,202,000** |

Katika kupitia nyaraka mbalimbali zikiwemo taarifa za Benki, Hundi zilizolipwa, vibutu vya Hundi, mipango kazi na taarifa za utekelezaji zinazohusu mapato na matumizi ya fedha za mradi wa Ukimwi (TACAIDS) ukaguzi iligundua kuwepo ubadhirifu wa jumla ya kiasi cha Sh.227,752,000 wa fedha za mradi uliofanywa na watumishi wa Halmashauri ambao wametajwa katika kila tukio la ubadhilifu kama ifuatavyo:

#### 2.7.2.3.1 Fedha ambazo hazikuhamishwa kwenda katika akaunti ya mradi Sh. 53,202,000

Ilibainika kuwa kiasi cha Sh. 53,202,000 zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Ukimwi kwa maana ya TACAIDS na Global Fund mpaka wakati wa ukaguzi huu mwezi June 2011 takribani miezi 12-24 tangu kupokelewa katika akaunti ya Maendeleo hazijahamishiwa katika ya Ukimwi ili zitumike kwa shughuli za mradi zilizokusudiwa kama inavyoonesha katika jedwali hapo juu. Hali hii imesababishwa Kutotekelezwa kwa shughuli na malengo yaliyokusudiwa hasa miradi ya maendeleo katika nyanja mbalimbali kunatokana na ukosefu wa fedha uliotokana na wizi na ubadhilifu. **Angalia kielelezo AD1 - AD5**

### 2 .7 .2.3.2 Malipo yasiyojulikana kwa walipwaji wasiojulikana Sh. 20,800,000

Katika kupitia daftari la fedha kwa mwaka 2009/2010 ilibainika jumla ya Sh. 20,800,000 zililipwa kutoka akaunti ya Ukimwi Na. 3071200102 ikiwa ni malipo yasiyojulikana kwa walipwaji wasiojulikana bila idhini ya Mkurugenzi wa Halmashauri ambayo yalihusisha malipo yaliyofanyika bila hati za malipo, kulipwa kwa hundi zilizofutwa lakini zikalipwa na Benki, malipo yalilipwa zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa katika hati za malipo na Malipo ya hundi zilizolipwa na benki wakati zikiwa zimesainiwa na watia sahihi ambao siyo walioidhinishwa.

### 2.7.2.3.3 Hundi zilizoghushiwa na kulipwa zaidi ikilinganishwa na vibutu Sh.87,050,000

Ukaguzi uliofanyika kwa kulinganisha rekodi za Halmashauri na zile za Benki, ulibaini kuwepo malipo nyenye mashaka Sh.87,050,000 yaliyotokana na kugushiwa hundi katika akaunti namba 30712000102. Malipo hayo ni kama ifuatavyo:

| Mlipwaji | Namba ya Hundi | Kiasi cha malipo kwenye vitabu vya malipo | Tarehe ilipolipwa benki | Kiasi cha malipo kwenye Hundi Sh |
|---|---|---|---|---|
| DED - Kishapu | 005688745 | 250,000 | 20/6/2009 | 16,250,000 |
| DED - Kishapu | 005688746 | 100,000 | 2/6/2009 | 10,000,000 |
| DED - Kishapu | 005688747 | 110,000 | 14/6/2009 | 11,000,000 |
| DED - Kishapu | 005688749 | 200,000 | 12/6/2009 | 5,200,000 |
| DED - Kishapu | 112851 | 250,000 | 12/6/2009 | 4,200,000 |
| DED - Kishapu | 005688748 | 400,000 | 3/4/2009 | 40,400,000 |
| **Jumla ndogo** | | | | **87,050,000** |

Aidha**,** katika kupitia taarifa za utekelezaji za mwaka 2009/2010 ilibainika kuwa shughuli za Global Fund na Ukimwi(TACAIDS) zenye jumla ya Sh. 87,050,000 ziliathirika kutokana na ubadhirifu wa fedha za mradi hivyo Halmashauri kushindwa kutekeleza shughuli kama ilivyokusudiwa. **Angalia vielelezo TACAIDS - R5 - R11.**

### 2.7.2.3.4 Uhamishaji wa fedha bila idhini Sh.66,700,000

Formatted: Font: 12 pt

Katika kupitia daftari la fedha 2009/2010 ilibainika jumla ya Sh. 66,700,000 zilihamishwa kutoka akaunti ya Ukimwi Na. 3071200102 kwenda katika akaunti mbalimbali bila idhini ya Mkurugenzi wa Halmashauri kama inavyooneshwa hapo chini:

| Tarehe | Nambari ya hati | Namba ya Hundi | Akaunti zilikohamishiwa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 15/03/2010 | GLP02966 | 112881 | Haikutajwa | 9,300,000.00 |
| 09/07/2009 | GLP02368 | Bank Slip | Haikutajwa | 6,000,000.00 |
| 15/07/2009 | GLP02372 | 5688748 | Maendeleo | 40,400,000.00 |
| 09/07/2009 | GLP02371 | 5688747 | Amana | 11,000,000.00 |
| **Jumla** | | | | **66,700,000** |

Formatted: Font: 12 pt

Formatted: Font: 12 pt

**Rejea kielelezo T17**

### 2.7.2.3.5 Shughuli zilizoathirika na ubadhirifu wa fedha za Mradi Sh. 57,454,000

Katika kupitia taarifa za utekelezaji za Mwaka 2009/2010 ilibainika kuwa shughuli za miradi zenye jumla ya Sh.57,454,000 hazikutekelezwa kutokana na ubadhirifu wa fedha za mradi uliobainishwa katika aya zilizotangulia. Aidha, kwa Halmashauri kushindwa kutekeleza shughuli zilizokusudiwa kama zilivyoainishwa katika mpango kazi kama ifuatavyo:

| | **A: GLOBAL FUND** | |
|---|---|---|
| **Na.** | **Lengo la Mradi** | **Kiasi (Sh)** |
| 1. | Kukarabati chumba cha madawa cha wilaya | 3,850,000 |
| 2. | kufanya mafunzo ya kudhibiti wa STI | 22,610,000 |
| 3. | Kufanya usimamizi na matengenezo ya magari | 6,360,000 |
| 4. | Usimamizi wa mradi | 3,811,500 |
| 5. | Ununuzi wa madawa - OI's | 5,068,000 |
| 6. | Ununuzi wa pikipiki | 7,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | **48,699,500** |
| **B: UKIMWI (TACAIDS)** | | |
| 1. | Kutoa mafunzo kwa watumishi wa Wilaya kuhusu elimu ya Ukimwi | 20,275,000 |
| 2. | Kufanya utambuzi wa WAVVU miongoni mwa waajiriwa ifikapo Juni 2010 | 2,250,000 |
| 3. | Kutoa elimu ya Afya kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi. | 5,820,000 |
| 4 | Kuelimisha makundi yaliyo katika mazingira hatarishi matumizi sahihi ya kondom. | 1,780,000 |
| 5 | Kuelimisha watu 200 wanaoishi na virusi vya Ukimwi kuhusu uambukizaji wa makusudi kufikia Juni 2010. | 8,200,000 |
| 6 | Kuhamasisha jamii katika kata 20 kuhusu uambukizaji wa makusudi hadi kufikia Juni 2010. | 2,650,000 |
| 7 | Kuwatambua na kuwasajili yatima 200. | 1,224,500 |
| 8 | Kuwasaidia watu waishio na virusi vya Ukimwi kujiunga na VIKOBA. | 6,239,500 |
| 9 | Kuwatambua wajane na watoto/watu waishio mazingira hatarishi/waishio na virusi vya ukimwi pamoja na mahitaji yao. | 915,000 |
| 10. | Kufanya warsha ya kubadilishana uzoefu kuhusu vyanzo vya mapato uli kusaidia makundi ya WAVVU, wajane na watoto walio katika | 3,800,000 |

| | | |
|---|---|---|
| | mazingira hatarishi | |
| 11. | Kutambua makundi yaliyo katika mazingira hatarishi kwa HTA ifikapo 2010. | 500,000 |
| 12. | Kutoa mafunzo kwa wanaume/wanawake kuhusu mwenendo wa mabadiliko ya tabia. | 3, 800,000 |
| | **Jumla** | **57,454,000** |

Katika kupitia nyaraka mbalimbali ikiwemo mpango kazi na taarifa ya utekelezaji ilibainika kwamba, shughuli zilizokusudiwa zenye thamani ya Sh.32,194,000 hazikuweza kutekelezwa**.** Aidha, katika mahojiano yaliyofanyika yakiwahusisha Bw. David Kijo (Afisa maendeleo ya jamii II) na Bw. Edwini Nzela (Mratibu wa Ukimwi wa Wilaya) ilisemekana kwamba, kiasi hicho cha fedha hakikuhamishwa kutoka katika akaunti ya maendeleo kwenda katika akaunti ya Ukimwi kama taratibu zinavyotaka. **Angalia kielelezo AD3 na AD7**

**Mapendekezo**

Bwana Muhidini Mohamed aliyekuwa Mweka Hazina anawajibika kwa kutohamishwa fedha jumla ya Sh.53,202,000 katika akaunti ya mradi husika.

#### 2.7.2.4 Mfuko wa Elizabeth Glacier Paediatric Aids Fund (EGPAF)

Katika kupitia stakabadhi za mapokezi na taarifa za Benki (Bank Statements) za mwaka wa fedha 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010 ilibainika kuwa Halmashauri ilipokea jumla ya Sh. 612,621,267 kupitia akaunti ya Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za EGPAF kama inavyooneshwa hapo chini:

| **2007/2008** | | |
|---|---|---|
| **Tarehe** | **Maelezo** | **Kiasi (Shs)** |
| 17/1/2007 | Elizabeth Glaser | 50,348,049 |
| 27/2/2008 | Elizabeth Glaser | 12,874,000 |
| 19/6/2008 | Elizabeth Glaser | 55,325,514 |
| **Jumla ndogo** | | **118,547,563** |
| **2008/2009** | | |
| 6/8/2008 | Elizabeth Glaser | 62,308,269 |
| 8/10/2008 | Elizabeth Glaser | 49,392,777 |
| 17/10/2008 | Elizabeth Glaser | 19,045,328 |
| 31/10/2008 | Elizabeth Glaser | 24,222,250 |
| 10/12/2008 | Elizabeth Glaser | 38,682,501 |
| 27/01/2009 | Elizabeth Glaser | 38,517,468 |
| 27/01/2009 | Elizabeth Glaser | 21,456,039 |
| 27/01/2009 | Elizabeth Glaser | 6,582,521 |
| 13/03/2009 | Elizabeth Glaser | 12,857,575 |
| 07/05/2009 | Elizabeth Glaser | 21,753,137 |
| 3/06/2009 | Elizabeth Glaser | 55,683,215 |

| | | |
|---|---|---|
| 3/06/2009 | Elizabeth Glaser | 1,272,240 |
| 30/6/2009 | Elizabeth Glaser | 1,261,654 |
| **Jumla ndogo** | | **353,034,974** |
| | | **2009/2010** |
| 02/07/2009 | Elizabeth Glaser | 14,142,181 |
| 22/07/2009 | Elizabeth Glaser | 8,621,296 |
| 28/08/2009 | Elizabeth Glaser | 21,274,026 |
| 29/09/2009 | Elizabeth Glaser | 33,099,420 |
| 05/11/2009 | Elizabeth Glaser | 17,236,361 |
| 19/02/2010 | Elizabeth Glaser | 3,495,350 |
| 03/02/2010 | Elizabeth Glaser | 4,171,720 |
| 03/05/2010 | Elizabeth Glaser | 6,615,366 |
| 31/05/2010 | Elizabeth Glaser | 9,847,860 |
| 07/06/2010 | Elizabeth Glaser | 14,897,100 |
| 22/06/2010 | Elizabeth Glaser | 7,638,050 |
| **Jumla ndogo** | | **141,038,730** |
| **Jumla Kuu** | | **612,621,267** |
| | | |

Katika kupitia nyaraka mbalimbali zikiwemo taarifa za Benki, Hundi zilizolipwa, vibutu vya Hundi, mipango kazi na taarifa za utekelezaji zinazohusu mapato na matumizi ya fedha za mradi wa EGPAF ukaguzi uligundua kuwepo ubadhirifu wa jumla ya kiasi cha Sh.81,628,000 wa fedha za mradi uliofanywa na watumishi wa Halmashauri ambao wametajwa katika kila tukio la ubadhilifu kama ifuatavyo:

#### 2.7.2.4.1 Uhamishaji wa fedha bila idhini Sh.53,000,000

Katika kupitia daftari la fedha 2009/2010 ilibainika jumla ya Sh.53,000,000 zilihamishwa kutoka akaunti ya EGPAF Na. 3071200119 kwenda katika akaunti mbalimbali bila idhini ya Mkurugenzi wa Halmashauri kama inavyooneshwa hapa chini:

| Tarehe | Nambari ya hati | Namba ya Hundi | Akaunti zilikohamishiwa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 28/10/2009 | GLP01778 | 184951 | Afya | 10,000,000 |
| 02/12/2009 | GLP01779 | 184953 | Mfuko wa Barabara | 20,000,000 |
| 02/12/2009 | GLP01780 | 184952 | haikutajwa | 5,000,000 |
| 01/07/2009 | GLP01353 | | Afya | 3,000,000 |
| 21/10/2009 | GLP00789 | 112147 | Maendeleo II | 15,000,000 |
| **Jumla** | | | | **53,000,000** |

#### 2.7.2.4.2 Hundi zilizoghushiwa na kulipwa zaidi ikilinganishwa na vibutu Sh.28,628,000

Ukaguzi uliofanyika kwa kulinganisha rekodi za Halmashauri na zile za Benki, ulibaini kuwepo malipo yenye mashaka yaliyotokana na uwezekano wa kugushi hundi katika akauti namba 30712000119 - EGPAF . Malipo hayo ni kama ifuatavyo:

| Na. | Mlipwaji | Namba ya Hundi | Tarehe iliyolipwa Benki | Maelezo ya hundi | Kiasi kwenye Hundi Sh |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KDC | 112066 | 29/4/2009 | ilifutwa | 28,628,000 |
| | **Jumla** | | | | **28,628,000** |

Hundi Na.112066 inaoneshwa kwenye vitabu vya malipo (Cash book) na vibutu kuwa ilifutwa (Cancelled) lakini katika taarifa za benki (Bank statement) inaoneshwa zililipwa tarehe 29/04/2009.

Watuhumiwa wa hujuma zilizoainishwa hapo juu ni Bw. Walugu Mussa ambaye ni Mtunza Fedha, Bw. Muhidini Mohamed ambaye ni Mweka Hazina na Watumishi/Mtumishi wa NMB Tawi la Manoga Shinyanga ambao wametajwa katika barua yenye Kumb.Na. KDC/C.A/30/3/32 ya tarehe 3/9/2010 iliyoandikwa na Mkurugenzi wa Halmashauri kwenda kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga. Kutokuwepo kwa mfumo thabiti wa udhibiti wa ndani hivyo kumepelekea mfuko wa EGPAF kushindwa kutoa huduma zilizokusudiwa. . **Angalia Kielelezo.Q2**

**Mapendekezo**

- Halmashauri inatakiwa kurudisha fedha za mfuko wa EGPAF zilizotumika kinyume na taratibu ili ziweze kutumika katika malengo yaliyokusudiwa.
- Menejimenti ya Halmashauri ihakikishe kuwa waliohusika wanachukuliwa hatua na fedha hizo zirudishwe katika akaunti husika.
- Menejimenti ya halmashauri inatakiwa kuhakikisha mfumo wa udhibiti wa ndani unaboreshwa ili kuzuia uwezekano wa wizi wa fedha zake.

#### 2.7.2.5 Utunzaji wa Hesabu zinazohusiana na mapato ya mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu Mfuko wa Afya ya Jamii ulianza mwaka 2008 kwa sheria ndogo Na. GN 257 ya tarehe 31/10/2008, hata hivyo michango ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ilianza kupokelewa toka kwa wanachama iliyorithi toka Halmashauri ya Shinyanga Vijijini na kupata mgawo Sh. 27,000,000 ikiwa ni ada tokea mwaka 2003.

Katika kuendesha mpango huu, Wilaya ilipitisha kuwa kila mwanachama (kaya) achangie shilingi 5,000 kwa ajili ya kuhudumia familia nzima yaani Baba, Mama na watoto 6 chini ya miaka 18. Michango ya papo kwa papo ni

Sh.1,000 kwa Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali. Malipo haya ni kwa wagonjwa wasio wanachama na huwekwa kwenye Akaunti Na.2071200091 iliyoko NMB- Manonga ambayo inatunzwa na kuangaliwa na Bodi ya Afya ya Halmashauri.

Hadi kufikia tarehe 30/6/2010 michango iliyokusanywa kuanzia tarehe 01/7/2007 kulingana na taarifa za Benki ni Sh.132,987,185 kama inavyooneshwa hapo chini:

| Tarehe | Maelezo | Kiasi (Sh) |
|---|---|---:|
| 01/7/2007 | Salio anzia | 4,759,528 |
| 03/1/2007 - 19/9/2009 | Michango ya wanachama | 115,884,940 |
| 3/10/2009 - 30/12/2009 | Michango ya wanachama | 7,202,755.00 |
| 7/1/2010 – 17/6/2010 | Michango ya wanachama | 5,139,962 |
| **Jumla** | | **132,987,185** |

Hata hivyo kwa mujibu wa barua yenye Kumb. Na. KDC/CHF/VOL.1/1/39 ya tarehe 15/3 /2008 inaonesha Halmashauri ilipata mgawo wa kiasi cha Sh. 27,000,000 toka Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, ukaguzi ulipofuatilia mapokezi ya fedha hizi haikuweza kufahamika zilipokelewa katika akaunti ipi ya Halmashauri kwani katika taarifa za Benki akaunti ya CHF hazikuonekana. **Angalia kielelezo AD8**

Katika kupitia nyaraka mbalimbali zikiwemo taarifa za Benki, Hundi zilizolipwa, vibutu vya hundi, mipango kazi na taarifa za utekelezaji zinazohusu mapato na matumizi ya fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ukaguzi uligundua kuwepo ubadhirifu wa jumla wa kiasi cha Sh.107,539,500 wa fedha za mradi uliofanywa na watumishi wa Halmashauri ambao wametajwa katika kila tukio la ubadhirifu ambao ni Mweka Hazina Bwana Muhidini Mohamed, Mtunza Fedha Bwana Mussa Limbe na Watumishi wa Benki NMB Manonga ambao pia wamatajwa katika barua yenye Kumb. Na. KDC/CA/30/3/32 ya tarehe 3/9/2010.**Angalia kielelezo H1**

### 2. 2.7.2.6 Matumizi ya Fedha ya Mfuko yasiyoidhinishwa na kwa malengo yasiyokusudiwa Sh.126,806,000

Kinyume na Kanuni za mfuko wa Afya ya jamii, matumizi yenye jumla ya Sh.126,806,000 yalifanyika kulipia matumizi mbalimbali yasiyolenga malengo ya Mfuko wa Afya ya Jamii kinyume na Kifungu Na. 5 cha Sheria ndogo ya Mfuko wa Afya ya Jamii kinachosisitiza matumizi yafanyike katika kutoa huduma bora ya Afya ya jamii kwa wanachama na kuboresha huduma za Afya kwa jamii kwa kugawa madaraka na kuiwezesha jamii kutoa maamuzi katika mambo yanayoathiri afya ya jamii.

Malipo ambayo yalifanyika bila idhini na kwa malengo yasiyokusudiwa ni kama yafuatayo:

| Tarehe | Namba ya Hundi. | Kiasi (Shs) |
|---|---|---|
| 16/10/2007 | 108651 | 13,626,000 |
| 13/12/2007 | 108665 | 16,626,000 |
| 27/02/2008 | 108656 | 750,000 |
| 03/03/2008 | 108552 | 13,626,000 |
| 12/03/2008 | 108558 | 19,257,500 |
| 31/5/2008 | 108659 | 10,150,000 |
| **Jumla ndogo** | | **74,035,500** |
| **2008/2009** | | |
| 09/7/2008 | 108657 | 19,257,500 |
| 11/10/2008 | 108660 | 420,000 |
| 02/04/2009 | 108662 | 14,620,000 |
| **Jumla ndogo** | | **34,297,500** |
| **2009/2010** | | |
| 29/06/2009 | 108663 | 6,118,000 |
| 9/11/2009 | 108664 | 358,000 |
| 02/12/2009 | 108666 | 12,000,000 |
| **Jumla ndogo** | | **18,476,000** |
| **Jumla Kuu** | | **126,809,000** |

**Angalia kielelezo.AD9**, **AD10 na AD11**

Kifungu cha 8 (3) cha kanuni ndogo cha Mfuko wa Afya ya Jamii kinaeleza kuwa waweka sahihi watakaoruhusiwa kuwa watia saini katika akaunti ya Mfuko ili kuidhinisha malipo watateuliwa na Bodi ya Afya ambao ni Mwenyekiti wa Bodi na Mwanachama mmoja wa Bodi wanatakiwa kuwa Kundi '**A**' na Katibu wa Bodi ambaye ni Mganga Mkuu wa Wilaya pamoja na Mweka Hazina wanatakiwa kuwa Kundi **'B'.** Kinyume na kifungu namba 8 kifungu kidogo namba 3 na 4 cha sheria ndogo za mwaka 2008 ambapo Halmashauri imewaweka watia saini wa kundi '**A**' ambao ni Mkurugenzi wa Halmashauri na Mtumishi wa Afya badala ya Mwenyekiti wa Bodi na mjumbe mmoja aliyeteuliwa na Bodi.

Pia ukaguzi maalum ulishindwa kupata kumbukumbu mbalimbali za Mfuko wa Afya ya Jamii kama vile mihtasari ya vikao vya Bodi ya Afya, Taarifa za mapato na matumizi, hati za malipo na daftari la mapato na matumizi la mwaka 2008/2009. Ubadhirifu wa Fedha za mfuko huu umeainishwa katika aya ya 2.6 ya taarifa hii.

Mapungufu haya yametokana na udhaifu wa usimamizi wa mfuko huu hivyo kupelekea Mfuko wa Afya ya Jamii kushindwa kutoa huduma bora za Afya kwa wanachama hivyo kuwavunja moyo na ari ya kuchangia huduma hiyo na

shughuli za tiba na kinga kwa wanachama zilizokusudiwa zinakwama kuendelea kutokana fedha hizo kutotumika kwa shughuli iliyokusudiwa.

**Mapendekezo**

- Halmashauri inatakiwa kurudisha fedha za mfuko wa Afya zilizotumika kinyume na taratibu ili ziweze kutumika katika malengo yaliyokusudiwa.
- Mamlaka husika iwachukulie hatua stahiki; Mweka Hazina Ndugu Muhidini Mohamed na Bwana Mussa Limbe ambaye ni Mtunza Fedha na fedha hizo zirudishwe katika akaunti hiyo.
- Menejimenti ya halmashauri inatakiwa kuhakikisha mfumo wa udhibiti wa ndani unaboreshwa ili kuzuia uwezekano wa wizi wa fedha zake.
- Halmashauri inatakiwa kuhakikisha uendeshaji wa Mfuko unafuata taratibu zilizoainishwa katika Sheria ndogo na kuhakikisha kuwa mapungufu yote yaliyojitokeza yanarekebishwa na kuhakikishwa kuwa watia saini katika akaunti ya Mfuko wanawekwa wale walioainishwa katika Sheria ya Mfuko huo.
- Mfuko wa Afya ya Jamii kwa kushirikiana na Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu unatakiwa kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizopo ili kufanikisha malengo ya kuanzishwa kwa Mfuko.

## 2.8 Miradi ya Maendeleo (LGCDG)

### 2.8.1. Kutokamilika kwa miradi ya ujezi wa Maabara 21.

Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Halmashauri ya wilaya ya Kishapu ilipeleka Sh. 260,803,765 katika kata ishirini (20) kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa Maabara 21 za shule za Sekondari. Maabara hizo zilipangwa kujengwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilihusu ujenzi wa msingi na sehemu ya ukuta kabla ya lenta. Hii ilikwishakamilika katika maabara nyingi. Orodha ya shule za Sekondari zilizopelekewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Maabara ni kama inavyooneshwa katika **kiambatanisho "J".**

Katika awamu ya pili ya ujenzi wa Maabara, Halmashauri ilingia mikataba na wakandarasi kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ambayo ilijumuisha ujenzi wa ukuta tokea madirishani, lenta, uezekaji wa mabati, uwekaji wa milango na madirisha, sakafu na kupaka rangi ndani na nje. Kati ya maabara hizo 21, Maabara 12 zilitembelewa na timu ya ukaguzi maalum. Kati ya hizo 12, maabara 11 zilikuwa bado hazijakamilika. Maabara moja katika Shule ya Sekondari Mipa, ndiyo ambayo ujenzi wake ulikuwa unaridhisha kulingana na mkataba, kama inavyoonekana katika picha hapa chini:



*Jengo la Maabara shule ya Sekondari Mipa, kama inavyoonekana nje*

**Mapungufu ya jumla yaliyobainika katika ujenzi wa maabara ni kama yafuatayo:**

- Mikataba na orodha ya vifaa haikueleza wazi ni hatua gani awamu ya kwanza iliishia na mkandarasi alitakiwa kuanzia hatua gani kwa kila maabara, hivyo ilikuwa vigumu kwa ukaguzi kujiridhisha na thamani ya kazi iliyotolewa kwa mkandarasi.
- Mikataba yote haikuwa na tarehe iliyowazi ya lini mkandarasi anatakiwa kuanza, kazi na tarehe ya kukamilisha kazi isipokuwa ilionesha siku za muda wa kazi kukamilika kinyume na Kanuni Na. 105 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (GN 97) za 2005.
- Wakandarasi wote walikuwa nyuma ya muda wa kukamilisha kazi kwa mujibu wa mikataba zaidi ya miezi 19 na kazi nyingi bado hazijakamilika pamoja na muda wa mikataba kuwa umekwisha. Hakuna hatua zozote za adhabu ya ucheleweshaji zilizochukuliwa na Halmashauri kwa mujibu wa mkataba kinyume na Kanuni Na. 119 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2005.
- Wakati wa kutembelea miradi ilibainika kuwa Wakandarasi wote hawakuwepo maeneo yao ya ujenzi kwa muda usiojulikana, pamoja na kuwa kazi zilikuwa hazijakamilika.
- Pia ilibainika kuwa Halmashauri haikufanya usimamizi madhubuti wa miradi hiyo, kwa vile Mhandisi na wasaidizi wake hawakuweza kutoa maelezo fasaha walipohojiwa na timu ya Ukaguzi.

- Mchakato wa uteuzi wa baadhi ya wakandarasi pia haukuzingatia uwezo wa utendaji kazi walionao, kwa vile katika baadhi ya miradi kazi zilizofanywa na wakandarasi zimeonekana kuwa chini ya viwango vya ubora.

- Kutokuwepo ushirikishwaji thabiti wa wadau au walengwa wa miradi katika kila kazi inayofanyika, hata kama kazi hiyo inafanywa na mkandarasi kwa fedha inayotoka moja kwa moja Halmashauri kwani Wakuu wa Shule walielezea kutoshirikishwa katika mchakato mzima wa usimamizi wa ujenzi wa maabara hizo.

Miradi iliyotembelewa na timu ya ukaguzi na matokeo ya ukaguzi wa kazi zilizofanyika katika awamu ya pili ni kama ifuatavyo:

#### 2.8.1.1 Ujenzi wa vyumba vitatu vya maabara katika shule ya sekondari Igaga

Timu ya ukaguzi ilipotembelea eneo la mradi mnamo tarehe 23/06/2011 ilibaini mapungufu haya; Mkataba wa mradi huu haukuweza kupatikana, milango pamoja na fremu zake hazikuwekwa, Sakafu ya maabara haikujengwa, Jengo halijapigwa ripu na jengo hilo la maabara halijapakwa rangi.

Hadi wakati wa ukaguzi maalum ilionesha wazi kuwa mkandarasi alikuwa tayari ameshaondoka eneo la mradi na hakuna kazi yoyote iliyokuwa ikiendelea na hakukuwa na taarifa yoyote inayohusu maendeleo ya mradi kama inavyoonekana hapa chini:



#### 2.8.1.2 Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya maabara shule ya sekondari Mwamalasa

Mnamo tarehe 10/11/2009 Halmashauri ya Wilaya Kishapu iliingia makataba na M/s Yayeli-1922 Investment Co Ltd wa S.LP 2265, Shinyanga kwa mkataba

namba LGA/108/2009/10/W/DEV/C.02 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vitatu vya maabara katika shule ya Sekondari Mwamalasa na ukamilishaji nyumba ya mtumishi shule ya sekondari Somagedi. Thamani ya mkataba ilikuwa ni Sh. 62,753,665 na mkataba huu ulianza tarehe 17/11/2009 na ulitegemewa kumalizika 17/01/2010.

**Mapungufu yaliyojitokeza**

Timu ya ukaguzi maalum ilitembelea mradi huu mnamo tarehe 24/06/2011, pamoja na kufanya mahojiano na Mwalimu Emmanuel Dominic, ilibainika kuwa Milango haikuwa imewekwa ikiwa na thamani ya Sh. 330,000, plasta ya nje haikupigwa ikiwa na thamani ya Sh. 1,247,500 na zege ya kibaraza haikuwa imewekwa.

Hadi kipindi hiki cha ukaguzi huu maalum miezi 17 ilishapita tangu kukamilika kwa muda wa Mkataba na hakukuwa na barua yoyote ya maombi ya kuongezewa muda, wala tozo kwa mkandarasi kwa kuchelewa kumaliza kazi kinyume na Kanuni Na. 119 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (GN 97) za 2005.

Katika kupitia faili la Mkandarasi ilibainika kuwa mkandarasi alikwisha mwandikia barua Mkurugenzi wa Halmashauri ili kumkabidhi jengo hilo la maabara, kwa madai kwamba tayari lilikuwa limemalizika na lipo tayari kwa matumizi yaliyokusudiwa. Barua hiyo yenye kumbukumbu Na. YIL-1922/WRK/2009/10/03 ya tarehe 9/04/2010 ilipitishwa na Mkurugenzi na cheti cha malipo cha tarehe 21/10/2010, yenye jumla ya Sh. 8,138,600 kililipwa kwa mkandarasi. **Angalia vielelezo AJ1 - AJ 6**.

Picha za Maabara ya shule ya Sekonadari Mwamalasa ni kama zinavyoonekana hapa chini:



*Jengo la maabara shule ya sekondari Mwamalasa*

**Malipo kwa mkandarasi**

Mkandarasi huyu kwa ujumla alilipwa kiasi cha shilingi 21,858,600 kati ya kiasi kilicho katika mkataba Sh. 62,753,665, kama inavyooneshwa hapa chini:

| Namba ya Cheti cha malipo | Kiasi (Sh.) | Tarehe ya Cheti |
|---|---:|---|
| Na. 01 | 13,720,000 | 15/02/2010 |
| Na. 02 | 8,138,600 | 21/10/2010 |
| **Jumla** | **21,858,600** | |

### 2.8.1.3 Ujenzi wa vyumba vitatu vya maabara katika shule ya sekondari Ukenyenge

Mnamo tarehe 10/11/2009 Halmashauri ya wilaya Kishapu iliingia makataba na M/s Mussa Romore wa S.LP 13, Kishapu kwa mkataba namba LGA/108/2009/10/W/DEV/C.06 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vitatu vya maabara, nyumba ya mtumishi na darasa moja katika shule ya sekondari Ukenyenge. Thamani ya awali mkataba ilikuwa ni Sh.51, 777,180 na ongezeko la Sh.7, 218,240. Mkataba huu ulianza tarehe 17/11/2009 na ulitegemewa kumalizika 17/01/2010. Mkataba huu ulikuwa ni mwendelezo wa ujenzi wa maabara katika awamu ya pili baada ya awamu ya kwanza kuishia hatua ya ukuta. **Angalia Kielelezo AJ 7 - AJ15**

**Mapungufu yaliyojitokeza**

Timu ya ukaguzi maalum ilitembelea mradi huu mnamo tarehe 23/06/2011 na mapungufu yafuatayo yalibainika:

i. Kutoainishwa kwa mwisho wa kazi za awamu ya kwanza na mwanzo wa kazi za awamu ya pili.

ii. Kuchelewa kukamilika kwa kazi ndani ya siku zilizokubalika katika mkataba. Hadi tarehe ya ukaguzi huu maalum kazi ilikuwa imechelewa kwa miezi 17, ingawa Mkandarasi aliomba kuongezewa muda wa kazi kwa siku 90 kwa barua isiyo na kumbukumbu namba ya tarehe 22/01/2010. Kazi zifuatazo zilikuwa bado hazijafanyika mpaka tarehe ya ukaguzi huu (Juni 2011):

- Fremu za madirisha zimewekwa 19 kati 21 na pia fremu 3 ambazo hazijawekwa zimeanza kuliwa na mchwa baada ya kuachwa kwa muda mrefu kama inavyoonekana katika picha hapo chini. Shata za madirisha zenye thamani ya Sh. 2,730,000 pia hazipo.
- Sakafu ya ndani na plasta haijawekwa yenye thamani ya Sh. 1,497,510 na milango yenye thamani ya Sh. 300,000 haijawekwa. **Angalia Kielelezo AJ 7.**
- Kazi yenye thamani ya Sh.9,886,910 kama ilivyooneshwa kwenye BOQ ilikuwa haijafanyika hadi kufikia kipindi cha ukaguzi maalum.

Ilibainika kwamba mkandarasi alikuwa tayari ameshaondoka katika eneo la mradi na hakuna dalili za kuendelea kwa kazi hiyo na kuacha kazi haijakamilika kama zinavyoonekana hapa chini:



*Vyumba vitatu vya maabara katika shule ya sekondari Ukenyenge*

**Malipo kwa mkandarasi**

Mkandarasi huyu alilipwa jumla ya kiasi cha shilingi **56,914,350** kati ya kiasi kilicho katika mkataba Sh. 58,995,420 ( Sh.51,777,180 + Sh.7,218,240) kama inavyooneshwa hapa chini:

| Namba ya Cheti cha malipo | Kiasi (Sh.) | Tarehe ya Cheti |
|---|---:|---|
| Na. 01 | 5,648,430 | 10/12/2009 |
| Na. 02 | 6,997,500 | 05/03/2010 |
| Na – 03 | 10,679,000 | 27/04/2010 |
| Na – 04 | 10,244,800 | 07/06/2010 |
| Na – 05 | 7,563,580 | 05/07/2010 |
| Na – 06 | 5,536,240 | 02/08/2010 |
| Cheti cha mwisho | 10,244,800 | 07/06/2010 |
| **Jumla** | **56,914,350** | |

**Angalia Kielelezo AJ 8 - AJ14**

#### 2.8.1.4 Ukamilishaji wa nyumba mbili za watumishi katika shule ya sekondari Ukenyenge

Mkandarasi aliandikiwa cheti cha malipo na Mhandisi wa Halmashauri Eng. L.B.L. Mashamba baada ya ukaguzi wa kazi kuonekana unakidhi viwango, mwezi Agosti, 2010, lakini baadae mwezi Septemba, 2010 Mkuu wa shule ya Sekondari Ukenyenge alilalamikia mapungufu yaliyojitokeza kwenye ujenzi wa nyumba ya mtumishi kwa barua yenye Kumb.Na.UKSESCO/S.2282/16/49 ya tarehe 28/9/2010. Hii inaonesha cheti kiliandikwa bila kufanya ukaguzi wa kina na mkandarasi hakuwa akisimamiwa ipasavyo. **Angalia Kielelezo AJ16.**

Kulikuwa na ongezeko la kazi lisilo la kawaida la Sh.7, 218,240 sawa na 71.5% ya thamani ya mkataba wa awali uliokuwa na thamani ya Sh.10, 100,190. Vitu vya muhimu vilivyosahaulika katika mkataba wa awali na kusababisha ongezeko la kazi ni uwekaji wa dari, rangi, shata, vioo na frame za madirisa; ingawa mkataba wa kwanza pia ulikuwa na madirisha yenye nyavu za mbu. **Angalia Kielelezo AJ17 - AJ20.**

**Mapungufu yaliyojitokeza:**
Timu ya ukaguzi maalum ilipotembelea katika mradi huu ilibainika kuwa mkandarasi hakufanya kazi kama zilivyoainishwa katika BOQ:

(i) Vitasa vilivyotumika havikuwa vile vilivyopendekezwa katika BOQ yaani Vitasa vilivyowekwa ni "Canon" badala ya "Union". Vitasa vya "Canon" havina ubora unaolingana na "Union".

(ii) Kazi yenye thamani ya Sh. 700,000 ambayo ilikuwa ni kwa ajili ya ujenzi wa shimo la choo haikuanishwa katika BOQ.

(iii) Kazi kuchelewa kumalizika kwa miezi 17 mpaka wakati wa ukaguzi (Juni, 2011) wa miradi hii na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na Uongozi wa Halmashauri dhidi ya Mkandarasi kinyume na Kanuni Na. 119 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (GN 97) za 2005.

(iv) Baadhi ya Vioo vimevunjika, nyavu za mbu hazipo, baadhi ya fremu za milango zimepinda pia milango haifungiki na sehemu ya vyumba vya uani na vyoo havijamalizika.

Picha ya nyumba moja kati ya mbili za watumishi katika shule ya sekondari Ukenyenge ni kama zinavyoonekana hapa chini:



**2.8.1.5 Ukamilishaji wa jengo la darasa katika shule ya sekondari Ukenyenge**

Timu ya ukaguzi maalum ilipotembelea katika mradi huu ilibainika kuwa mkandarasi alitakiwa kufanya kazi kama zilivyoainishwa katika BOQ kwa kila nyumba. **Angalia Kielelezo AJ 21, AJ 22 na AJ23**

Mapungufu yaliyojitokeza ni sakafu haina ubora ina nyufa nyingi na mlango mmoja umeharibika kama inavyoonekana katika picha hapa chini. Pia jengo hilo la darasa halitumiki hadi ukaguzi huu maalum ulipokuwa unafanyika:



*Mlango katika shule ya sekondari ukenyenge ulitengezwa chini ya kiwango*



*Sakafu katika shule ya sekondari ukenyenge iliyojengwa chini ya kiwango*

### 2.8.1.6 Ujenzi wa vyumba vitatu vya maabara katika shule ya sekondari Balele

Mnamo tarehe 10/11/2009 Halmashauri ya wilaya Kishapu iliingia mkataba na M/s Nima Enterprises wa S.LP 1, Kishapu kwa mkataba namba LGA/108/2009/10/W/DEV/C.15, kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba viwili vya madarasa Mwadui Technical, pia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa, maabara moja, nyumba ya mwalimu yenye vyumba vitatu na choo katika shule ya sekondari Balele. Thamani ya mkataba ya awali ilikuwa ni Sh. 66,669,354, baadaye mkandarasi aliongezewa kazi ya Sh. 11,100,600 kwa barua isiyo na Kumb. Namba ya tarehe 19/01/2010 hivyo kufanya jumla ya gharama ya mkataba kufikia Sh. 77,769,954. Mkataba huu ulianza tarehe 17/11/2009 na ulitegemewa kumalizika tarehe 1/2/2010, hata hivyo kazi zilizoongezeka hazikuainishwa. **Angalia Kielelezo AJ 24**

Mkandarasi huyu kwa ujumla alilipwa kiasi cha shilingi 20,565,280 ikiwa ni cheti cha malipo Na 01 kati ya gharama ya mkataba ya Sh.77, 769,954. **Angalia Kielelezo AJ 25**

**Mapungufu yaliyojitokeza.**

Timu ya ukaguzi maalum ilitembelea mradi huu mnamo tarehe 23/06/2011 na mapungufu yafuatayo yalibainika:

- Kazi za hatua ya kuweka zege la ndani (substructure) ikiwa na gharama ya Sh.8,716,950 zilikuwa hazijafanyika.

- Pia hadi timu ya ukaguzi ilipofika katika eneo la mradi ilibaini kuwa kazi hii ilikuwa imesimama na kazi ilikuwa imechelewa kumalizika kwa miezi 16 mpaka tarehe ya ukaguzi wa mradi huu kinyume na Kanuni Na. 119 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma 9GN 97) za 2005.

Picha za Maabara ya shule ya Sekonadari Balele ni kama zinavyoonekana hapa chini:



*Jengo la maabara shule ya sekondari Balele*

### 2.8.1.7 Ujenzi nyumba ya mwalimu pamoja na choo cha wanafunzi katika shule ya Sekondari Balele

Katika ujenzi wa nyumba hii ya Mwalimu pamoja na choo cha wanafunzi Mkandarasi alitakiwa kufanya kazi zifuatazo:

| Na. | Kazi aliyotakiwa kufanya | Thamani ya kazi (Shs) |
|---|---|---|
| 1. | Kuweka zege ya ndani (substructure) | 1,203,300 |
| 2. | Kuweka kenchi | 2,261,400 |
| 3. | Kupaua jengo kwa mabati gauges 28g | 1,660,954 |
| 4. | Kuweka milango pamoja na fremu zake | 3,480,790 |
| 5. | Kuweka madirisha pamoja na fremu zake | 2,090,000 |
| 6. | Kujenga shimo la maji taka | 800,000 |
| | **Jumla ndogo** | **11,496,444** |
| | Ujenzi wa choo | 1,472,060 |
| | **Jumla kuu** | **12,968,504** |

**Angalia Kielelezo AJ 26**

**Mapungufu yaliyojitokeza**

Timu ya ukaguzi maalum ilitembelea mradi huu mnamo tarehe 23/06/2011 na mapungufu yafuatayo yalibainika:

- Choo chenye thamani ya Sh.1, 472,060 hakikujengwa. **Angalia Kielelezo AJ27.**
- Madirisha pamoja na fremu zake vyenye thamani ya Sh.2,090,000 havikuwekwa. Pia milango pamoja na fremu zake vyenye thamani ya Sh.3,480,790 havikuwekwa.Vile vile Shimo la maji taka lenye gharama ya Sh.800,000 halikujengwa.

- Kazi kuchelewa kumalizika kwa miezi 16 mpaka tarehe ya ukaguzi wa miradi na hakuna hatua zilizochukuliwa na Uongozi wa Halmashauri kinyume na Kanuni Na. 119 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (GN 97) za 2005 kama inavyoonekana hapa chini:



*Nyumba ya mwalimu (vyumba vitatu) katika shule ya sekondari Balel*

### 2.8.1.8 Ukamilishaji wa vyumba vitatu vya maabara shule ya sekondari Talaga

Mnamo tarehe 10/11/2009 Halmashauri ya wilaya Kishapu iliingia mkataba na M/s Musa Romore wa S.LP 13, Kishapu kwa mkataba Na.LGA/108/2009/10/W/DEV/C.09 wa tarehe 10 /11/2009, kwa ajili aya ukamilishaji wa jengo la maabara, vyumba viwili vya madarasa katika shule ya sekondari Busiya na ukamilishaji wa maabara na vyumba vitatu vya madarasa shule ya sekondari Talaga. Thamani ya mkataba ilikuwa ni Sh. 72,260,760. Mkataba huu ulianza tarehe 17/11/2009 na ulitegemewa kumalizika 17/01/2010. **Angalia vielelezo AJ 28 na AJ 29.**

**Malipo kwa mkandarasi**

Mkandarasi huyu kwa ujumla alilipwa kiasi cha shilingi 42,190,650 kama inavyooneshwa hapa chini:

| Namba ya Cheti cha malipo | Kiasi (Sh.) | Tarehe ya Cheti |
|---|---:|---|
| Na. 01 | 20,241,300 | 10/12/2009 |
| Na. 02 | 4,621,350 | 27/04/2010 |
| Na. 03 | 17,328,000 | 25/08/2010 |
| **Jumla** | **42,190,650** | |

**Angalia Kielelezo AJ 30, AJ 31 ,AJ 32**

**Mapungufu yaliyojitokeza**

- "Ficial board" yenye thamani ya Sh. 420,000 haikuwekwa, Fremu na shata za milango yenye thamani ya Sh. 3,510,000 hazikuwekwa pia kazi za umaliziaji zenye jumla ya Sh. 1,497,000 hazikufanyika.
- Mbao za kenchi hazikuwekwa dawa ya kutosha, Nondo zilizotumika katika kutengeneza lenta ni milimita 10 badala ya 12mm ambazo thamani yake ni Sh. 1,190,820 na Sakafu yenye thamani ya Sh.6,545,450 haikuwekwa.
- Timu ya ukaguzi maalum ilitembelea mradi huu mnamo tarehe 23/06/2011 na kubaini kuwa kazi yaijakamilika na ilikuwa imechelewa kwa miezi 17 na hakuna hatua zilizochukuliwa na Uongozi wa Halmashauri kinyume na Kanuni Na. 119 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2005. Hali halisi ya ujenzi ni kama inavyoonekana katika picha hapa chini: **Angalia Kielelezo AJ 33**



*Chumba cha maabara shule ya sekondari Talaga ambacho hakijawekwa sakafu*

### 2.8.1.9 Ukamilishaji wa vyumba vitatu vya maabara shule ya sekondari Busiya

Mnamo tarehe 10/11/2009 Halmashauri ya wilaya Kishapu iliingia mkataba na M/s Musa Romore wa S.L.P 13, Kishapu kwa mkataba Na. LGA/108/2009/10/W/DEV/09/01 wa tarehe 02/11/2009 Kwa ajili aya ukamilishaji wa jengo la maabara, vyumba viwili vya madarasa shule ya sekondari Busiya na ukamilishaji wa maabara na vyumba vitatu vya madarasa shule ya sekondari Talaga. Thamani ya mkataba ilikuwa ni Sh. 72,260,760 mkataba huu ulianza tarehe 17/11/2009 na ulitegemewa kumalizika 17/01/2010.

**Mapungufu yaliyojitokeza**

- Timu ya ukaguzi maalum ilitembelea mradi huu mnamo tarehe 23/06/2011 na kukuta jengo lipo katika hatua ya lenta na kazi zilizoainishwa katika mkataba na BOQ hazijafanyika na Mkandarasi amelipwa kiasi cha Sh.42,190,650 kwa mujibu wa cheti cha malipo Na. 02 cha tarehe 27/02/2010. **Angalia Kielelezo AJ 34.**

- Mkataba umechelewa kukamilika kwa miezi 17 hadi terehe ya ukaguzi wa mradi huu na hakuna hatua zilizochukuliwa na Uongozi wa Halmashauri kinyume na Kanuni Na. 119 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (GN 97) za 2005. Hali halisi ya Jengo ni kama inavyoonekana katika picha hapa chini:



*Jengo la maabara shule ya sekondari Busiya*

### 2.8.1.10 Ukamilishaji wa vyumba viwili vya madarasa shule ya sekondari Busiya

Timu ya ukaguzi maalum ilipotembelea eneo la mradi mnamo tarehe 25/06/2011 na kufanya mahojiano na mwalimu Daudi Nyalulu na baadaye kufanya mahojiano kwa njia ya simu na Mwalimu mkuu wa shule hiyo Bwana Deogratias C. Bukani (mwenye nambari ya simu 0754250831) ilibaini kuwa gharama za makisio ya mradi (BOQ) na mkataba wa ujenzi zinaonesha mkandarasi alitakiwa kujenga madarasa mawili, lakini timu ya ukaguzi ilikuta madarasa matatu yaliyojengwa chini ya kiwango. **Angalia Kielelezo AJ 35**

Katika ujenzi wa madarasa haya ya shule ya sekondari Busiya Mkandarasi alitakiwa kufanya kazi zifuatazo:

| Na. | Kazi aliyotakiwa kufanya | Thamani ya kazi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | Kuweka zege ya ndani (substructure) | 2,400,000 |
| 2. | Kujenga ukuta superstructure | 1,125,000 |
| 3. | Kuweka milango na madirisha pamoja na fremu zake | 2,780,000 |
| | **Jumla** | **6,305,000** |

Ukaguzi maalum ulibaini mapungufu yafuatayo katika utekelezaji wa mkataba huu:

Kuna utata kuhusu kufahamu hatua ambayo mkandarasi huyo alianzia kujenga kwa awamu ya kumalizia, Sakafu imejengwa kwa kiwango kisichoridhisha na tayari imeanza kubanduka baada ya kutumika kwa muda mfupi, Madirisha yametengenezwa chini ya kiwango na Jengo hilo la madarasa halina sehemu ya kibaraza (verandah).

- Wavu uliowekwa kwenye madirisha umewekwa kwa mtindo wa kuunganisha vipande tofauti pasipo umakini na kuleta picha isiyopendeza na darasa hilo halijapigwa ripu ya kwenye msingi pamoja na kupakwa rangi.

**2.8.1.11 Ujenzi wa vyumba vya maabara katika shule ya sekondari Mwamashele**

Mnamo tarehe 10/11/2009 Halmashauri ya wilaya ya Kishapu iliingia mkataba na M/s Famoyo Contractors wa S.L.P 275, Kasulu kwa mkataba namba LGA/108/2009/10/W/DEV/C.12, kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vitatu vya maabara, nyumba ya mtumishi na madarasa mawili katika shule ya sekondari Mwamashele. Thamani ya mkataba ilikuwa ni Sh. 63,367,825 na kazi ilitakiwa kuanza tarehe 10/11/2009 na ilitegemewa kumalizika 09/01/2010. **Angalia Kielelezo J 36.**

Timu ya ukaguzi ilipotembelea katika eneo la mradi iliweza kubaini mapungufu yafuatayo:

- Mkandarasi alilipwa kiasi cha shilingi 20,104,445 kwa cheti Na 01 na mkataba huu ulivunjwa tarehe 10/02/2011 kwa barua yenye kumb. Na.LGA/108/2009/10/W/DEV/C.12/04 ya 10/11/2011 baada ya mkandarasi kutoonekana eneo la mradi kwa muda mrefu na hakufanya kazi yoyote. **Angalia Kielelezo AJ37,AJ 38 na AJ39**.
- Kazi haijafanyika tangu mkataba huu umevunjwa tarehe 10/11/2009 na wakati mkataba unavunjwa na muda wa kumaliza kazi ulishapita kwa miezi 13 hivyo mkandarasi alilipwa kwa kazi asiyoifanya.
- Kazi iliyofanyika katika awamu ya kwanza ilifikia usawa wa madirisha ilikuwa chini ya kiwango kutokana na mchanganyo wa sementi na mchanga kutofuata utaalamu na kazi hii iligharimu kiasi cha Sh.10,514,465.

- Jengo limefikia katika hatua ya ukuta na kuta zake zimepinda sana huku zikiwa na nyufa nyingi sana na kuta ziko katika hatari ya kuanguka kama linavyoonekana hapa chini:



*Sehemu ya jengo la maabara katika shule ya sekondari Mwamashele*



*Sehemu ya jengo la maabara katika shule ya sekondari Mwamashele*

### 2.8.1.12 Ujenzi wa nyumba ya mtumishi kijiji cha Lagana

Mnamo tarehe 10/11/2009 Halmashauri ya wilaya ya Kishapu iliingia mkataba na M/s Famoyo Contractors wa S.L.P. 275, Kasulu kwa mkataba namba LGA/108/2009/10/W/DEV/C.12 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vitatu vya maabara, nyumba ya mwalimu na madarasa mawili katika shule ya sekondari Mwamashele. Thamani ya mkataba ni Sh.63,367,825, mkataba ulianza tarehe 10/11/2009 na ulitegemewa kumalizika 09/01/2010. Mkandarasi alilipwa kiasi cha Sh. 20,104,445 na mkataba huu ulivunjwa tarehe 10/02/2011 kwa barua yenye kumb. Na.

LGA/108/20090/10/W/DEV/C.12/04 ya 10/11/2011 baada ya mkandarasi kutoonekana katika eneo la mradi kwa muda mrefu. **Angalia vielelezo AJ 40**

Hata hivyo timu ya ukaguzi maalum ilipotembelea katika mradi huo ilibaini mapungufu yafuatayo:

- Madirisha yenye thamani ya Sh. 1,755,000 hayakuwekwa, Milango ya ndani, chooni na stoo vyenye jumla ya Sh.480,000 havikuwekwa.
- Nyumba hiyo haijapakwa rangi na ilikuwa imetengewa kiasi cha Sh.800,000 na "fiscial board" zenye thamani ya Sh.234,000 hazikuwekwa.
- Wakati mkataba huu unavunjwa, nyumba ilikuwa haijamalizika na muda wa kumaliza kazi ulishapita kwa jumla ya miezi 13.
- Pia ilibainika kwamba katika nyumba hiyo kuna Mratibu Elimu wa Kata ya Lagana anaishi na familia yake pasipo kukabidhiwa na kabla haijamalizika.
- Hata hivyo pamoja na kazi zilizoorodheshwa kutofanyika ipasavyo, cheti cha malipo Na. 01 kilichotolewa na kasainiwa na Mkandarasi wa Wilaya Eng.Loenard Mashamba kilionesha kuwa kazi hizo zilikwishakamilika, ingawa baadaye kazi hizo kuachwa bila kukamilika.



*Nyumba ya Mwalimu kijiji cha Lagana*

### 2.8.1.13 Ukamilishaji wa vyumba viwili vya maabara Mangu sekondari

Mnamo tarehe 10/11/2009 Halmashauri ya wilaya ya Kishapu iliingia mkataba na M/s Rubebe Building contractors wa S.L.P 2001, Shinyanga kwa mkataba

namba LGA/108/2009/10/W/DEV/C.01, kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vitatu vya maabara katika shule za sekondari za Mangu na Bulekela. Thamani ya mkataba ilikuwa ni Sh.63,263,270 na mkataba huu ulianza tarehe 10/11/2009 na ulitegemewa kumalizika 09/01/2010. Mkataba huu ulikuwa ni mwendelezo wa ujenzi wa maabara katika awamu ya pili baada ya awamu ya kwanza kuishia katika hatua ya ukuta chini ya madirisha. **Angalia Kielelezo AJ 41**

Mkandarasi huyu kwa ujumla alilipwa kiasi cha shilingi 37,390,640 kati ya gharama ya mkataba ya Shs.63,263,270 kama inavyooneshwa hapa chini:

| **Namba ya Cheti cha malipo** | **Kiasi (Sh.)** | **Tarehe ya Cheti** |
|---|---:|---|
| Na. 01 | 16,608,900 | 14/12/2009 |
| Na. 02 | 6,541,000 | 27/04/2010 |
| Na. 03 | 14,240,740 | 25/08/2010 |
| **Jumla** | **37,390,640** | |

**Angalia Kielelezo AJ 42, AJ 43 , AJ 44 na AJ45**

Hata hivyo timu ya ukaguzi huu maalum ilipotembelea mradi huu mnamo tarehe 24/06/2011, ili kujua utelezaji wa mradi huu iliweza kufanya mahojiano na Mwalimu mkuu wa shule Bw. Shija Dominic Kulewa na kubaini kuwa kulikuwa na makubaliano kati ya wananchi na Halmashauri kwamba maabara hii itajengwa na wananchi kwa fedha za Halmashauri katika hatua ya kuchimba msingi na kufyatua matofali na baadaye Halmashauri kumalizia kazi zote zilizobaki kwa kutumia mkandarasi.

Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo katika utekelezaji wa mradi huu:

- Lenta na ukuta vimejengwa chini ya kiwango ambapo nondo ziko nje ya zege na lenta zimekatika magungufu haya yalitokana na usimamizi dhaifu wa Mhandisi wa Ujenzi.
- Kazi za umaliziaji zenye thamani ya Sh. 23,747,580 kuanzia hatua ya ukuta hazikufanyika.
- Pamoja na kutoendelea na kazi na kutokuwepo katika eneo la kazi, mkandarasi hajachukuliwa hatua yeyote na Halmashauri.
- Ilibainika kuwa Mkandarasi pamoja na kulipwa hayupo katika eneo la mradi kwa muda mrefu sasa.
- Mkandarasi ameshindwa kumaliza kazi zilizoainishwa katika mkataba kwa muda wa miezi 17 na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na Uongozi wa Halmashauri kinyume na Kanuni Na. 119 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2005. Hali halisi ya Jengo ni kama inavyoonekana katika picha hapa chini:



*Jengo la maabara shule ya sekondari Mangu jinsi linavyoonekana*



*Jengo la maabara shule ya sekondari Mangu jinsi linavyoonekana*

### 2.8.1.14 Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya maabara shule ya sekondari Kiloleli

Ujenzi wa Maabara ya vyumba vitatu (3) shule ya sekondari Kiloleli hadi hatua moja chini ya sehemu yanapoanzia madirisha, ulitekelezwa na wananchi na fedha za Halmashauri na baada ya hapo awamu ya pili ya ujenzi haijaendelea. Timu ya ukaguzi ilipotembelea eneo la mradi haikupata ushahidi wowote au kuona dalili zozote za kuuendeleza mradi kwa siku za karibuni hivyo mradi huu kuwa umetelekezwa. Vile vile kulikuwa na dalili za

wazi kuonesha kuwa hata matofali yaliyotumika katika hatua za mwanzo za ujenzi yalikuwa chini ya kiwango cha ubora, kwa vile yalishaanza kumeguka.

**Mapungufu yafuatayo yalibainika wakati wa ukaguzi:**

- Mkataba wa ujenzi wa maabara hiyo wa awamu ya pili, haukuweza kutolewa na sababu za kutoendelea kwa ujenzi wa mradi na zile zilizopelekea ujenzi ukafanyika katika kiwango duni hazijabainishwa.
- Kasoro nyingi zilijizojitokeza zilitokana na udhaifu katika usimamizi na kutoshirikishwa kwa Uongozi wa shule katika kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mradi.

Picha ya jengo la maabara ya shule ya sekondari Kiloleli ni kama inavyoonekana hapa chini:



*Jengo la Maabara, shule ya Sekondari Kiloleli, lilivyokuwa mwezi Juni, 2011*

### 2.8.1.15 Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya maabara shule ya sekondari Wishiteleja

Ujenzi wa awamu ya kwanza wa Maabara ya vyumba vitatu (3) shule ya sekondari Wishiteleja, ulitekelezwa kwa nguvu za wananchi na fedha za Halmashauri, kutoka hatua ya msingi hadi kuishia katika hatua ya ukuta chini ya madirisha, baada ya hapo ujenzi ulifanywa na Mkandarasi M/S DGS Co. Ltd wa S.L.P. 482 Bariadi aliyejenga mpaka hatua ya upauaji. Timu ya ukaguzi ilipotembelea eneo la mradi haikupata ushahidi wowote au kuona dalili zozote za kuuendeleza mradi kwa siku za karibuni. Vile vile mapungufu yafuatayo yalibainika:

- Mkataba wa ujenzi wa Maabara hiyo haukuwasilishwa kwa ukaguzi, jengo halijakamilika na sakafu na milango hazijawekwa pia rangi haijapakwa.

- Ujenzi wa jengo haukuzingatia viwango na hivyo kupelekea ukuta wa “gabble” kubomolewa. Ripu, milango, madirisha pamoja na “frem” zake havikuwepo na mfumo wa utoaji maji na mfumo wa umeme vilikuwa bado kujengwa.

- Kazi hii ilikuwa imesimama kwa muda mrefu kwa madai kwamba mkandarasi alifariki. Hivyo kulikuwa na wasiwasi kuwa ujenzi haungeweza kuendelea.

Picha za jengo la maabara ya shule ya sekondari Wishiteleja ni kama inavyoonekana hapa chini:



*Vyumba vitatu (3) vya maabara shule ya sekondari Wishiteleja kama inavyoonekana nje*



*Sehemu ya jengo la Maabara shule ya sekondari Wishiteleja ilivyo ndani.*

### 2.8.1.16 Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya madarasa shule ya sekondari Wishiteleja

Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya madarasa ya shule ya sekondari Wishiteleja ulifanywa na Mkandarasi M/S DGS Co. Ltd wa S.L.P. 482 Bariadi. Timu ya ukaguzi ilipotembelea eneo la mradi ilibaini mapungufu yafuatayo:

- Mkataba wa ujenzi wa Madarasa hayo haukuwasilishwa kwa ukaguzi na darasa moja limekamilika na mengine mawili hayajakamilika na moja liko hatua ya msingi na jingine hatua ya umaliziaji.

- Kazi ya ujenzi imesimama kwa muda mrefu kwa madai kwamba mkandarasi alifariki, hivyo kulikuwa na wasiwasi kuwa ujenzi haungeweza kuendelea.

Picha ya jengo la madarasa ya shule ya sekondari Wishiteleja ni kama inavyoonekana hapa chini:



*Moja ya madarasa matatu (3) shule ya Sekondari Wishiteleja ambalo liko hatua ya msingi*

### 2.8.1.17 Ujenzi wa nyumba ya Mwalimu shule ya sekondari Wishiteleja

Ujenzi wa nyumba ya Mwalimu shule ya sekondari Wishiteleja ulifanywa na Mkandarasi M/S DGS Co. Ltd wa S.L.P. 482 Bariadi. Timu ya ukaguzi ilipotembelea eneo la mradi ilibaini mapungufu kama vile nyumba haikuwa na milango ya chooni, stoo na bafu pia milango miwili ya ndani haikuwepo.Zaidi ya hayo umaliziaji wa "fascia board" haukufanyika.

Picha za jengo la nyumba ya mwalimu shule ya sekondari Wishiteleja ni kama zinavyoonekana hapa chini:



*Nyumba ya Mwalimu shule ya sekondari Wishiteleja kama ilivyo nje*



*Milango ya Jiko na stoo ya nyumba ya Mwalimu shule ya sekondari Wishiteleja*

### 2.8.1.18 Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya maabara shule ya sekondari Songwa

Ujenzi wa Maabara ya vyumba vitatu (3) shule ya sekondari Songwa hadi hatua ya upauaji, ulitekelezwa na wananchi kwa kutumia fedha zilizotolewa na Halmashauri, kutoka hatua ya msingi hadi hatua yanapoanzia madirisha, baada ya hapo ujenzi ulifanywa na Mkandarasi aliyejenga mpaka hatua ya upauaji. Timu ya ukaguzi ilipotembelea eneo la mradi mapungufu yafuatayo yalibainika:

- Mkataba wa ujenzi wa Maabara hiyo haukuwasilishwa kwa ukaguzi, jengo halijakamilika pia sakafu na milango havijawekwa.

- Rangi haijapakwa pia ripu, milango, madirisha pamoja na frem zake havikuwepo

Picha za jengo la Maabara shule ya sekondari Songwa ni kama zinavyoonekana hapa chini:



*Jengo la Maabara shule ya Sekondari Songwa kama linavyoonekana nje*

Sababu zilizopelekea kuzorota kwa ukamilishaji wa ujenzi wa maabara ni kukosekana kwa usimamizi madhubuti na ufuatiliaji wa karibu wakati wa kutekeleza miradi na kukosekana kwa umakini kwa watendaji wa idara ya ujenzi katika kukagua na kutoa taarifa ya ukaguzi wa kazi na hivyo kuishawishi Halmashauri kuwalipa wakandarasi kwa kazi ambazo hazijafanyika, hali ambayo imepelekea kuchelewa kukamilika kwa maabara,shule na nyumba za walimu kwa wakati kunasababisha gharama za vifaa vya ujenzi kuongezeka, hatimaye mkandarasi anaweza kufanya kazi ya ujenzi iliyo chini ya kiwango kwa kuepuka hasara. Hii ikitokea, thamani ya kazi itakuwa hailingani na thamani ya fedha zilizotolewa wakati wa makubaliano ya awali.

**Mapendekezo**

- Mapungufu yaliyojitokeza yarekebishwe na Halmashauri ihakikishe kazi za ujenzi zinakamilika ndani ya wakati uliokubalika, vinginevyo Wakandarasi wachukuliwe hatua muafaka kulingana makubaliano yalivyo kwenye mkataba.
- Menejimenti itoe maelezo ya kina kuhusu mipango ya kukamilisha ujenzi wa majengo yote ambayo hayajakamilika na sababu za kutowasilishwa kwa mikataba kwa baadhi ya majengo kwa ajili ya ukaguzi. Mhandisi wa Wilaya Bwana Leoard Mashamba na Afisa Ugavi Bwana Medson Matarana wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa kusababisha kukosekana kwa Mikataba.

- Mhandisi Bwana Leonard Mashamba awajibike kwa usimamizi mbovu wa Miradi hii.
- Katika kutekeleza kazi za miradi ambayo ipo katika hatua za umaliziaji Halmashuri inatakiwa kuonesha bayana katika Mkataba na BOQ hatua ambayo mkandarasi aliyepitishwa anatakiwa kuanzia au kumalizia kabla ya kuanza umaliziaji huo ili kuondoa utata katika kutambua kazi anazotakiwa kufanya.
- Kuweko na ushirikishwaji thabiti kwa Uongozi wa Shule katika kila kazi inayofanyika hata kama kazi hiyo inafanyika kwa fedha inayotoka moja kwa moja kutoka Halmashauri.

## 2.9 MIRADI YA TASAF

### 2.9.1 Ujenzi wa madarasa mawili katika shule ya sekondari Igaga “B”

Katika Mwaka wa fedha 2008/2009 Halmashauri ya wilaya ya Kishapu katika kutekeleza miradi yake kupitia mfuko wa jamii (TASAF) ilitoa kwa kamati ya ujenzi kiasi cha Sh.36, 232,660 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili katika Shule ya Sekondari ya Igaga “B” kwa ajili ya kugharimia shughuli zifuatazo:

| Na | Maelezo ya kazi | Thamani yakazi (shs) |
|---|---|---|
| 1. | Vifaa vya kazi | 965,000 |
| 2. | Gharama za usafirishaji wa vifaa vya kazi | 9,589,400 |
| 3. | Kuchimba na kujenga msingi | 5,458,460 |
| 4. | Kujenga ukuta wa matofali | 4,949,000 |
| 5. | Kupaua | 6,349,500 |
| 6. | Kupachika Milango na madirisha | 6,496,600 |
| 7. | Umaliziaji | 1,105,500 |
| 8. | Kupaka rangi | 170,000 |
| 9. | mafunzo ya CMC kwa siku 3 | 683,600 |
| 10. | Kazi za nje | 232,800 |
| 11. | Gharama za utawala | 232,800 |
| **Jumla** | | **36,232,660** |

**Angalia Kielelezo AJ46.**

**Mapungufu yaliyojitokeza**

Timu ya ukaguzi maalum ilipotembelea mradi huu ili kujua utekelezaji wake ilibaini mapungufu yafuatayo:

- Kati ya madirisha kumi yaliyopo madirisha matano hayana fremu na hakuna wavu mkubwa (weld mesh). Pia hakuna fremu za milango pamoja na shutter katika madarasa vyote vina thamani ya Sh. 6,724,944.
- Ripu ya ndani na nje haijapigwa ambayo gharama yake ni Sh. 1,999,800 na dari ya nyumba haijawekwa gharama yake ni Sh. 1,822,000.
- “Fiscial boards” zenye gharama ya Sh 414,000 hazikuwekwa , rangi haikupakwa gharama yake ni Sh. 1,245,000, sakafu haijawekwa ambayo gharama yake ni

Sh.867,800 pia samani zote zilizoainishwa katika BOQ hazijatengenezwa na kupelekwa katika mradi gharama yake ni Sh. 112,000.

- Katika kupitia kumbukumbu za mkataba huo, ilibainika kwamba hadi kufikia kipindi hiki cha ukaguzi maalum muda uliopangwa kumaliza kazi hiyo ulikuwa tayari umekwisha kulingana malengo ya kamati ya mradi (yaani miezi 19 tangu tarehe 8/11/2009) na hadi sasa hakuna kazi inayoendelea.
- Pia katika kupitia mkataba huo wenye Na. KISHO/SP/17 ilibainika kwamba kuna utata katika gharama zilizoainishwa na kuafikiwa kuhusu jumla ya gharama ya kusafirisha vifaa vya kazi na gharama ya vifaa vilivyonunuliwa. Gharama ya ununuzi wa vifaa vya kazi ni Sh. 965,000 na gharama ya kusafirisha vifaa hivyo ni Sh. 9,589,400 ambayo ni mara kumi (10) zaidi ya gharama za ununuzi wa vifaa hivyo. **Angalia Kielelezo AJ 46 na 47**

Picha ya madarasa mawili yaliyojengwa katika shule ya sekondari Igaga "B" ni kama inavyoonekana hapa chini:



*Jengo la madarasa mawili katika Shule ya sekondari Igaga ambalo bado halijakamilika*

### 2.9.2 Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) zahanati ya Mwamanota

Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Halmashauri ilitoa kwa kamati ya ujenzi kiasi cha Sh.28,695,282 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la OPD katika zahanati ya Mwamanota na mchango toka kwa wananchi ulikadiriwa kuwa Sh.7,695,475. **Angalia Kielelezo AJ 48.**

Katika kutekeleza mradi huu Halmashauri ilianisha gharama za mradi kama ifuatavyo:

| Na | Maelezo ya kazi | Thamani ya kazi (shs) |
|---|---|---:|
| 1. | Vifaa vya kazi | 1,069,500 |
| 2. | Gharama za usafirishaji wa vifaa vya kazi | 600,000 |
| 3. | Kuchimba msingi | 7,359,380 |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Kujenga ukuta wa matofali | 6,199,100 |
| 5. | Kupaua | 5,900,177 |
| 6. | Kupachika Milango na madirisha | 4,100,500 |
| 7. | Umaliziaji | 6,590,500 |
| 8. | Kupaka rangi | 2,090,200 |
| | | |
| | | |
| 9. | Mafunzo ya CMC kwa siku 3 | 578,600 |
| 10. | Kazi za nje | 170,000 |
| 11. | Gharama za Utawala | 232,800 |
| 12. | Uvunaji maji ya mvua | 1,497,000 |
| **Jumla** | | **36,387,757** |

**Mapungufu yaliyojitokeza**

- Jengo limekamilika lakini bado halijaanza kutumika, ila mkandarasi hajaweka makinga maji yenye gharama ya Sh.491,200.
- Tarehe ya kuanza na kumaliza kazi ya ujenzi haikuwekwa wazi katika mkataba kinyume na kanuni Namba 105 ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma (GN 97) za mwaka 2005.

Picha ya jengo la idara ya wagonjwa wa nje (OPD) katika zahanati ya Mwamanota ni kama inavyoonekana hapa chini:



### 2.9.3 Ujenzi wa jengo la idara ya wagonjwa wa nje (OPD) katika zahanati ya Kisesa

Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Halmashauri ilitoa kwa kamati ya ujenzi kiasi cha Sh.28,695,282 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la OPD katika zahanati ya Kisesa na mchango wa wananchi ulikadiriwa kuwa Sh.7,695,475, gharama za mradi ni kama ifuatavyo:

| Na | Maelezo ya kazi | Thamani ya kazi (shs) |
|---|---|---:|
| 1. | Vifaa vya kazi | 1,069,500 |
| 2. | Gharama za usafirishaji wa vifaa vya kazi | 600,000 |
| 3. | Kuchimba msingi | 7,359,380 |
| 4. | Kujenga ukuta wa matofali | 6,199,100 |
| 5. | Kupaua | 5,900,177 |
| 6. | Kupachika Milango na madirisha | 4,100,500 |
| 7. | Umaliziaji | 6,590,500 |
| 8. | Kupaka rangi | 2,090,200 |
| 9. | mafunzo ya CMC kwa siku 3 | 578,600 |
| 10. | Kazi za nje | 170,000 |
| 11. | Gharama za utawala | 232,800 |
| 12. | Uvunaji maji ya mvua | 1,497,000 |
| | **Jumla** | **36,387,757** |

**Angalia Kielelezo AJ 49.**

**Mapungufu yaliyojitokeza**

- Jengo limekamilika lakini bado halijaanza kutumika.Rangi iliyopakwa mara moja (mkono mmoja) tu badala ya mara tatu ambayo gharama yake ni Sh. 1,393,466.
- Kumekuwa na uwazi mkubwa kati ya mlango na fremu na pia makinga maji bado hayajawekwa katika paa ambayo gharama yake ni Sh. 491,200. Tarehe ya kuanza na kumaliza kazi ya ujenzi haikuwekwa wazi katika mkataba kinyume na kanuni Namba 105 ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma (GN 97) za mwaka 2005.

Picha ya jengo la idara ya wagonjwa wa nje (OPD) katika zahanati ya Kisesa ni kama inavyoonekana hapa chini:



*Jengo la Idara ya wagonjwa wa nje (OPD) katika zahanati ya kisesa*

### 2.9.4. Ujenzi wa jengo la idara ya wagonjwa wa nje (OPD) katika zahanati ya Bulima

Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Halmashauri) ilitoa kwa kamati ya ujenzi kiasi cha Sh.28,695,282 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la OPD katika zahanati ya Kisesa na mchango toka kwa wananchi ulikadiriwa kuwa Sh.7,695,475. Gharama za mradi ni kama ifuatavyo:

| Na | Maelezo ya kazi | Thamani ya kazi (shs) |
|---|---|---:|
| 1. | Ununuzi wa vifaa vya kazi | 1,069,500 |
| 2. | Gharama za usafirishaji wa vifaa vya kazi | 600,000 |
| 3. | Kuchimba msingi | 7,359,380 |
| 4. | Kujenga ukuta wa matofali | 6,199,100 |
| 5. | Kupaua | 5,900,177 |
| 6. | Kupachika Milango na madirisha | 4,100,500 |
| 7. | Umaliziaji | 6,590,500 |
| 8. | Kupaka rangi | 2,090,200 |
| 9. | Mafunzo ya CMC | 578,600 |
| 10. | Kazi za nje | 170,000 |
| 11. | Gharama za utawala | 232,800 |
| 12. | Uvunaji maji ya mvua | 1,497,000 |
| **Jumla** | | **36,387,757** |

**Angalia Kielelezo AJ 50 na AJ 51**

**Mapungufu yaliyojitokeza.**

- Mkataba hauna muda maalum wa kuanza na kukamilika, kutokana na udhaifu huo, utekelezaji umechukua muda mrefu kukamilika kwani mpaka timu ya ukaguzi maalum ilipokuwa inatembelea eneo la mradi mwezi Juni, 2011, ujenzi ulikuwa bado unaendelea na hakuna hatua iliyochukuliwa na Uongozi wa

Halmashauri kinyume na Kanuni Na, 119 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2005.

- Kazi zilizokuwa bado kufanyika wakati wa mradi hadi mwezi Juni,2011 ni pamoja na uvunaji wa maji ya mvua ambao gharama yake ni Sh. 1,497,000.00 , Dari (Ceiling board) yenye gharama ya Sh. 1,857,800.00 , Kazi za nje zenye thamani ya Sh. 170,000 .

Picha ya jengo la idara ya wagonjwa wa nje (OPD) katika zahanati ya Bulima ni kama inavyoonekana hapa chini:



*Jengo la idara ya wagonjwa wa nje (OPD) katika zahanati ya Bulima*

### 2.9.5. Ujenzi wa Josho la Mifugo Mwamanota

Moja ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kupitia mfuko wa TASAF, kwa mwaka wa fedha 2008/2009 ni ujenzi wa Josho la Mwamanota. Mradi huu ulitekelezwa na Mkandarasi M/S Famoyo Contractor wa S.L.P. 227 Shinyanga, kwa mkataba Na. KDC/DASIP/M.NOTA/02 kwa gharama ya Sh. 12,660,780. **Angalia Kielelezo AJ 52.**

Timu ya ukaguzi ilipotembelea eneo la mradi, ilikuta mradi umekamilika, ingawa Josho lilikuwa halitumiki na halikuwa na maji. Hivyo mradi huu ulionekana kutokuwa na tija na usio endelevu kutokana na kutotekeleza lengo kusudiwa. Picha ya Josho ni kama inavyoonekana hapa chini:



*Josho la Mwamanota ambalo halijatumika tangu limekamilika.*

### 2.9.6. Mradi ya ujenzi wa Lambo la Ng'wang'halanga.

Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Halmashauri ilitekeleza kazi ya ujenzi wa Lambo la Ng'wang'halanga kwa kutumia mfuko TASAF kwa mkataba Na. KISH 1/FS/005, iliyofanywa na mkandarasi M/s CMC kwa gharama ya Sh. 28,997,430. Ujenzi ulifanyika kwa wiki 7, kuanzia tarehe 11/09/2010 hadi 13/11/2010. Nia ya ujenzi wa Lambo hilo ni kuhifadhi maji kwa ajili ya matumizi ya watu, mifugo na kilimo cha umwagiliaji. **Angalia Kielelezo AJ 53.**

Timu ya ukauzi maalum ilitembelea mradi huo na kubaini mapungufu yafuatayo:

- Lambo halina eneo rafiki kimazingira inayoliwezesha kuhimili ukosefu wa mvua kwa muda mrefu au mvua nyingi. Halijazungukwa na aina yeyote ya miti.
- Lambo lilijengwa bila kuzingatia haja ya kuhifadhi mazingira yanayolizunguka na hivyo kutokuwa endelevu.
- Mradi haukuwa na vyanzo vya maji vya kudumu, na hivyo kuwa na uwezekano wa kukauka kunapokuwa na vipindi virefu vya upungufu/ukosefu wa mvua.
- Miradi kutotimiza malengo ya kuwasaidia wananchi kutekeleza kilimo cha umwagiliaji, kutokana na uchache wa maji.
- Mahitaji ya maji yalikuwa makubwa kuliko uwezo wa Lambo kuhimili, hasa wakati wa kiangazi ambapo lambo hilo maji yanakauka kama inavyoonekana katika picha:



*Lambo la Ng'wang'halanga likiwa halina maji ya kutosha mwezi Juni, 2011*

**Mapendekezo**

- Ujenzi wa Malambo uzingatie maeneo muafaka ili kulinda fedha za umma na kuepusha kufanyika mradi ambao haukidhi mahitaji ya eneo husika.
- Uhifadhi wa mazingira kwa maeneo yanayolizunguka lambo ni vyema ukazingatiwa ili kulinda eneo la mradi.

## 2.10 MIRADI YA PEDP

### 2.10.1 Ukamilishaji ujenzi wa madarasa ya Shule ya msingi za Ipililo, Mwamala na Maganzo

Mnamo tarehe 10/11/2009 Halmashauri ya wilaya Kishapu iliingia mkataba na M/s Senga Senga Civil and Building Contractors wa S.L.P 1176, Kishapu kwa mkataba namba LGA/108/2009/10/W/PEDP/C.14 wa ukamilishaji wa madarasa 3 Shule ya msingi Ipililo, madarasa 2 Shule Msingi Mwamala na madarasa 2 Shule ya msingi Maganzo, kwa kiasi cha Sh.33,861,380, kazi ilitakiwa kuanza tarehe 17/11/2009 na kumalizika tarehe 17/01/2010. **Angalia Kielelezo AJ 54**.

#### 2.10.1.1 Ukamilishaji wa madarasa 3 katika shule ya msingi Ipililo

Ujenzi wa madarasa katika shule ya msingi Ipililo ulianza kwa nguvu za wananchi na kufikisha madarasa hayo katika hatua ya ukuta na baadaye kumaliziwa na Halmashauri.

Kwa mujibu wa cheti cha malipo Na. 2 cha tarehe 30/7/2010 Mkandarasi alishalipwa jumla ya Sh. 22,151,662 kati ya gharama ya mkataba ya Sh. 33,861,380, aidha cheti cha malipo namba 1 hakikuwasilishwa kwa ukaguzi kama ilivyokubalika. Mkandarasi alitakiwa kufanya kazi zifuatazo kama zilivyooneshwa katika BOQ. **Angalia Kielelezo AJ 55 na AJ 56.**

Hata hivyo ukaguzi huu maalum ulipotembelea mradi huu mnamo tarehe 25/06/2011 ili kujua utekelezaji wake pamoja na kufanya mahojiano na walimu wakiwemo Mwl. Bernad Shilatu na Mwl.Justo Yusuph ambao walikuwepo tangu kuanza kwa ujenzi wa madarasa hayo, ilibainika kuwa madarasa hayo yalijengwa kwa nguvu za wananchi hadi kufikia usawa wa linta na baadaye kuendalezwa na Mkandarasi kwa hatua iliyobaki.

Timu ya ukaguzi ilibaini mapungufu yafuatayo:

- Ujenzi uliofanyika kuanzia hatua ya msingi hadi hatua ya madirisha kabla kuwekwa Lenta ulifanywa kwa mchango wa Halmashauri, kabla ya mkataba huu, lakini BOQ iliyotumika katika mkataba huu inaonesha kuwa kazi hiyo alipewa mkandarasi. **Angalia Kielelezo AJ54, AJ 55 na AJ 57(2)**
- Ukuta wa "gabble" wenye thamani ya Sh.348,000 haujajengwa na ujenzi wa kenchi, uezekaji pamoja na umaliziaji wa sakafu na ripu wenye thamani ya Sh. 8,389,080 havijafanyika na hakuna dalili ya Mkandarasi kuwepo eneo la mradi hadi kenchi alizozitayarisha kwa takribani mwaka zimeshaoza na kuliwa na mchwa na hazifai tena kwa ujenzi.
- Ushirikishwaji duni wa mkuu wa idara ya Elimu (Afisa Elimu- msingi Mr. Magubiki) ambaye alionekana kutofahamu lolote juu ya ujenzi na matatizo yaliyopo. Afisa huyu wa elimu aliambatana na timu ya ukaguzi na alikiri kuwa hafahamu lolote kuhusu ujenzi na matatizo yaliyopo.
- Ilibainika wazi kutokuwepo kwa uaminifu katika utendaji wa Halmashauri hasa mhandisi wa ujenzi (Eng. L.B.L Mashamba) ambaye alisaini na kuidhinisha malipo ya cheti cha malipo Na.01 (certificate of certification) kuthibitisha kuwa kazi iliyofanyika imekaguliwa na kuonekana inaridhisha kinyume na hali halisi. **Angalia kielelzo AJ 58**
- Katika kupitia mafaili mbalimbali ya wakandarasi, ukaguzi huu maalum ulibaini kuwepo kwa ucheleshwaji wa malipo kwa wakandarasi. Hii ni kutokana na barua za malalamiko ya mkandarasi, zilizopatikana katika mafaili hayo. **Angalia kielelzo AJ 59.**
- Ujenzi wa linta ulifanyika chini ya kiwango, kulingana na barua yenye folio Na. 8 katika faili la mkandarasi iliyoandikwa na msimamizi wa kazi Bwana George Medadi kutoka ofisi ya Mhandisi wa Wilaya katika ripoti yake ya ukaguzi iliyotolewa tarehe 06 Aprili 2010 ikimtaka mkandarasi kuvunja lenta hiyo na kutenganeza upya, hata hivyo timu ya ukaguzi haikuweza kupata uthibitisho kama mapungufu hayo yalirekebishwa. **Angalia Kielelezo AJ 57(1)**
- Mradi haujakamilika, mpaka wakati wa ukaguzi huu uliofanyika Juni, 2011 ilishapita miezi 17 tangu tarehe ya kumaliza kazi kufika na hakuna hatua

iliyochukuliwa na uongozi wa Halmashauri kinyume na Kanuni 119 ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma (GN 97) za mwaka 2005.

Picha za jengo la madarasa matatu katika Shule ya msingi Ipililo na kenchi ni kama zinavyoonekana hapa chini:



*Jengo la darasa katika shule ya msingi Ipililo ambalo limeachwa kwa muda mrefu likiwa limejengwa chini ya kiwango.*



*Kenchi zilizokutwa zimeachwa kwa muda wa mwaka mzima katika shule ya msingi Ipililo – Kishapu*

**2.10.1.2 Ujenzi madarasa mawili katika Shule ya msingi Mwamala.**

Timu ya ukaguzi maalum ulipotembelea eneo la mradi na kufanya mahojiano na wananchi akiwemo Mwalimu James Mshobozi ili kufahamu utekelezaji wa mradi huu ilibainika kwamba, ujenzi wa jengo hili ulianza kwa Halmashauri kupeleka fedha shuleni na mchango wa nguvu za wananchi hadi kufikia hatua ya madirisha na kwa

mkataba huu Halmashauri iliingia mkataba na mkandarasi M/s Senga Senga wa kumalizia kazi kuanzia ujenzi wa lenta.

**Mapungufu yaliyojitokeza**

- Ujenzi uliofanyika kuanzia hatua ya msingi hadi hatua ya madirisha kabla kuwekwa Lenta ulifanywa kwa mchango wa halmashauri, kabla ya mkataba huu, lakini BOQ iliyotumika katika mkataba huu inaonesha kuwa kazi hiyo alipewa mkandarasi lakini katika BOQ ziliorodheshwa kazi ambazo zilikuwa zimeshafanyika.**Angalia Kielelezo AJ 60 na AJ 57(2)**

- Ilibainika kwamba katika jengo hilo kuna mabati ambayo yaligundulika kuwa hayajakidhi viwango vilivyothibishwa katika uezekaji wa majengo ya Serikali (yaani gauge 28), mkandarasi aliweka mabati yenye geji 30 badala ya geji 28. Baada ya mahojiano na Mwalimu James Mshobozi ambaye alikuwepo tangu jengo hilo lilipoanza kujengwa, alisema kuwa mkandarasi aliamriwa na uongozi wa Halmashuri (George Medadi – Ofisi ya Mhandisi) kuondoa mabati hayo lakini hakufanya hivyo. Pia timu ya ukaguzi maalum ilipitia faili la mkandarasi huyo na kubaini kulikuwepo na ushahidi wa kimaandishi wa barua ya tarehe 06/04/2010 iliyokuwa ikimtaka Mkandarasi huyo kuondoa mabati hayo**,** pia barua hiyo ilimtaka Mkandarasi huyo kuondoa sehemu ya zege (jamvi) ya sakafu iliyowekwa chini ya kiwango na kuweka nyingine. Pia kumekuwa na mipasuko mingi kwenye baadhi ya kuta na **"**Ceiling board" yenye thamani ya shilingi 1,172,000 haikuwekwa katika jengo hilo. Vile vile imebainika kuwa sakafu iliyowekwa ilikuwa chini ya kiwango na lenta iliyowekwa ilikuwa na nondo mbili (2) tu badala ya nne (4). **Rejea kielelezo AJ 61**

  Picha za jengo la madarasa mawili katika Shule ya msingi Mwamala ni kama zinavyoonekana hapa chini:



*Madarasa mawili katika shule ya msingi Mwamala yaliyojengwa chini ya kiwango na nyufa hatarishi (horizontal cracks)*

### 2.10.1.3 Ujenzi madarasa 3 katika Shule ya msingi Maganzo

Timu ya ukaguzi maalum ulipotembelea eneo la mradi na kufanya mahojiano na wananchi akiwemo Mwalimu James Mshobozi ili kufahamu utekelezaji wa mradi huu ilibainika kwamba, ujenzi wa jengo hili ulianza kwa Halmashauri kupeleka fedha shuleni na mchango wa nguvu za wananchi hadi kufikia hatua kufikia hatua ya lenta na Halmashauri iliingia mkataba na mkandarasi M/s Senga Senga wa kumalizia kazi kuanzia ujenzi wa gebo.

**Mapungufu yaliyojitokeza**

- Ujenzi uliofanyika kuanzia hatua ya msingi hadi hatua ya lenta kabla kuwekwa gebo kazi ilifanywa kwa mchango wa fedha toka Halmashauri pamoja na mchango wa wananchi, kabla ya mkataba huu, lakini BOQ iliyotumika katika mkataba huu inaonesha kuwa kazi hiyo alipewa mkandarasi lakini katika BOQ ziliainishwa kazi ambazo zilifanyika. **Angalia Kielelezo AJ 57(2) na AJ 62**

- Kazi ilishakamilika na madarasa yalikuwa yakitumika. Hata hivyo, katika kupitia BOQ na kulinganisha Ceiling board yenye thamani ya Sh. 1,152,000 haikuwekwa. **Angalia Kielelezo AJ 62**



*Jengo la madarasa katika shule ya msingi Maganzo*

### 2.10.2 Ujenzi wa nyumba ya Mwalimu shule ya msingi Mwamashimba

Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Halmashauri ilitekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba ya Mwalimu (Two in one) shule ya msingi Mwamashimba**,** chini ya mpango wa PEDEP/MMEM. Halmashauri ilichangia Sh.5, 000,000 kusaidia nguvu za wananchi. Timu ya ukaguzi maalum ilipotembelea mradi huo, ilibaini mapungufu yafuatayo:

- Mkataba na BOQ havikuweza kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, nyumba ilikuwa haijakamilika na ilikuwa imejengwa upande mmoja na upande wa pili umeishia kwenye hatua ya msingi.
- Hakuna maelezo yaliyo fasaha na mchanganuo kuonesha kiwango cha mchango wa wananchi na hatua iliyochangiwa na fedha za Halmashauri.
- Ujenzi umekoma kwa muda mrefu na hakuna taarifa zozote za gharama zilizokwisha tumika hadi kufikia hatua hiyo na nyumba haina sakafu wala haijapigwa lipu ndani na nje.



*Sehemu moja ya jengo la nyumba ya Mwalimu shule ya Msingi Mwamashimba*

Katika kuhakiki mchakato wa uteuzi wa mkandarasi aliyekabidhiwa mradi huo haukuzingatia uwezo wake kiutendaji, pia hakukuwa na ushirikishwaji wa wadau husika katika miradi yote ya ujenzi wa madarasa, ili kufuatilia maendeleo ya kazi husika. Aidha malipo ya kazi hewa yalitokana na kutokuwa makini kwa Mhandisi wa Ujenzi wakati akiandaa orodha ya vifaa (BOQs)

Hali hii imepelekea utekelezaji duni wa miradi na imeisababishia hasara Halmashauri na walengwa hawakufaidika na thamani halisi ya fedha.

**Mapendekezo**

- Halmashauri ihakikishe miradi yote ambayo haijakamilika, inakamilishwa na mkandarasi katika viwango vinavyokubalika kulingana na mkataba.
- Mkandarasi atozwe tozo la kuchelewa kukamilisha ujenzi hasa katika mradi wa ujenzi wa madarasa matatu katika Shule ya msingi Ipililo, kama ilivyoainishwa kwenye mkataba.
- Watendaji wa Halmashauri katika ngazi zote washirikishwe katika usimamizi na ufuatiliaji wa maendeleo ya utekelezaji wa mkataba au kazi zinazowahusu katika vitengo vyao.

- Mhandisi Bwana Leonard Mashamba na aliyekuwa Afisa Ugavi Bwana Faraja Muredere wawajibishwe kwa kuandaa orodha ya bei na vifaa (BOQ) isiyolingana na kazi halisi.
- Malipo yanayolipwa kwa mkandarasi kwa kazi hewa Sh.14,084,900 yakatwe kutoka kwa Mkandarasi M/s Senga Senga

## 2.11 Mradi wa Uwekezaji Katika Nyanja ya Kilimo (DASIP)

### 2.11.1 Ubadhirifu wa fedha za mradi zenye jumla ya Sh. 200,184,270

Katika kupitia stakabadhi za mapokezi na Taarifa za Benki (Bank Statements) na Vitabu vya Halmashauri (Cash Books) za mwaka wa fedha 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010 Halmashauri ilipokea jumla ya Sh.954,640,280 toka DASIP Makao Makuu Mwanza kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Kilimo na kupokelewa akaunti ya Halmashauri ya DASIP kama inavyooneshwa hapo chini:

| Tarehe | Kiasi kilichopokelewa(Sh.) |
|---|---|
| **2007/2008** | |
| 07/09/2007 | 28,649,994 |
| 17/09/2007 | 40,609,686 |
| 01/10/2007 | 14,889,000 |
| 02/11/2007 | 29,784,000 |
| 22/12/2008 | 81,968,000 |
| 14/04/2008 | 140,000,000 |
| **Sub total** | **335,900,680** |
| **2008/2009** | |
| 29/08/2008 | 24,000,000 |
| 12/09/2008 | 90,000,000 |
| 16/10/2008 | 142,366,000 |
| 10/11/2008 | 10,042,000 |
| 14/11/2008 | 142,366,000 |
| **Sub total** | **408,774,000** |
| **2009/2010** | |
| 19/08/2009 | 90,000,000 |
| 20/08/2009 | 58,365,600 |
| 19/02/2010 | 61,600,000 |
| **Sub total** | **209,965,600** |
| | **954,640,280** |

Katika kupitia nyaraka mbalimbali zikiwemo taarifa za Benki, Hundi zilizolipwa, vibutu vya Hundi, mipango kazi na taarifa za utekelezaji zinazohusu mapato na matumizi ya fedha za mradi wa DASIP, Timu ya ukaguzi iligundua kuwepo ubadhirifu wa jumla ya kiasi cha Sh. 200,184,270 wa fedha za mradi uliofanywa na watumishi wa Halmashauri ambao ni Mtunza fedha na Bw. Walugu Mussa,

Bw. Muhidini Mohamed ambaye ni Mweka Hazina na Watumishi/Mtumishi wa NMB Tawi la Manoga Shinyanga.**Angalia vielelezo R12 - R20.**

**Mapendekezo**

- Halmashauri inatakiwa kufanya taratibu za kuwasiliana na Benki ya NMB Tawi la Manonga kuhakikisha fedha zilizochukuliwa kutokana na uzembe wa Benki zinarejeshwa.
- Mamlaka husika iwachukulie hatua zinazofaa Watumishi waliohusika na upotevu wa fedha jumla ya Sh.200,184,270 na kughushi nyaraka za Benki.

### 2.11.2 Miradi ambayo haikutekelezwa kutokana na ubadhirifu wa fedha Sh.532, 408,600

Jumla ya fedha za miradi 14 yenye thamani ya Sh.532,408,600 kwa mujibu wa mpango kazi haikuweza kutekelezwa kwa kutokana na ubadhirifu wa fedha za mradi, aidha shughuli zilizoathirika na ubadhirifu huo kwa mujibu wa mpango kazi na taarifa za utekelezaji kwa mwaka 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010 zilivyoainishwa ni kama ifuatavyo:

| Na. | Lengo la mradi | Kiasi (Sh) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| | **2007/2008** | | |
| 1 | Ukarabati wa OTC kijiji cha Mwamanota | 14,043,000 | Fedha hazikuhamishiwa akaunti za vijiji |
| | **Jumla ndogo** | **14,043,000** | |
| | **2008/2009** | | |
| 2 | Ujinzi wa lambo kijiji cha Kijongo | 28,000,000 | Fedha hazikuhamishiwa akaunti za vijiji |
| 3 | Uundaji wa vikundi shirikishi180 vya wakulima | 90,000,000 | Fedha hazihuhamishiwa akaunti za vijiji |
| | **Jumla ndogo** | **118,000,000** | |
| | **2009/2010** | | |
| 4 | Uanzishaji wa miradi midogo midogo | 58,365,600 | Fedha hazihuhamishiwa akaunti za vijiji |
| 5 | Mafunzo ya muda mrefu kwa vikundi vya wakulima | 90,000,000 | Fedha hazihuhamishiwa akaunti za vijiji |
| 6 | Ujenzi wa ghala kijiji cha Ngeme. | 28,000,000 | Fedha hazihuhamishiwa akaunti za vijiji |
| 7 | Ujenzi wa lambo kijij cha Bulimba | 28,000,000 | Fedha hazihuhamishiwa akaunti za vijiji |
| 8 | Ujenzi wa lambo kijij cha Mwaweja | 28,000,000 | Fedha hazihuhamishiwa akaunti za vijiji |
| 9 | Ujenzi wa lambo kijij cha Bugoro | 28,000,000 | Fedha hazihuhamishiwa akaunti za vijiji |
| 10 | Ujenzi wa ghala la mazao kijiji cha Mwajiginya B | 28,000,000 | Fedha hazihuhamishiwa akaunti za vijiji |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11 | Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Ikoma | 28,000,000 | Fedha hazihuhamishiwa akaunti za vijiji |
| 12 | Ujenzi wa ghala la mazao kijiji cha Dulisi | 28,000,000 | Fedha hazihuhamishiwa akaunti za vijiji |
| 13 | Ujenzi wa ghala la mazao kijiji cha Mwamishoni | 28,000,000 | Fedha hazihuhamishiwa akaunti za vijiji |
| 14 | Ujenzi wa ghala la mazao kijiji cha Mwamishoni | 28,000,000 | Fedha hazihuhamishiwa akaunti za vijiji |
| | **Jumla ndogo** | **400,365,600** | |
| | **Jumla kuu** | **532,408,600** | |

Hali hii imepelekea kutotekelezwa kwa shughuli na malengo yaliyokusudiwa hasa miradi ya maendeleo katika nyanja mbalimbali kunatokana na ukosefu wa fedha uliotokana na wizi na ubadhilifu.

**Mapendekezo**
Menejimenti ya Halmashauri iimarishe udhibiti wa ndani ili kuhakikisha kuwa fedha zinatumika kwa malengo yaliyoidhinishwa.

### 2.11.3 Ujenzi wa Ghala kijiji cha Kabila

Mnamo tarehe 10/11/2009 Halmashauri ya wilaya kishapu iliingia mkataba na M/s Shilinde Construction Co. Ltd wa S.L.P 124, Meatu, Shinyanga kwa mkataba namba KDC/DASIP/2007/08/C.10 kwa ajili ya ujenzi wa ghala la kuhifadhi chakula. Thamani ya mkataba ilikuwa ni Sh. 34,132,025. Mkataba huu ulianza tarehe 29/09/2008 na ulitegemewa kumalizika tarehe 29/12/2008. Mkandarasi alitakiwa kufanya kazi kulingana na makubaliano na kama ilivyoonekana katika BOQ. **Angalia Kielelezo AJ 63**

Timu ya ukaguzi maalum ilipotembelea katika eneo la mradi ilibaini mapungufu yafuatayo:

- Geti la chuma katika mlango mkubwa halikuoneshwa katika BOQ, ingawa timu ya ukaguzi ilibaini Geti hilo lipo ndani lakini halijafungwa. Hii inaonesha udhaifu mkubwa katika uandaaji wa makisio ya gharama ya mradi (BOQ) ambao hupelekea kufanyika kwa marekebisho (variation) yasiyo na tija. Timu ya ukaguzi ilishindwa kupata gharama halisi ya mlango huo.
- Nguzo moja ya chuma katika kibaraza haijawekwa yenye thamani ya Sh. 30,000 na rangi ya kuta za nje na ndani haijapakwa yenye thamani ya Sh. 1,200,000 na Sh.640,000.
- Chumba cha ofisi ya Ghala hilo hakina nyavu za kwenye madirisha. Gharama hii haikuainishwa katika BOQ hivyo kushindwa kujua gharama halisi. Pia sakafu ina nyufa kabla ya kuanza kutumika. **Angalia Kielelezo AJ 64.**

- Faili la Mkandarasi halina taarifa zozote za malipo yaliyofanywa na Halmashauri kwa mkandarasi. Hii inaonesha kwamba kulikuwa na kila dalili za ucheleweshaji wa malipo.

Picha ya Ghala la kijiji cha Kabila ni kama zinavyoonekana hapa chini:



*Ghala la chakula kijiji cha Kabila*

### 2.11.4 Ujenzi wa Ghala la kuhifadhi chakula kijiji cha Mwigumbi

Mnamo tarehe 22/12/2008 Kamati ya mradi kijiji cha Mwigumbi iliingia mkataba na M/s DGS Co. Ltd wa S.L.P 482 Bariadi, kwa mkataba namba KDC/DASIP/MGUMBI/2007/08/C.10, kwa ajili ya ujenzi wa Ghala la kuhifadhi chakula kijiji cha Mwigumbi. Thamani ya mkataba ulikuwa ni Shs. 34,714,700 mkataba huu ulianza tarehe 22/12/2008 na ulitegemewa kumalizika 22/03/2009. **Angalia Kielelezo AJ 65 na AJ 66**

**Malipo kwa mkandarasi**

Mkandarasi huyu kwa ujumla alilipwa kiasi cha shilingi 33,061,926 kati ya gharama ya mkataba ya shs 34,714,700, kama inavyooneshwa hapa chini:

| Namba ya Cheti cha malipo | Kiasi (Sh.) | Tarehe ya Cheti |
|---|---:|---|
| Na. 01 | 11,341,260 | 9/03/2009 |
| Na. 02 | 14,816,661 | 20/04/2009 |
| Na. 03 | 6,904,005 | 28/05/2010 |
| **Jumla** | **33,061,926** | |

**Angalia Kielelezo AJ, AJ 68 na AJ 69**

- Tofauti ya malipo ya vyeti na kiasi cha mkataba inatokana na utofauti kati ya thamani ya fedha ikilinganishwa na shilingi ya Tanzania na Dola ya Marekani

  Timu ya ukaguzi maalum ilipotembelea katika eneo la mradi ilibaini kuwa Ghala lilikuwa limekamilika lakini halijakabidhiwa na halitumiki.



*Ghala la kuhifadhi chakula katika kijiji cha Mwigumbi*

Kutokabidhiwa na kutotumika kwa ghala hilo ambalo limegharimu fedha nyingi ni kutozingatia thamani ya fedha pia kuwanyima huduma wananchi ambao walilengwa kutumia ghala hilo.

**Mapendekezo ya Ukaguzi**

Halmashauri kupitia Mhandisi wa ujenzi inatakiwa kuhakikisha kwamba Ghala hilo linakabidhiwa na kuanza kutumika ili thamani ya fedha iliyotumika katika ujenzi wa Ghala hilo ipatikane kwa walengwa.

### 2.12 Miradi ya maendeleo ambayo mikataba yake haikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi

Wakati wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo iligundulika kwamba ipo miradi mingi ambayo mikataba yake haikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Hata hivyo wakati wa kutembelea miradi hiyo timu ya ukaguzi ilibaini mapungufu ya wazi katika utekelezaji wa miradi hiyo, baadhi ya miradi iliyotembelewa, ambayo haikuwa na mikataba na mapungufu yake ni kama ilivyoorodheshwa katika **kiambatanisho “K”**

Kutopatikana kwa mikataba hiyo kunatokana na udhaifu katika utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka ndani ya Halmashauri na kutokuwepo kwa mgawanyo wa

kazi katika Halmashauri na msisitizo unaoelekeza na kutoa majukumu ya utunzaji mikataba ya wakandarasi inayotekelezwa katika idara mbalimbali za Halmashauri hali hii imepelekea tathmini ya utekelezwaji wa miradi husika kutofanyika wakati wa ukaguzi.

**Mapendekezo**
Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuhakikisha mikataba inapatikana na kuwepo utaratibu wa kuhifadhi mikataba hiyo katika hali ya usalama.

Ndugu Medson Matarana ambaye ni Afisa Ugavi na Mhandisi wa Ujenzi Bwana Leonard Mashamba wawajibishwe kwa kukosekana kwa mikataba husika.

## 2.13 MIRADI YA RUZUKU YA MAENDELEO

### 2.13.1 Malipo yenye shaka kwa Mkandarasi Shs. 21,445,559.35

Halmashauri ya wilaya Kishapu kwa kushindwa kufanya usimamizi mzuri wa mikataba kwa kipindi cha 2007/2008 ililipa kiasi cha Sh. 21,445,559.35 ikiwa ni malipo yenye shaka kwa mkandarasi kama inavyoonekana katika vipengele (i) hadi (iii) kama ifuatavyo:

(i) Halmashauri iliingia mkataba na M/s Gold Star & Co Ltd kwa mkataba Na. KDC/R.40/3/2007/08/C.11 wa tarehe 22/02/2008 kwa ujenzi wa nyumba ya Mtumishi - awamu ya pili kwa Sh.24, 052,150. **Angalia kielelezo AK1**

Katika kupitia utaratibu wa manunuzi na usimamizi wa mikataba ilibainika mkandarasi aliomba kulipwa kiasi cha Sh.2,000,000 kwa barua yenye kumbukumbu Na.GSL/058/2009 ya tarehe 31/8/2009, ikiwa ni tofauti ya kile kilichoandikwa katika mkataba uliosianiwa na orodha ya gharama ya kazi (BOQs) Sh.26,052,150 ikieleza kulikuwepo na makosa ya kihesabu yaliyopelekea tofauti hiyo na hatimaye kuandikwa kwenye mkataba huo. **Angalia keilelezo AK1, AK2 na AK3.**

Aidha, ukaguzi huu uligundua kwamba marekebisho hayo hayakupelekwa katika Bodi ya Zabuni kuidhinishwa kinyume na Kanuni Namba ya 18 (b) ya Kanuni za Bodi ya Zabuni ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa (GN 177)ya mwaka 2007.

(ii) Pia ilibainika kwamba katika malipo yaliyotolewa katika cheti Na 01 ya tarehe 25/3/2008, fedha za matazamio (retention money) ya asilimia 5% ya Sh.11,812,935 sawa na Sh. 590,646.85 hazikukatwa kinyume na kifungu 51.1 cha mkataba. **Angalia kielelezo AK4.**

(iii) Vile vile ilibainika kwamba thamani ya kazi iliyokubaliwa katika mkataba uliofungwa awali ilikuwa shs. 24,052,150 na baadaye kulitokea ongezeko la kazi (variation) kiasi cha sh. 13,615,735 bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni

kinyume na Kanuni Na. 18 (b) ya Kanuni za Bodi ya Zabuni ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ( GN 177) ya mwaka 2007.

Katika kupitia vyeti vya malipo ilibainika Mkandarasi alilipwa Sh.5,239,177.50 zaidi ya alivyostahili kama ilivyooneshwa hapa chini:

| Na. | Cheti cha malipo Na. | Kiasi halisi kilicholipwa (Tshs) | Kiasi kilicholipwa kama malipo ya matazamio (Retention) Tshs |
|---|---|---|---|
| 1. | 01 | 11,812,937.00 | NIL |
| 2. | 02 | 6,130,350.00 | 322,650.00 |
| 3. | 03 | 12,709,418.25 | 668,916.75 |
| 4. | 04 | 2,622,000.00 | 138,000.00 |
| 5. | 05 | 931,000.00 | 49,000.00 |
| 6. | Mwisho | 7,522,790.50 | NILL |
| **Jumla ndogo** | | **41,728,495.75** | **1,178,566.75** |
| **Jumla kuu (Malipo halisi + Retention) (B)** | | **42,907,062.50** | |
| **Jumla ya gharama kazi zote (C)** | | **37,667,885.00** | |
| **Kiasi kilichozidi (B)-(C)** | | **5,239,177.50** | |

**Angalia vielelezo AK5 - AK10**

### 2.13.2 Ujenzi wa Nyumba ya Watumishi " Two in one" ( Head - Quarter)

Halmashauri iliingia mkataba namba LGA.108/STF-HSES/2010-2011/DEV/02/TYP-C na Mkandarasi M/s Michadec Co.Ltd tarehe 27/10/2010 kwa makubaliano ya awali ya kufanya kazi hiyo kwa jumla ya Shs 53,360,882.00, kwa muda wa siku 90. Mkandarasi alitakiwa kuanza kazi tarehe 3/11/2010 na kumaliza kazi tarehe 2/2/2011, **Angalia kielelezo AL1.**
Katika vyeti vya malipo, jumla ya Sh. 51, 319,791 sawa na 96% ya malipo yote tayari yamefanyika kama inavyoonekana katika cheti cha malipo namba 4 **Angalia kielelezo AL2.**

**Mapungufu katika utekelezaji**
Mradi huu bado haujakamilika japokuwa sehemu kubwa ya malipo imefanyika, mapungufu yaliyojitokeza katika usimamizi wa mradi huu ni kama ifuatavyo:

- Kazi ya kuweka milango, madirisha, pamoja na vitasa vya milango hiyo havina ubora, mbao zilizotumika kutengeneza milango miwili ya ndani ya nyumba zilikuwa zina matundu na makovu mengi kiasi cha kutofaa kwa kazi hiyo.

- Vitasa na komeo vilivyowekwa katika madirisha na milango havikuwa na ubora pia vilikuwa ni vya aina tofauti ya vile vilivyohitajika katika B.O.Q kwa mfano,

mkandarasi hakuweka vitasa vya milango aina ya ‘Three lever mortice lock’ baadhi ya vitasa hivyo vilikuwa tayari vimeanza kuharibika kabla ya jengo kukamilika, hata hivyo cheti cha malipo namba 04 kinaonyesha jumla ya shs. 1,300,000 kulipwa kwa ajili ya kazi hiyo. **Angalia vielelezo AL 3**.

- Katika ukaguzi wa kazi ya kuweka “6mm thick tinted glass” haikuwemo kwenye BOQ, lakini malipo ya jumla ya shs.109, 440 yaliandaliwa katika cheti cha malipo namba 04 kwa kazi hiyo. **Angali vielelezo AL3**
- Door closer (shs.80, 000), “38mm rubber door stopper” (shs.40, 000), kazi hizo hazijafanyika japo malipo yaliandaliwa.
- Katika cheti namba 04 Malipo ya Kazi ya electrical installation yenye thamani ya shs.2, 500,000 yaliandaliwa pamoja na kazi hiyo kutokamilika. Hata hivyo kazi hiyo inaonekana kulipwa mara mbili, katika cheti cha malipo namba 03 Sh. 1,000,000 zililipwa katika kazi hii, hivyo hata kama kazi hiyo ingekuwa imekamilika Sh. 1,000,000 zingekuwa zimelipwa zaidi ya stahili na hapakuwa na nyaraka yeyote ya kuongezeka kwa thamani ya kazi hiyo. **Angalia vielelezo. AL4,AL 5 na AL 6**
- Pamoja na kuwa kazi ilikuwa bado haijakamilika mkandarasi hakuwepo katika eneo la kazi.
- Hapakuwa na taarifa ya ukaguzi wa mwisho kufanyika kabla ya malipo ya mwisho kufanyika.





**Moja ya** *vitasa aina ya “2lever lock” kilichowekwa badala ya aina ya 3lever lock*



*Sehemu ya kazi ya umeme ambayo haijakamilika lakini malipo kufanyika Sh.1, 000,000*

### 2.13.3 Ujenzi wa Nyumba ya Watumishi "Two in one" (Head - Quarter)

Halmashauri iliingia mkataba na kampuni ya Mwifumbo Investment Co.ltd kwa mkataba wenye Kumb namba LGA/108/STF-HSES/2010-2011/DEV/02/TYP-D wa tarehe 27/10/2010 kwa makubaliano ya Sh.50, 682,225. Mkandarasi alitakiwa kuanza kazi tarehe 3/11/2010 na kumaliza kazi tarehe 2/2/2011 sawa na siku tisini (90), **Angalia kielelezo AM1.**

Katika utekelezaji wa mradi huu kulikuwa na ongezeko la kazi lililopitishwa na bodi ya zabuni la jumla ya shs. 8, 046,820 hivyo thamani ya mkataba ilibadilika na kuwa Sh. 58,729,045. **Angalia kielelezo na AM2.**
Hata hivyo kulikuwa na ongezeko jingine la kazi ya kuweka milango mitatu yenye thamani ya shs. 936, 000 ambapo hakuna uthibitisho Kama ongezeko hilo lilipitishwa na bodi ya zabuni. **Angalia kielelezo na AM3.**

Cheti cha malipo ya mwisho ya mkataba huo ni jumla ya shs.58, 729,045 kiliandaliwa na kupitishwa tarehe 15/04/2011, **Angalia kielelzo na. AM4**

**Mapungufu**

Mradi huu tayari umekabidhiwa na upo katika kipindi cha matazamio, hata hivyo ukaguzi ulibaini kuwapo kwa mapungufu mbalimbali katika kazi iliyokabidhiwa kama ifuatavyo:

- Sakafu ya sehemu ya nyuma ya jengo (court yard) ilikuwa inapukutika hii ikiashiria kutokuwapo kwa uwiano mzuri kati ya mchanga na simenti wakati wa ufanyaji wa kazi hii.

- Ongezeko la kazi hizi linaonekana dhahiri kuwa ni kutokana na Uzembe au kutokuwa makini wakati wa uandaji wa makadirio, mfano wa kazi ya kuweka dari “ceiling board” katika jengo zima na milango mitatu kusahaulika.
- Hapakuwa na taarifa ya ukaguzi wa mwisho kufanyika kabla ya malipo ya mwisho kufanyika.



**Sakafu katika sehemu ya nyumba ambayo haikuwa na ubora**

### 2.13.4 Ujenzi wa Nyumba ya Watumishi “Two in one” (Head - Quarter)

Halmashauri iliingia mkataba na M/s Plenimar Inv. & Mutyama Inv.Co.Ltd kwa mkataba Na.LGA.108/STF-HSES/2010/11/DEV/02/TYP-E wa tarehe 27/10/2010 wa jumla ya Sh. 50,682,225 kwa ajili ya ujenzi Nyumba ya Watumishi “Two in one” (Head - Quarter). Mradi ulitakiwa kuanza tarehe 3/11/2010 na kukamilika tarehe 2/03/2011 zikiwa ni siku 90 toka tarehe ya kuanza kazi, **Angalia kielelezo na AN1.**

Katika utekelezaji wa mradi huu kulikuwa na ongezeko la kazi la jumla ya Sh. 11,564,350, kazi ya ujenzi wa “septic” na “soakawaypit” iliyogharimu jumla ya Sh. 6,120,750 ilifanyika ikiwa ni sehemu ya kazi zilizoongeka, hata hivyo hapakuwa na nyaraka zozote zilizopitishwa na bodi ya zabuni za kupitisha ongezeko hilo la kazi. **Angalia kielelezo na. AN2.**

**Mapungufu**
Mradi huu bado haujakamilika japokuwa sehemu kubwa (shs.43, 138,660) ya malipo imefanyika kama inavyoonekana katika cheti cha malipo na. 3, **Angalia kielelezo na. AN3.**

Mapungufu yaliyojitokeza katika usimamizi wa mradi huu ni pamoja na;

- Ongezeko la kazi hizi linaonekana kuwa ni kutokana na Uzembe wakati wa uandaji wa makadirio, mfano kwa kawaida nyumba huwa na choo pamoja na mashimo ya maji machafu lakini katika mradi huu mashimo ya maji machafu yalisahaulika.
- Katika cheti cha malipo namba 03 cha tarehe 27/04/2011 jumla ya sh 4,704,500 zililipwa kwa kazi nzima ya kuweka madirisha na milango, hata hivyo hali halisi ni kuwa kazi hii haijakamilika na kilichofanyika ni kuweka "frame" za milango na madirisha. **Angalia kielelezo na AN4**
- Kutokuwepo kwa mkandarasi katika eneo la kazi, japokuwa kazi bado haijakamilika.



*Nyumba ya watumishi (walimu) ambayo bado haijakamilika*

### 2.13.5 Ujenzi wa Nyumba ya Watumishi Grade one "staff Quarter House phase II"

Halmashauri wa Wilaya ya Kishapu iliingia mkataba namba Na.KDC/R.40/3/2007/08/C.11 tarehe 22/02/2008 na Mkandarasi M/s Gold – Star & Company Ltd wenye thamani ya Sh. 26,052,150. Mkandarasi alitakiwa kuanza kazi tarehe 29/2/2008 na kumaliza tarehe 22/5/2008 sawa na siku 84. **Angalia kielelezo na AP1**

Katika utekelezaji wa mradi huu kulikuwa na ongezeko la kazi la Sh.12, 765,735 na kufanya thamani mpya ya mradi kuwa Sh. 38,817,885.20.Timu ya ukaguzi maalumu ilibaini kuwa katika utekelezaji wa Mkataba mkandarasi alilipwa jumla ya Sh.2,907,063.50 kama ifuatavyo:

| Cheti cha Malipo | Kiasi (Sh.) |
|---|---:|
| Cheti na. 1 | 11,812,937.00 |
| Cheti na. 2 | 6,453,000.00 |
| Cheti na. 3 | 13,378,335.00 |
| Cheti na. 4 | 2,760,000.00 |
| Cheti na. 5 | 980,000.00 |
| Cheti cha Mwisho | 7,522,791.50 |
| **Jumla ya Malipo** | **42,907,063.50** |

**Angalia kielelezo na AP2**

Aidha ukaguzi umebaini kuwa Mkandarasi amelipwa zaidi ya bei iliyo katika mkataba kwa Sh.4, 089,178.30 (42,907,063.50 - 38,817,885.20).

**Mapungufu**

Mkandarasi alifanya kazi ya kuweka mfumo wa maji “plumbing” ambao haukujaribiwa kama umewekwa vizuri, kitu kilichopelekea mfumo huo kuwa unavuja baada ya maji kuingizwa katika nyumba hiyo. Gharama za kurekebisha mfumo huo wa maji zilifanywa na Halmashauri.

Kinyume na kanuni Na. 44 ya Kanuni ya Sheria na Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005, Halmashauri ilishindwa kuwasilisha Muhatasari wa kikao cha zabuni kilichopitisha ongezeko la kazi la Sh.12, 765,735.

Katika malipo ya cheti (certificate) namba nne ya Sh.931, 000 mkandarasi alilipwa fedha kwa ajili ya kwenda kununua vifaa vya kazi, huu si utaratibu wa kazi kwani kwa kawaida mkandarasi hulipwa kwa kazi aliyofanya na si kupewa fedha ya kwenda kununua vifaa. **Angalia kielelezo na. AP3**

Katika sehemu za bafuni na choo (wet areas) maelekezo yalikuwa ni kuweka milango 6 aina ya “flush doors” lakini ukaguzi maalum ulibaini kuwa milango iliyowekwa ilikuwa ni aina ya “panel door” na hapakuwa na maelezo yeyote ya kubadili kazi hiyo. **Angalia kielelezo na AP4**

Katika malipo ya kwanza ya cheti (Certificate) Na. 1 ya Sh. 11,812,937 mkandarasi hakukatwa fedha ya matazamio ya kazi ‘retention money’. **Rejea kielelezo AP2**

### 2.13.6 Ukamilishaji wa Nyumba ya Mtumishi “Staff House Grade II

Halmashauri iliingia mkataba namba Na.LGA/108/STF-HSES/2010-2011/DEV/02/GRD II tarehe 27/10/2010 na Mkandarasi M/s KAL –HOLDING CO.LTD wenye thamani ya Sh. 35,984,160. Mkataba huu ulikuwa ni wa awamu ya tatu ambapo mkandarasi alitakiwa kumalizia kazi iliyobakia na kuacha kazi ya uwekaji wa shutter za milango na madirisha. Mkandarasi alitakiwa

kufanya/kumalizia ujenzi wa nyumba mbili zinazofuatana kwa gharama ya shilingi 17,991,080 kwa kila moja. Kazi ilitakiwa kuanza tarehe 3/11/2010 na kumalizika tarehe 2/2/2011. **Angalia kielelezo na. AQ1 na. AQ2**

**Mapungufu katika utekelezaji**
Ukaguzi maalumu ulibaini kuwa pamoja na malipo ya mkataba wote kufanyika na kuandaliwa tangu tarehe 13/03/2011 matengenezo ya nyumba mojawapo yalikuwa bado hayajakamilika kama ifuatavyo:

- Uwekaji wa vigae katika kuta za vyoo ulikuwa haujakamilika, msimamizi wa mradi huu alieleza kuwa marekebisho hayo yatafanywa katika kipindi cha muda wa matazamio. Mtazamo huo wa msimamizi wa kazi kutoka Halmashauri haukuwa sahihi kutokana na kuwa kazi ambazo hufanyika katika kipindi hiki huwa ni za marekebisho ya kazi zilizofanyika na sio kufanya kazi ya kumalizia matengenezo.

- Mkandarasi alikuwa hajamaliza kupaka rangi katika nyumba mojawapo hasa katika sehemu ya chini ya kuta. **Angalia kielelezo AQ2**




*Kazi ya kuweka vigae katika vyoo ambayo haijakamilika lakini imetayarishiwa malipo/imelipwa*

### 2.13.7 Umaliziaji wa Nyumba ya Mtumishi

Halmashauri iliingia mkataba namba Na.LGA/108/STF-HSES/2010-2011/DEV/02/TYP-B tarehe 27/10/2010 na Mkandarasi M/s KAL –HOLDING CO.LTD wenye thamani ya Sh. 48,755,345 wa muda wa siku 90 kwa ajili ya mradi wa "Construction of Grade one staff Quarter House". Mkandarasi alitakiwa

kuanza kazi tarehe 3/11/2010 na kumaliza tarehe 1/2/2011, **Angalia kielelezo na. AR1**

**Mapungufu katika utekelezaji**
Ukaguzi maalumu ulibaini kuwa pamoja na malipo ya mkataba wote kufanyika na kuandaliwa tangu tarehe 2/05/2011 kama kinavyoonyesha cheti cha malipo ya mwisho, matengenezo ya nyumba hiyo yalikuwa hayajakamilika. Kazi za kuweka Milango, Madirisha, sinki zilikuwa zimefanywa bila kukamilika, mfano baadhi ya madirisha hayana vioo kama inavyoonekana katika picha hapa chini: **Angalia kielelezo AR2.**

**Kazi ya kuweka madirisha na sinki la maji ya kunawia, ikiwa ni moja kati ya kazi ambazo hazijamalizika.**

### 2.13.8. Ujenzi wa Jengo la Utawala (Administration block)

Halmashauri iliingia Mkataba namba LGA/108/2008/09/ADMNBLK/C.01 tarehe 27/1/2009. Mradi huu ulitekelezwa katika kipindi cha awamu nne, katika vipindi vyote mradi huu ulifanywa na mkandarasi Nela Construction ltd akisimamiwa na Mjenzi mshauri-Wakala wa Majengo wa Mkoa wa Shinyanga (TBA) pamoja na Halmashauri katika vipindi tofauti**. Angalia kielelezo na AT1**
Mkandarasi alitakiwa kuanza kazi tarehe 3/2/2009 na kumaliza kazi tarehe 3/11/2009.

| Awamu | Aina ya kazi | Gharama ya awali ya mkataba (Sh.) |
|---|---|---|
| I | Construction of substructure (Supervised by TBA) | 159, 049,750 |
| II | Concrete frame and stairs (Supervised by TBA) | 399,109,145 |
| III | Walling, Roofing, Plumbing, Finishing (Supervised by TBA) | 388,422,300 |
| IV | Painting, Electrical installation (Supervised | 329,021,220 |

| | | |
|---|---|---|
| | by District council) | |
| Ujenzi wa Choo cha nje | External toilet (Supervised by District council) | 23,536,010 |
| Jumla ya fedha iliyotumika | | **1,140,088,675** |

**Mapungufu;**
Katika utekelezaji wa mradi wa awamu ya tatu kazi ambayo haikuonekana katika jengo lakini ililipwa ni kazi ya "Roof drainage" inayogharimu kiasi cha Sh.2, 711,200. Kazi hii ilionekana kulipwa katika cheti namba nne. **Angalia kielelezo na. AT2**

Pia katika awamu ya tatu mchakato wa manunuzi hasa katika hatua ya kutangazwa haukuwa wa uwazi. Kazi ilitangazwa katika mbao za matangazo "notice boards" za Halmashauri ya Shinyanga na Mwanza pekee. Kitu kilichopelekea wakandarasi watatu pekee kuwasilisha Zabuni, ambapo wawili walikuwa ni daraja la tano na zaidi huku mkandarasi Nela Co.Ltd akibaki bila ushindani. Hii ni kinyume na Kanuni namba 80(5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (GN 97) ya mwaka 2005 inavyoelekeza kuwa tangazo kama hilo lilitakiwa kutolewa katika gazeti.



**Uonekano wa mbele wa jengo la Halmashauri lililojengwa kwa awamu nne**

Mapungufu na kasoro zilizobainika zimesababishwa na Usimamizi dhaifu wa wataalamu wa Halmashauri kutoka katika Idara ya ujenzi uliosababisha kufanyika kwa kazi zisizo na ubora hivyo kusababisha Halmashauri kumlipa mkandarasi fedha zaidi ya kazi iliyofanyika na kutozingatiwa kwa sheria, taratibu na kanuni za utendaji kazi hasa wakati wa malipo ya kazi iliyofanyika.

**Mapendekezo**

- Mkandarasi afanye marekebisho kwa kazi zote ambazo hazina ubora pamoja na Kubadilisha vifaa vyote ambavyo viliwekwa tofauti na maelekezo ya B.O.Q.

- Mhandisi wa Ujenzi Bwana Leonard Mashamba achukuliwe hatua stahiki kwa kutosimamia ipasavyo mradi huu na uzembe uliosababisha malipo ya ziada ya Sh.6, 800,278.30. Pia na kiasi hiki kirejeshwe na Wakandarasi waliolipwa zaidi.

### 2.14 Mapungufu ya nyaraka na udhaifu katika usimamizi wa mikataba na miradi yenye jumla ya Sh.4,258,312,634

Katika mafaili ya miradi ambayo ilichaguliwa kwa ajili ya uhakiki yenye thamani ya Sh.4,258,312,634 yalibainika kuwa na mapungufu ya nyaraka muhimu hivyo kuzuia ukaguzi kupata taarifa na takwimu muhimu zinazohusu miradi, katika maeneo ya usimamizi wa miradi na mikataba, usahihi wa malipo kwa wakandarasi na uhalali wa malipo ya ongezeko la gharama za bei za mikataba kulitokana na kutokuwemo kwa nyaraka na mapungufu mbalimbali katika mafaili husika kama vile tarehe za kuanza na kumaliza kazi za mikataba, baadhi ya vyeti vya kuidhinisha malipo (Payment Certificates) na taarifa za tathimini ya wazabuni walioomba Tenda.

Pia kukosekana kwa uthibitisho wa idhini ya ongezeko la bei (Variations) ya mikataba, maelekezo na michanganuo ya kazi za ziada (site instructions and variation orders) na taarifa za mapitio ya maendeleo ya kazi za mkataba (work evaluation reports).

Vile vile kutokuwatoza wakandarasi adhabu ya uchelewaji wa kumaliza kazi kwa wakati ambayo ni kinyume na Kanuni Na.119 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2005, kutokuwa na dhamana kwa malipo ya awali, kutokuwepo kwa mihutasari ya vikao katika eneo la ujenzi (site meetings) na vyeti vya kumaliza kazi (Certificate of completion). Kwa ujumla hali hii inaonesha udhaifu wa Uongozi wa Halmashauri katika kusimamia miradi ya maendeleo na mapungufu ya usimamizi wa rasilimali za umma. Pia, kutowajibika kwa vitengo vya Uhasibu, Idara ya Ujenzi, Masijala na Uongozi wa Halmashauri kwa ujumla, hali hii inapelekea miradi kutokamilika kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa na pia kuwepo kwa ongezeko la bei katika mikataba na kuisababishia Halmashauri hasara na wakandarasi kulipwa zaidi ya bei ya mkataba.

**Mapendekezo**

- Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuhahakikisha kuwa mafaili ya miradi yanakuwa kamili kwa kuwa na nyaraka zote zinazohusiana na miradi hiyo, pia Halmashauri inatakiwa kuhakikisha kuwa nyaraka zote zilizokosekana katika mafaili husika ya miradi iliyoainishwa kwenye kiambatanisho zinapatikana na kuwasilishwa ukaguzi kwa uhakiki.

- Kuhakikisha kuwa kazi zote za ziada zinaidhinishwa na Bodi ya Zabuni kabla ya kulipwa.

## 2.15 Mapungufu baada ya kukagua hati za malipo zilizopatikana

### 2.15.1 Orodha ya Watumishi waliolipwa gharama za uhamisho haikutolewa Sh.16,384,915

Kiasi cha Sh.16,384,915 kililipwa kutoka akaunti ya General Fund kama gharama za uhamisho kwa watumishi waliohama kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kuja kuanzisha Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu Mwezi Julai, 2006 kwa hati ya malipo Na.8/12/2009, hundi Na.183470 ya tarehe 4/12/2009 na ililipwa kwa Mkurugenzi Mtendaji – Kishapu kupitia akaunti ya Mfuko mkuu ( General Fund )

Timu ya ukaguzi ilifuatilia kupata orodha ya watumishi kutoka kwa Afisa Utumishi na kitengo cha uhasibu bila mafanikio na orodha hiyo haikutolewa ili kuhakiki uhalali wa malipo hayo. Kwa kutopatikana kwa viambatanisho husika pamoja na hati za malipo kunapelekea kutothibitisha uhalali wa malipo hayo ambayo ni kinyume na Agizo Na. 5 (c) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997. **Angalia kielelezo AH1**

**Mapendekezo**

Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuhakikisha Mweka Hazina wa Halmashauri anahusika na usimamizi wa nyaraka hizi muhimu kama ilivyo katika Agizo Na.5 (c) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1997.

### 2.15.2 Malipo ya Fidia yenye Mashaka Sh.12, 050,000.

Kiasi cha Sh. 12,050,000 kililipwa kwa hati ya malipo Na. 24/3/2010 na hundi Na.103773 ya tarehe 12.3.2010 kama fidia kwa wamiliki wa eneo ambalo limetwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda katika akaunti ya Ardhi. Katika kupitia orodha ya malipo hakukuwa na uthibitisho wa Mtendaji wa Kijiji kuthibitisha utambuzi wa wafidiwa halali. Kumekuwepo na udhaifu wa kufuata taratibu za ulipaji wa fidia hivyo kufanya kuwepo kwa uwezekano mkubwa wa kulipwa walipwaji hewa na kuiletea Halmashauri hasara ya kufanya malipo yasiyo na tija. **Angalia kielelzo AH2 na AH3.**

**Mapendekezo**

Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuhakikisha kuwa aliyehusika na kutopatikana kwa nyaraka husika anachukuliwa hatua stahiki. Pia Halmashauri iimarishe utunzaji wa nyaraka zote.

## 2.16 Hati za Malipo ambazo hazikuidhinishwa Sh.221, 805,777

Katika kupitia hati za malipo za mwaka 2009/2010, ilibainika kwamba hati za malipo zenye thamani ya Sh. 221,805,777.43 hazikuidhinishwa na Mkurugenzi ambaye kwa mujibu wa kifungu Na. 33 cha Sheria ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 yeye ndiye Afisa Masuuli ambapo malipo yote yanatakiwa yaidhinishwe kama inavyooneshwa katika **kiambatanisho "L". Angalia kielelezo AF1 - AF20.**

Wakati wa kupitia mfumo wa udhibiti wa ndani, kufanya mahojiano na Mkurugenzi wa Halmashauri, Mweka Hazina ilifahamisha kuwa akaunti ya TASAF inawaweka saini watatu kwa maana ya Mkurugenzi, Mratibu wa TASAF na Mhasibu wa TASAF. Hundi husainiwa na maafisa wawili kati ya watia saini hawa na maombi ya malipo yanatakiwa kuidhinishwa na Mkuu wa idara, Mweka Hazina pamoja na Mkurugenzi . Kisha hati ya malipo kuandaliwa na Mhasibu ambayo inatakiwa pia kusainiwa na Mkuu wa Idara, Mweka Hazina kisha Mkurugenzi.

Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2009 aliyekuwa Mhasibu wa TASAF kwa kipindi hicho Bwana H. Makokola hakusimamia vizuri utaratibu wa uidhinishaji hivyo hati hizo za malipo hazikuwa zimesainiwa na Mkurugenzi. Hayo yote yametokea kwa sababu ya ukosefu wa umakini katika kuzingatia taratibu za uombaji, uandaaji na uidhinishaji wa malipo. **Angalia kielelezo AG**

**Mapendekezo**
Watendaji wa Halmashauri wanatakiwa kuwa makini katika kufuata taratibu za uombaji, uandaaji na uidhinishaji wa malipo.

## 2.17 Kitengo cha Usafiri na Usafirishaji:

### 2.17.1. Kutokuwepo ufuatiliaji wa mwenendo wa Mafuta.

Timu ya ukaguzi iligundua kuwa Halmashauri haitumii ipasavyo kitengo cha Usafirishaji kwani Afisa Usafirishaji aliyepo hakupewa majukumu ya kufuatilia mwenendo wa matumizi ya Mafuta.

Kwa mujibu wa Agizo Na. 331 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mtaa ya mwaka 1997, Afisa Usafirishaji anapaswa kuratibu mwenendo wa vyombo vya usafiri na matengenezo yake ikiwemo matumizi ya mafuta kwa vyombo husika.

Hii ilithibitika baada ya kufanya Mahojiano na Bi. Eliza (Afisa Usafirishaji) pamoja na anayekaimu nafasi ya kitengo cha Manunuzi Bwana Medson Matarana juu ya utendaji wa kitengo cha usafirishaji na manunuzi katika mwenendo wa matumizi ya mafuta.

Kutokuwepo kwa udhibiti wa mafuta kunatokana na kutoshirkishwa kwa Afisa Usafirishaji na kutoainishwa kwa majukumu ya utendaji kazi kufuatilia mwenendo wa mafuta katika majukumu ya Afisa Usafirishaji.hivyo kuwepo uwezekano wa mafuta kutumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa.

**Mapendekezo**
Halmashauri imtumie ipasavyo Afisa Usafirishaji kwa kumpa jukumu la kufuatilia mwenendo wa matumizi ya mafuta sanjari na mwenendo mzima wa wa matumizi ya magari na ikiwa pamoja na kuratibu matengezenezo ya magari hayo.

### 2.17.2 Mafuta ambayo hayakuthibitika Matumizi yake Sh.42,180,300

Katika kupitia leja za mafuta kwa Mwaka 2008/2009 na 2009/2010 ukaguzi ulibaini kuwepo kwa salio la mafuta yenye jumla ya sh. 42,180,300.00 kama inavyoonesha hapa chini:

| Aina ya Mafuta | Lita | @ | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---:|
| Diesel | 21721 | 1800 | 39,097,800 |
| Petrol | 1712.5 | 1800 | 3,082,500 |
| **Jumla** | | | **42,180,300** |

**Angalia kielelezo AW na kiambatanisho “M”**

Matumizi ya Mafuta hayo hayakuweza kuthibitishwa kama yamekwishatumika kwani leja zinaonesha salio lakini hali halisi ni kuwa mafuta hayo hayapo. Hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa mafuta kutokana na kutoshirikishwa kwa Afisa Usafirishaji na kutoainishwa kwa majukumu ya utendaji kazi.

**Mapendekezo**

Afisa usafirishaji asimamie matumizi ya Mafuta. Pia Maafisa waliokuwepo kwa vipindi tofauti katika kitengo cha Ugavi Bwana Faraja Muredere, Bwana Elias Simiyu na Bwana Medson Matarana wachukuliwe hatua stahiki kwa kutotoa hesabu (Accountability) ya Mafuta yenye thamani ya sh. 42,180,300.

**SURA YA TATU**

## 3.1 KIINI CHA TATIZO

- Idara mbalimbali kuongozwa na wafanyakazi ambao walitoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, ambao aidha walikabidhiwa majukumu makubwa kuliko yale waliyokuwa nayo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga au hawakuwa na sifa stahiki za kuongoza idara walizokabidhiwa.
- Mabadiliko ya uongozi ya mara kwa mara katika vipindi vifupi. Pamoja na kuwa Halmashauri ilikuwa mpya, mabadiliko haya hayakuwawezesha wale waliokuwa na nyadhifa mbalimbali katika Halmashauri, kujenga mfumo wa kudumu na imara wa udhibiti wa ndani na kuhakikisha unaendelezwa, kwa sababu ya kutokuwepo kwa kipindi kirefu. Kutokana na kuhamahama kila mara, viongozi wengi wa idara hawakuweza kujenga mfumo thabiti wa jinsi ya kutekeleza majukumu yao kwa mtazamo endelevu.
- Kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya uongozi, nafasi nyingi za uongozi wa Idara zilikuwa zinakaimiwa kwa vipindi virefu. Waliokaimishwa mara nyingi walitekeleza majukumu yao kwa malengo na mtazamo wa muda mfupi, ambao haukuwezesha kuwepo kwa mfumo imara wa udhibiti wa ndani.
- Katika hali isiyo ya kawaida Mtunza fedha (Cashier) Ndugu Walumu Musa Limbe alitambulishwa kwa Meneja wa Benki na kuidhinishwa kwa barua isiyo na Kumb. namba ya tarehe 20/07/2005 iliyoandikwa na Mkurugenzi Mtendaji kwenda kwa Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Manonga, iliyompa mamlaka ya kushughulikia masuala yote yanayohusu fedha katika akaunti za benki.

  Kwa idhini hiyo, aliweza kufanya kazi za kuweka na kutoa fedha katika Benki kwa wakati wowote bila kizuizi na alitumia mwanya huo kuchota fedha za Halmashauri kwa kushirikiana na watumishi wengine pamoja na watumishi wa Benki.

- Mapungufu na udhaifu wa udhibiti wa ndani na kutokuwepo kwa mfumo Funganishi wa usimamizi wa Fedha- IFMS na kutokuwepo kwa mgawanyo wa kazi za wahasibu unaokidhi uwiano wa mgawanyo wa majukumu yanayomfanya mhasibu mmoja asiwe na kazi za mwendelezo zinazoweza kumpa nafasi ya kufanya ubadhirifu bila kugundulika.

- Uhamishaji wa fedha usio na idhini wala kibali cha Mkurugenzi wa Halmashauri ambapo mfumo uliwafanya wahusika kufanya wizi wa fedha hizo bila kizuizi chochote kwa kushirikiana na watumishi/mtumishi wa Benki ya NMB tawi la Manonga.

- Halmashuri kutofanya usuluhisho wa benki wa mara kwa mara na kubaini kiasi cha mapokezi ya fedha ambayo hayakupelekwa benki.

SURA YA NNE

# 4.0 MAFUNZO KUTOKANA NA HALI ILIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI HUU MAALUMU

## 4.1 Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Kama ilivyoainishwa katika sura zilizopita imedhihirika ya kuwa kuna udhaifu mkubwa katika Uongozi wa Halmashauri juu ya Uwekaji na Usimamiaji wa Mfumo thabiti wa Udhibiti wa Ndani (Internal Control System). Hali hii imepelekea hadi watu wawili kushirikiana na kukamilisha miamala (transactions) ya kibadhirifu bila kutambuliwa na mfumo uliokuwepo kwa njia mbalimbali zikiwemo kufanya malipo bila hati za malipo wala Hundi.

Mweka Hazina ndiye mwenye majukumu ya kuhakikisha anasimamia mwenendo wa Fedha za Halmashauri na udhibiti wake pamoja na kusimamia kitengo cha Fedha. Hali ambayo imekuwa tofauti kabisa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ambapo Mweka Hazina Bw. Muhidin Mohamed alikosa uaminifu kwa kuwa mstari wa mbele kwa kushirikiana na baadhi ya watumishi kuchukua fedha za Halmashauri kinyume na utaratibu.

Aidha Mfumo wa orodha ya Hundi (cheques list) haukuwepo hapo awali na kupelekea baadhi ya Hundi kuongezewa kiasi zaidi ya kile kilichoandikwa katika uso wa Hundi hizo.

Udhaifu huu wa Mfumo wa Udhibiti wa Ndani uliwezesha kufichwa kwa ukweli "deception/misrepresentation" wa hali halisi ya mwenendo wa taarifa za Benki katika akaunti mbalimbali. Hali ambayo iliwafanya wakuu wa Idara kutumia taarifa hizo za Benki ambazo zilighushiwa. Hali hii inaonesha kuwa mkazo wa ufuatiliaji wa Taarifa za Benki (Bank Confirmation) pamoja na ufanyikaji wa usuluhishi wa Benki (Bank Reconciliations) kuwa ni maeneo ambayo yanatakiwa kuangaliwa kwa umakini zaidi.

Kutokana na hali hiyo iliyojitokeza ni wazi kuwa viashiria vya ubadhirifu "red flags" vinapaswa kurejewa na kuzingatiwa kwa umakini mkubwa katika Halmashauri na mamlaka nyingine zote hapa nchini ili kuweza kugundua ubadhirifu unaoweza kufanyika katika Fedha za Umma mapema zaidi. Aidha hakuna budi kuimarisha Mfumo wa Udhibiti wa Ndani ili kuzuia ubadhirifu kwa kuhakikisha uwepo wa mgawanyo wa kazi ambao utasaidia kazi ya mtumishi mmoja kuhakikiwa na mtumishi mwingine (Internal Check).

## 4.2 Ushiriki wa Watumishi wa Benki "Collusions"

Katika ukaguzi huu maalum imedhihirika kuwa watumishi wa Benki wasio waaminifu waliweza kushirikiana na watumishi wa Halmashauri kufanya ubadhirifu uliojitokeza. Kwa hali isiyo ya kawaida watumishi wa Benki waliweza kuruhusu kufanyika miamala mbalimbali ambayo ilikuwa ni kinyume na taratibu zilizowekwa kati ya Benki na Halmashauri pamoja na

taratibu za ujumla kwa Taasisi za Fedha. Hali inayoonesha kuwa mbali na kuwa ni sehemu ya udhibiti wa ubadhirifu (third part confirmation) Benki imekuwa ni njia ya kukamilika kwa uzandiki (deceit) wa watumishi wasio waaminifu akiwemo Mweka Hazina Ndg Muhidin Mohamed na Mtunza Fedha Ndg Walugu Musa Limbe. Ubadhirifu mwingi uliofanywa haungewezekana kufanyika bila kuwepo na ushirikiano kati ya watumishi wa Halmashauri na wale wa Benki.

### 4.3 Ukaguzi wa Ndani (Internal Audit).

Halmashauri haikuwa na Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (Chief Internal Auditor) hali iliyopelekea Mfumo wa Udhibiti wa Ndani kuwa dhaifu zaidi**.** Aidha, nafasi hiyo imekuwa ikikaimiwa kwa muda mrefu hali iliyosababisha mapungufu mengi katika utekelezaji wa shughuli za kitengo husika na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa Ndani kwa Uongozi wa Halmashauri.

Ukaguzi maalumu ulibaini kuwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani hakiandai Mpango wa kazi wa Ukaguzi wa mwaka na Mawanda ya utendaji wa mkaguzi wa ndani hayakuwa yameainishwa katika barua yake ya uteuzi, hali ambayo ilipelekea kufanyika kwa kazi zilizo nje ya Ukaguzi wa Ndani kama ukaguzi wa awali (pre- audit) wa hati za malipo.

### 4.4 Ulegevu wa Menejimenti katika usimamizi wa masuala ya fedha

Msimamizi Mkuu wa Rasilimali za Umma katika Halmashauri ni Mkurugenzi Mtendaji. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 33 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982. Ukaguzi maalum wa Halmashauri ya Kishapu umebaini kwamba kulikuwa na kukasimu madaraka kulikozidi kiwango (over delegation) kwa Mtunza Fedha (Cashier) bila kuweka udhibiti (controls). Hii ilisababisha Mtunza Fedha kuweka na kuchukuwa fedha za umma bila kizuizi chochote. Kukosekana kwa udhibiti kulimfanya pia Mtunza Fedha kushirikiana na watumishi wasio waaminifu wa Benki na Halmashauri kufanya udanganyifu.

### 4.5 Muda wa kuwepo katika kituo kimoja cha kazi

Pamoja na nia nzuri ya kubadilisha vituo vya kazi kwa watumishi wa umma ili kuboresha utoaji huduma kwa umma, ubadilishaji huu ukiwa ni kila baada ya muda mfupi unaathiri utendaji.

Ukaguzi Maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu umebaini kuwa uhamisho wa mara kwa mara na kukaimu muda mrefu kwa watumishi walioko katika timu ya Menejimenti kunaathiri uwajibikaji na hatimaye kuzorotesha utekelezaji wa kazi za maendeleo katika Halmashauri. Kwa mfano kwa kipindi cha miaka mitano (5) 2005-2009, Halmashauri ya Kishapu imeongozwa na Wakurugenzi Watendaji wanne (4) tofauti. Hali hii si nzuri kabisa kwa madhumuni ya kujenga mifumo ya udhibiti ya ndani imara.

## SURA YA TANO

## 5.0 MAPENDEKEZO

Kufuatia mambo yaliyoonekana wakati wa ukaguzi huu maalum ikiwa ni pamoja na hatua za kiutawala na kisheria zitakazochukuliwa na Mamlaka husika, ninashauri mambo yafuatayo kwa ajili ya kuboresha hali ya utendaji kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kwa kila upande shirikishi kama ifuatavyo:

### 5.1 Mapendekezo ya ukaguzi kwa OWM-TAMISEMI

- Imeonekana kuwa mabadiliko ya Wakurugenzi na Wakuu wa Idara mbalimbali ya mara kwa mara, pia ukaimu wa nafasi za wakuu wa Idara kwa muda mrefu kama Idara ya Fedha na Ukaguzi wa Ndani umekuwa ni kiini cha kupunguza uwajibikaji hivyo kuathiri mtiririko wa ufanisi katika utendaji. Mamlaka husika Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) inatakiwa kuhakikisha kunakuwepo na utaratibu mzuri wa kuhamisha Wakurugenzi na Wakuu wa Idara ili usiwe wa mara kwa mara, pia nafasi zinapoachwa wazi zisikae muda mrefu bila kujazwa kwa kuwathibitisha wanaozikaimu au kujazwa mapema nafasi hizo na wenye sifa.
- OWM-TAMISEMI ihakikishe kuwa Wakuu wa Idara wanaochaguliwa hasa Kitengo cha Uhasibu kwa maana ya Watunza Hazina wawe na sifa stahiki na uwezo wa kusimamia kitengo hicho kikamilifu. Hii ni pamoja na kuhakikisha uwepo wa msisitizo wa kufuatwa kwa miongozo ya fedha na mgawanyo wa kazi sambamba na mzunguko wa kazi (Job Rotation) wa watendaji katika Kitengo cha Fedha.
- Waweka Hazina wasisitizwe kuhakikisha kuwa Usuluhishi wa Kibenki (Bank Reconciliation) unafanyika kama inavyoelekezwa katika miongozo ya Fedha, na kutoa taarifa sahihi juu ya mapato na matumizi na ikiwa kuna upotevu wowote wa Fedha za Umma uanishwe mara moja kwa ajili ya hatua stahiki.
- Pia taasisi za Fedha (Banks) ambazo zinaingia makubaliano na Halmashauri ziandikiwe maonyo ya kuhakikisha kufuatwa kwa taratibu zilizowekwa katika makubaliano na zile za ujumla katika kulinda Fedha za Umma.
- Aidha watumishi ambao wanathibitika kufanya makosa ni vema wakachukuliwa hatua stahiki mara moja na sio kuhamishwa tu kituo cha kazi ambapo hali hiyo imejionesha kuleta matatizo katika utendaji wa kazi ndani ya baadhi ya Halmashauri zilizokaguliwa.

### 5.2 Mapendekezo kwa Uongozi wa Halmashauri

#### 5.2.1 Kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kiimarishwe kwa kuongezewa watumishi na vitendea kazi kama vile gari na Kompyuta. Hii itasaidia Halmashauri kuimarisha udhibiti wa ndani ikiwa ni pamoja na utunzaji wa vitabu vya fedha na matumizi ya fedha kwa kugundua kasoro zinazojitokeza wakati wa utendaji kazi kama zilivyoonekana wakati wa ukaguzi huu maalum.

#### 5.2.2 Kuimarisha kitengo cha Ukaguzi wa awali (Pre-audit) na matumizi ya IFMS

Halmashauri inatakiwa kuhakikisha kuwa uthibiti wa Mfumo Funganifu Usimamizi wa Fedha (IFMS) unaanzishwa na kuteua watumiaji angalau watano au sita na kuwasomesha kuuelewa mfumo huu na kuwagawia majukumu kwa maandishi ili kuepuka hujuma zilizobainika ambazo zinafanywa na baadhi ya wahasibu wasio waaminifu. Pia inatakiwa marekebisho yote (Adjustments) kwenye mtandao wa Epicor - IFMS yapate idhini kwanza ya Mweka Hazina na Mkurugenzi Mtendaji kwa kuandikiwa Journal Voucher inayoelezea marekebisho hayo, kabla marekebisho yeyote hayajafanywa kwenye mfumo huo.

#### 5.2.3 Uzingatiaji wa Bajeti

- Halmashauri iwe inafanya marejeo ya bajeti katikati ya mwaka (Mid year budget review) kwa fedha za salio la mwaka uliopita kama inavyotakiwa na miongozo toka TAMISEMI ili kuepuka matumizi zaidi (over expenditure) katika baadhi ya vifungu na hesabu za mwisho.

- Halmashauri inatakiwa kuhakikisha mgao wa mapato ya Vijiji ya asilimia 20 yafedha za vyanzo vya mapato vilivyofutwa inapelekwa katika vijiji husika mara tu fedha hiyo inapopokelewa na sio kusubiri muda upite hali ambayo inasababisha fedha hizo kutumika katika matumizi mengine**.**

#### 5.2.4 Kuimarisha Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato

- Uongozi wa Halmashauri uhakikishe kuwa mapato yote yanayokusanywa yanapelekwa benki kwa wakati kama linavyotakiwa na Agizo Na.189 la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya 1997 na mtindo wa kubadilisha hundi kwa fedha taslimu za mapato uachwe mara moja.

- Makusanyo yawasilishwe Makao Makuu ya Halmashauri kila siku au mapema iwezekanavyo na Mtunza Fedha akiri mapokezi baada ya Mhasibu wa Mapato (Revenue Accountant) kukagua makusanyo hayo. Pia, Mtunza Fedha apeleke Benki fedha zote alizopokea kwa kutumia ‘Bank Pay in slips’ ambazo zitaonesha namba za stakabadhi zilizopokelea fedha zinazopelekwa benki.

- Mkurugenzi Mtendaji awe na utaratibu wa kuwa na usimamizi wa karibu zaidi kuhusu mambo yanayohusu fedha za Halmashauri kupitia ripoti za mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima ikiwa ni pamoja na

kudai taarifa za ulinganisho wa daftari la fedha na benki (bank reconciliation statements).

- Kamati ya Fedha, Mipango na Utawala ya Halmashauri pamoja na Kamati ya Ukaguzi (Audit Committee) zitekeleze majukumu yao ya usimamizi na udhibiti wa fedha na rasilimali za Halmashauri kwa kudai na kuzifanyia kazi ipasavyo taarifa za Mweka Hazina na Mkaguzi wa Ndani.

- Halmashauri inatakiwa kuhakikisha kwamba inatumia fursa ya vyanzo vya mapato ya ndani vilivyopo katika Halmashauri na kutumia viwango vya ukusanyaji mapato kama vilivyoainishwa katika miongozo toka TAMISEMI, Sheria Ndogo za Halmashauri na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa.

- Vitabu vya kukusanyia mapato ambavyo havijatumika na vilivyotumika vihifadhiwe kwenye chumba imara (Strong Room) na Uongozi wa Halmashauri uteuwe mtumishi mmoja kwa maandishi ambaye atawajibika na kutunza vitabu vya risiti, kitabu cha kumbukumbu (Counterfoil register) na kuandaa taarifa za kila mwezi za vitabu vya mapato (monthly reports).

- Vitabu vya kukusanyia mapato ya Halmashauri viingizwe kwenye rejista ya mapato kwa kuonesha kumbukumbu ya uagizaji/upokeaji (LPOs na Delivery Notes) ili Halmashauri iwe na uhakika kama vitabu vyote vilivyoagizwa na kulipiwa vimepokelewa na kuingizwa kwenye 'Register' ipasavyo.

### 5.2.5 Kuwa na Utunzaji sahihi wa Hati za malipo

- Hati za malipo zilizolipwa kwa fedha taslimu (DED - Cash) ziwe zinawekwa kwenye faili (Batch) mara baada ya malipo kufanyika na sio kusubiri hadi walipwaji wote walipwe. Mlipaji atumie orodha ya kulipia (Pay list) kuliko kukaa na hati za malipo muda mrefu kabla ya kuziweka kwenye faili husika ambapo mara nyingi husahaulika au kupotea.

- Mtumishi anayehusika na kuweka hati za malipo kwenye mafaili (batches) ahakikishe anaziweka kwa wakati pindi zinapotoka kuandikiwa hundi, kuliko kuzikusanya hati hizo ili ziwe nyingi kwenye boksi ndipo aziweke kwenye mafaili husika. Hii ni moja ya sababu za upotevu wa hati za malipo.

- Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuteua Mtumishi mmoja kwa maandishi, ambaye atahakikisha hati zote za malipo zinakuwa na viambatanisho vyake na hati hizo zinatunzwa katika hali ya usalama na kuhakikisha kwamba anaratibu mienendo ya hati zote kuwa zinapochukuliwa zinakuwa zimekamilika. Pia Halmashauri itayarishe chumba maalum kwa ajili ya kuhifadhi hati za malipo na Mtumishi huyo awajibishwe kwa upotevu wowote utakaojitokeza.

- Uongozi wa Halmashauri uimarishe ufanyaji wa usuluhisho wa Benki (Bank Reconciliation) ambapo inatakiwa ufanywe kila mwisho wa mwezi na taarifa hizo ziwasilishwe kwa Mkurugenzi Mtendaji na Kamati ya Fedha, Mipango na Utawala.

### 5.2.6 Kuimarisha Kitengo cha Mishahara

Kitengo cha mishahara kiimarishwe kwa lengo la kushughulikia masuala ya mishahara kwa uangalifu na kwa haraka ili kupunguza au kuzuia kabisa mapungufu yaliyojitokeza hasa kushindwa kurejesha mishahara isiyolipwa kwa wakati, kuchelewa kulipa makato ya kisheria na hiari na kufuta majina ya wasiostahili kulipwa mishahara kwenye orodha ya wanaolipwa mishahara kwenye Halmashauri.

### 5.2.7 Kuimarisha usimamizi wa manunuzi ya Umma katika Halmashauri

- Kila idara inayohitaji kufanya manunuzi ya huduma au vifaa iwasilishe maombi kwenye kitengo cha usimamizi wa manunuzi (PMU) ambacho ndicho kinahusika na kinajua ni taratibu zipi za kufuata katika manunuzi. Utaratibu wa Wakuu wa Idara au vitengo kwenda kutafuta nukuu za bei "quotations" na hata kufanya manunuzi wenyewe ukomeshwe kuepukana na uvunjwaji wa sheria, kanuni na utaratibu wa manunuzi ya umma.
- Halmashauri inatakiwa kutumia nyaraka za zabuni (Tender Documents) na vigezo vya uchambuzi wa Zabuni (Tender Evaluation Criteria) zinazotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA).
- Uongozi wa Halmashauri uhakikishe kuwa Sheria na Kanuni za Manunuzi zinazingatiwa kwa kuhakikisha kuwa vifaa vyote vinavyonunuliwa vinakaguliwa na vinaingizwa katika leja na manunuzi yote yanayofanywa yanaidhinishwa kulingana na viwango vya uidhinishaji.

### 5.2.8 Manunuzi na matumizi ya mafuta

Halmashauri inafanya manunuzi ya mafuta kwa ajili ya matumizi kwa ku-deposit fedha kwenye vituo vya mafuta na magari yanajaza mafuta kadri yanapotakiwa lakini mafuta yanayochukuliwa yalikuwa hayaingizwi kwenye "log books". Halmashauri inashauriwa kuwa na "log books" ili kurekodi mafuta yanayojazwa kwenye magari na kilomita zinazotumika na ukaguzi wa "log books" hizo ufanyike mara kwa mara na Afisa Usafirishaji/Mkaguzi wa Ndani.

### 5.2.9 Utekelezaji na Usimamizi wa miradi ya Maendeleo

- Halmashauri inatakiwa iongeze jitihada katika usimamizi na utekelezaji wa miradi kwa kutumia fursa ya rasilimali fedha inayopata kwa kufuata mipango kazi wake iliyoidhinishwa. Pia, Halmashauri inatakiwa kupeleka fedha za miradi vijijini kwa wakati ili kuepuka kubakia na fedha nyingi za miradi mwisho wa mwaka, hali ambayo inarudisha nyuma maendeleo ya wananchi wa Kishapu.

- Halmashauri inatakiwa kuhakikisha kuwa fedha zinazopelekwa (transfers) katika kata, vijijini, mashuleni, zahanati n.k. zisifanywe kama matumizi moja kwa moja mpaka ziwe zimetumika kwa shughuli husika, na kama hazijatumika zionyeshwe katika hesabu za mwisho wa mwaka kama salio (Cash and Cash Equivalent balance) kama inavyotakiwa na mwongozo wa TAMISEMI wa ufungaji wa hesabu kwenye Halmashauri uliotolewa Septemba, 2009.

- Kuna mwamko mdogo wa wananchi katika kujitolea na kuchangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo inatakiwa kuchangiwa asilimia ishirini (20%) ya gharama ya mradi. Halmashauri iendelee kuhamasisha wananchi kuchangia maendeleo ya miradi yao ili uchumi wa Wilaya na Taifa kwa ujumla uboreshwe.

- Wakati wa utekelezaji wa miradi kumebainika kuwa na mapungufu mengi ikiwa ni pamoja na kazi mbalimbali kutokamilika, kutokuwa na viwango vya ujenzi vya kuridhisha, kutofuatwa kwa miongozo. Halmashauri inatakiwa kusimamia kwa karibu zaidi utekelezaji wa miradi kwa kumhusisha Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya katika miradi yote.

- Halmashauri inatakiwa kuandaa mikataba kulingana na maelekezo yanayotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ili kuhakikisha vipengele/vifungu vyote muhimu vinakuwemo kwenye mikataba inayoingiwa na wakandarasi mbalimbali. Pia, Halmashauri ihakikishe kuwa usanifu wa miradi ikiwemo kuandaa michoro na orodha ya vifaa na bei (BOQs) zinaandaliwa kikamilifu ili kuondoa matatizo wakati wa ujenzi kama vile ilivyojitokeza kwa kazi za ziada.

- Halmashauri inatakiwa kuhakikisha kuwa nyaraka na zote muhimu na miradi zinakuwemo katika majalada ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu utekelezaji wa miradi zinapohitajika.

### 5.2.10 Kutolewa Taarifa za Fedha kwenye vikao vya Uongozi (CMT)

Uongozi wa Halmashauri uhakikishe kuwa Taarifa za Fedha zinatolewa kwenye vikao vya CMT pamoja na kuhakikisha kuwa uhamisho wa Fedha unafanyika kwa mujibu wa miongozo na kanuni za utunzaji wa Fedha.

Aidha Wakuu wa Idara wahakikishe kuwa wanapatiwa taarifa za mapokezi ya Fedha za Miradi kwa wakati stahiki na kuhakikisha wanasimamia utekelezaji wake sambamba na kufuatilia mwenendo wa matumizi ya Fedha ili kuhakikisha kuwa hakuna upotevu wa Fedha hizo au kuelekezwa katika maeneo yasiyostahiki kinyume na utaratibu.

### 5.2.11 Umuhimu wa Halmashauri kuwa na mpango endelevu wa mafunzo

Halmashauri ziwe na utaratibu wa kutenga fungu la fedha kwa ajili ya mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani hasa Kamati ya Fedha, Mipango na Utawala pamoja Menejimenti na wafanyakazi wote wa Halmashauri. Hivyo, kwa umuhimu mkubwa wa Halmashauri kuwa na mikakati endelevu ya mafunzo.

### 5.2.12 Hatua stahiki dhidi ya watumishi wa Halmashauri waliohusika na ubadhirifu

Hatua stahiki za kisheria/kiutawala zichukuliwe dhidi ya watumishi waliotajwa kuhusiana na ubadhirifu wa fedha zilizoonekana katika vipengele mbalimbali vya taarifa hii ambao pia baadhi wametajwa katika barua yenye Kumb.Na. KDC/C.A/30/3/32 ya tarehe 3/9/2010 iliyoandikwa na Mkurugenzi wa Halmashauri kwenda kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga kati ya wahusika hao ni pamoja na:

- Mtunza Fedha (Cashier) Bw. Walugu Mussa Limbe.
- Watumishi/Mtumishi wa NMB Tawi la Manonga Shinyanga.
- Mweka Hazina wa Halmashauri Bw. Muhidini Mohamedi.
- Boniface Nkumingi.
- Mhandisi wa Halmashauri Bw. Leonard Mashamba.

## 5.3 Mapendekezo kwa Waheshimiwa Madiwani

- Waheshimiwa Madiwani wanasisitizwa kuhakikisha kuwa Taarifa zinazoletwa kwao zinajadiliwa kwa kina ili kupata kuzielewa na kupata maainisho ya hali ya utekelezaji halisi wa miradi ya maendeleo ikiwemo miradi ya ujenzi. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanapatiwa taarifa husika mapema kabla ya vikao.
- Pia kupitia Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi wahakikishe kuwa wanapatiwa taaarifa za Fedha za Miradi za robo mwaka na kuelewa matumizi yake pamoja na salio anzia na salio ishia katika vikao vyao ili kufuatilia na kutoa ushauri na mapendekezo endelevu ya utekelezwaji wa miradi ya maendeleo. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa madiwani wanakuwa na ari ya ufuatiliaji wa mienendo ya mambo katika kuimarisha maslahi ya Halmashauri na Taifa kwa ujumla.
- Aidha Kamati ya Fedha, Mipango na Utawala iundwe na Madiwani wenye sifa na uwezo mkubwa wa kuchambua masuala ya Fedha na Mipango ili kufuatilia kwa karibu na kupata taarifa sahihi kwa ajili ya Baraza la Madiwani (Full Council) na wananchi kwa ujumla.
- Kuimarisha mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani ili kuboresha uwezo wa kuisimamia Halmashauri katika masuala ya fedha, utawala bora na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- Kuna umuhimu mkubwa kwa Waheshimiwa Madiwani kupata mafunzo ya utawala na usimamizi wa mali na fedha za Halmashauri. Kamati ya

Fedha, Mipango na Utawala ipewe kipaumbele katika kuelimisha kuelewa hesabu, taarifa za fedha na bajeti za Halmashauri.

### 5.4 Pendekezo kwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)

Waheshimiwa Wabunge kupitia Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) wanaombwa kusisitiza kuchukuliwa hatua stahiki kulingana na matokeo ya ukaguzi pamoja na kuhakikisha kuwa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanazingatiwa kikamilifu kwa kutoa maagizo mbalimbali kwa Uongozi wa Halmashauri na Serikali kwa ujumla.

## SURA YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

Tarehe 13/07/2011 kilifanyika kikao cha pamoja (Exit meeting) ambacho kilihudhuriwa na Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu chini ya Uongozi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri pamoja na wawakilishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wakiongozwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga.

Mambo yote muhimu yaliojitokeza wakati wa ukaguzi huu yaliwekwa bayana na kuzungumziwa kwa kina. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu na Uongozi wa Mkoa waliahidi kuyashughulikia ipasavyo mambo yote yaliyobainishwa na ukaguzi huu maalum.

Kutokana na wingi wa viambatanisho na vielelezo kuhusu ripoti hii hatukuweza kuviweka katika taarifa hii ya Ukaguzi Maalum, hata hivyo, viambatanisho na vielelezo hivyo vinapatikana Makao Makuu ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kama vitahitajika.

Ludovick S. L. Utouh
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

Nakala:-

(i) Katibu Mkuu,
TAMISEMI,
S.L.P 1923,
**DODOMA.**

(ii) Mh. Mkuu wa Mkoa,
Mkoa wa Shinyanga,
S.L.P. 320,
**SHINYANGA.**

(iii) Mh. Mkuu wa Wilaya,
Wilaya ya Kishapu,
S.L.P. 1288,
**KISHAPU.**

(iv) Mh. Mwenyekiti,
Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu,
S.L.P. 1288,
**KISHAPU.**

(v) Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashuri ya Wilaya ya Kishapu,
S.L.P. 1288,
**KISHAPU.**

(vi) Mkaguzi Mkazi,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
S.L.P. 219,
**SHINYANGA.**